BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	**Mhe.**	**Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**

9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii,**
			na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi,**

			Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**

29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Uwezeshaji,**	**-**	**Naibu Waziri wa Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe. Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe. Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe. Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe. Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe. Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe. Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe. Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe. Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe. Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe. Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe. Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe. Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe. Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

49.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**

83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem	**-**	**Katibu**

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 09 Mei, 2018

(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kabisa nichukuwe nafasi hii kuwakaribisha sana katika Mkutano wetu huu wa Kumi wa Bajeti wa Baraza letu la Tisa ambao unaanza leo tarehe 09 Mei, 2018.

Waheshimiwa Wajumbe napenda kutoa kwenu na kwa Wananchi kwa ujumla taarifa kuhusu Miswada ya Sheria iliyopitishwa katika Mkutano uliyopita wa Baraza uliofanyika kuanzia tarehe 07 mpaka tarehe 28 Februari, 2018. Katika Mkutano wa Tisa wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Baraza lilipitisha Miswada 3 ya Sheria kama ifuatavyo:-

1. Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya mwaka 1995 na Kutunga Sheria Mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Kuweka Masharti bora Zaidi pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

2. Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya mwaka 2004 na Kutunga Sheria Mpya ya Adhabu Kuweka Msharti bora Zaidi pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

3. Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Mwenendo wa Jinai Nam. 7 ya mwaka 2004 na Kutunga Sheria Mpya ya Mwenendo wa Jinai na Kuweka utaratibu bora wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Usikilizaji wa Kesi za Jinai na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 91(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakiilishi Toleo la 2016, naomba kutowa taarifa kwamba Miswda yote hiyo niliyoitaja sasa imekuwa Sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na Vijalizo vyake kuanzia tarehe 29 Februari, 2018 naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2018/2019 naomba kuwasilisha.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati Mezani ya Hotuba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa fedha 2018/2019. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 17

Mgao wa Majiko Salama Kupunguza Athari za Mazingira

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Kny. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Hivi karibuni Kampuni ya *Export Group* ni iligawa majiko salama huko Mahonda kwa ajili ya kupunguza athari za kimazingira pamoja na kutoa elimu ya utunzaji mazingira.

(a) Kwa nini elimu na mgao huo umetolewa Mahonda tu.

(b) Kuna utaratibu gani wa mpango huo ukaenea katika maeneo mengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 lenye vifungu (a) na (b) naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-
Mhe. Spika, *Export Trading Group of Farmers* ni NGO ambayo inaundwa na wanachama mbali mbali wenye mashamba ya miwa na viwanda vya sukari Tanzania ikiwa ni pamoja na Kiwanda cha Mahonda Zanzibar. Kuanzia mwaka 2014 hadi mwaka 2016, NGO hii ilianzisha utaratibu wa kutoa misaada ya majiko sanifu yenye kutumia nishati ya *'ethanol'* kwa lengo la kupunguza uharibifu wa misitu na uzalishaji wa hewa ya ukaa (*Carbon Dioxide*).

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Mgao wa majiko hayo ulitolewa katika Wilaya tano za Unguja ambapo jumla ya majiko 139 yalitolewa kama ifuatavyo: Wilaya ya Kaskazini 'A' (majiko 10); Kaskazini 'B' (majiko 25); Magharibi A na B (81) na Wilaya ya Mjini (Majiko 23).

Aidha, mwaka 2017 NGO hiyo ilianzisha programu ya kuelimisha wanafunzi wa Kidato cha Nne juu ya uhifadhi ya mazingira kwa Skuli ambazo zipo jirani na viwanda vya Sukari. Programu hiyo pia ilihusisha mdahalo wa wanafunzi wa Skuli hizo ambao pia walipewa zawadi ya majiko hayo. Kwa kuwa kiwanda cha Sukari Zanzibar kipo Mahonda hivyo Skuli ya Mahonda ilipata bahati hiyo ambapo jumla ya wanafunzi 17 walipatiwa majiko hayo.

(b) Mhe. Spika, NGO hiyo hivi sasa inaendelea kuhamasisha nyenzo za kuendeleza programu hii katika maeneo mengine ya Unguja na Pemba. Kwa upande wa Serikali hivi sasa inaendelea na programu za kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutumia majiko sanifu na ambayo yanatumia gesi kwa nia ya kupunguza ukataji ovyo wa miti, ili kuweza kulinda afya na uhifadhi wa mazingira.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza niipongeze NGO hizi au hii kwa kazi nzuri wanayoifanya jinsi ya kuhakikisha mazingira yetu hayaharibi katika maeneo yetu, lakini pamoja na majibu hayo kwamba Wilaya 5 zimefaidika ikiwemo ya Magharibi B na A mfano.

Je ni Shehia gani zimefaidika kutokana na mgao huo pia kupata elimu juu athari ambazo zisitokee huko mbele tunakokwenda.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza (a) na (b) kama yafuatayo:-

NMhe. Spika, nitayajibu yote mawili kwa pamoja. Kama ambavyo nimesema NGO hii imeanza kuasisiwa mwaka 2014 na bahati nzuri waasisi wa lengo hili ni wenzetu wawekezaji wa Kiwanda cha Mahonda, ambao wao kupitia uwekezaji wao waliona sasa kila *product* ambayo wanaizalisha katika Kiwanda kile isitumike tu kama *west product* au isitumike tu kama mabaki lakini pia iweze kutumika kwa dhamira ya kutaka kuzalisha jambo. Sasa mabaki ya miwa yale maganda yake ndio inayopatikana *ethanol* hii sasa wakaona si jambo zuri kuitupa ndio maana wakaja na *program* hii lakini jambo kubwa ni kuhakikisha tunaweza kunusuru mazingira yetu, lakini sheria tunayotumia mpaka sasa tulikuwa tunajaribu kutumia taratibu na ushauri ambao tulioupata kutoka Idara ya Mazingira ambao pia nao waliweza kushauri namna bora ya kufanya ya kuweza kutunza mazingira yetu.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa jibu lake na niwapongeze hawa Kampuni kwa kuanza utaratibu huu, swali langu kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Jimbo la Mfenesini ni watumiaji wakubwa wa kuni na kuharibu mazingira na kwa kuwa Mahonda na Mfenesini ni jirani Shehia gani ya Jimbo la Mfenesini ambayo imefaidika na mradi huu na kama bado kuna mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Mfenesini.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake la nyongeza (a) na (b) kama yafuatayo:-

Mhe. Spika, majiko haya katika maeneo mengi yalikuwa yanatolewa katika *level* za Kiwilaya ndio maana tumetoa idadi ya majiko 81 katika Wilaya za Magharib 'A' na 'B' lakini ndani ya Wilaya hizi mna Shehia nyingi ambazo zimenufaika lakini pia Mheshimiwa Spika kwa ruhusa yako na kwa ridhaa yake tunanajua Jimbo la Mfenesini ni miongoni mwa Majimbo yaliyokuwepo jirani na bahati nzuri yawezekana wakawa hawajaanza kunufaika na suala la kupata majiko lakini tayari Mfenesini kupitia Kiwanda cha Mahonda tayari wakulima wake washaanza kuwezeshwa miwa kupanda miwa na wanapewa kila kitu ili kuweza kupata uzalishaji bora. Kwa hiyo yawezekana kama hawajanufaika na hili tayari washaanza kunufaika na jambo jengine kupitia mabonde ya walokuwa nayo katika Jimbo lao.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba kwa mgao uliofanyika ni kwa Wilaya 5 za Unguja lakini Mheshimiwa Spika, na Pemba nako mazingira yanapotea siku hadi siku yanakuwa yanaharibika na pia kuna wengine wananchi wetu wanatumia hadi kuni za Mikarafuu na ambao ndio zao letu la taifa.

Je Wizara yako inampango gani wa kuhakikisha Pemba nako wamepata majiko hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza kama yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza nakubaliana fika na jambo ambalo amelisema Mheshimiwa Mwakilishi kwamba Pemba bado tuna tatizo la athari ya mazingira ambalo linatokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na hili linatokana na namna ambavyo jamii imekuwa ikitumia *resource* ya kuni za mkaa katika kurahisisha mambo yetu nyumbani, lakini hili ambalo amelisema, bahati nzuri amelisema yeye mwenyewe kwanza Serikali imepiga marufuku kwa namna yoyote kuweza kukata mti wa mkarafuu kwa dhamira ya kutumia katika mazingira ya kuni ikiwa bado haujafikia katika *level* yake kwa hio hili tunaomba tushirikiane naye Mheshimiwa Mwakilishi lazima twende tukawape elimu wenzetu

waliopo katika Kisiwa cha Pemba. Mti wa mkarafuu ni *resource* kubwa sana katika Taifa letu na katika uchumi wetu sasa tunaomba tushirikiane nae katika kutoa elimu hiyo.
Lakini pia tumesema jambo hili limeanza katika Wilaya 5 za Unguja tunategemea litakapokuwa katika mazingira mazuri pia Pemba litafika kwa hiyo tunaomba atustahamilie mwendo huu mdogo mdogo lakini tutafika ipo siku tutafika katika jimbo lake la Ziwani. Nakushukuru Mhe. Spika.

Nam. 1

Uimarishaji wa Barabara za Ndani Tunguu

Mhe. Simai Mohammed Said – Aliuliza:-

Serikali imekata viwanja katika maeneo ya Tunguu mji mpya pamoja na Jumbi mji mpya, ambapo kwa sasa panaelekea kuwa ndio Makao Makuu ya Mkoa wa Kusini hasa ukizingatia ofisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar nyingi kuwepo katika maeneo hayo.

Je, ni lini Serikali itaboresha barabara za ndani katika maeneo ya Tunguu pamoja na Jumbi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la wananchi Tunguu swali lake Nam. 1 kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Nam. 7 ya mwaka 2014, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepewa jukumu la kuzifanyia matengenezo barabra za ndani (*feeder roads*) ziliomo katika maeneo yake ya utawala zikiwemo barabara za Jumbi na Tunguu. Katika kutekeleza jukumu hilo mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kuzifanyia matengenezo barabara hizo katika kiwango cha kifusi. Hata hivyo, kwa kuwa barabara zinazohitaji kufanyiwa matengenezo hayo ni nyingi ukilinganisha na uwezo wa halmashauri kifedha, kasi ya matengenezo ya barabara hizo imekua ndogo mno.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo naomba kumjibu Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali inaelewa umuhimu wa kuwepo kwa barabara zinazopitika kirahisi wakati wote katika maeneo ya Jumbi na Tunguu maeneo ambayo yanaonekana kukuwa kwa kasi kubwa kutokana na kuwepo kwa Taasisi nyingi za Serikali na kupanuka kwa makaazi ya watu.

Mhe. Spika, pamoja na kulielewa hilo, Serikali haina mpango wa kuzifanyia matengenezo barabara hizo katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 kutokana na uhaba wa fedha ambazo Serikali imezipata kwa ajili ya matengenezo ya barabara za ndani.

Hata hivyo, Serikali itaendelea kutoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka kipaumbele cha matengenezo ya barabara za ndani kwa kutumia fedha zake za ndani. Nachukua nafasi hii vilevile kutoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kushirikiana na Serikali za Mitaa katika matengenezo ya barabara hizo kwa kutumia fursa mbali mbali ikiwemo Mifuko ya Majimbo.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Spika, ahsante sana, pamoja na majibu ya wastani ya Mhe. Waziri, maana yake ingekuwa majibu mazuri angekuwa kanipa tarehe lini atafanya matengenezao. Kwa hivyo, haya sisemi kama ni majibu mazuri, lakini nimuulize swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, moja ya azma ya serikali ni kuhakikisha kuendeleza maeneo kama haya hasa ya Tunguu na Jumbi, wananchi kwa kweli wameitikia agizo la serikali na ukiangalia kwa eneo la Tunguu na Jumbi wananchi wengi kuna nyumba zaidi ya 400 sasa hivi ziko tayari kuhamiwa lakini imekuwa ni mtuhani.

Sasa je nimuulize Mhe. Waziri ni kwa nini serikali imewaruhusu wananchi kuendeleza kujenga wakati ikitambua juu chini kwamba hawa watakuwa tayari kuendeleza barabara hizi.

b) Kwa nini Wizara yake haoni akafanya mazungumzo na Serikali kuu ili kuhakikisha kwamba hizi barabara za ndani ambazo zina umuhimu sana kwa wananchi wa maeneo ya Tunguu na Jumbe, zikafanyiwa angalau ukarabati wa haraka hasa ukizingatia barabara ya IPA kuelekea ndani, barabara ya Mzee wa Kazi kuelekea kwa upande wa Jumbi, pamoja na ISTIKAMA kuelekea ZU, hizi angalau zikafanyiwa matengenezo ya haraka kwa kupitia mfuko wa kuomba fedha katika Serikali kuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza naomba nitoe maelezo mengine ya ziada kwamba Mheshimiwa sio kwamba Serikali imekataa kuzijenga barabara hizo za ndani kama vile ambavyo ungetaka wewe Mheshimiwa pamoja na wananchi wetu, lakini tulichokisema ni kwamba kwa mwaka wa 2018/19 bajeti yetu haina mpango kabisa au hatuna mpango katika kuzifanyia matengenezo barabara hizo, badala yake tumekuomba Mhe. Mwakilishi tusaidiane kushirikiana na Serikali kwa kupitia mifuko mbali mbali pamoja na mfuko wa Jimbo kama nilivyotangulia kusema.

Lakini pale itakapokuwa hali itakuwa inaruhusu Serikali haikatai kabisa kuzijenga barabara hizo na nyengine ambazo zitaweza kujitokeza, kwa hivyo kiufupi Mheshimiwa niombe kutoa maelekezo kwamba uwezo wa kuwaruhusu wananchi waendelee kujenga

ni sehemu nyengine, lakini vile vile na utekelezaji wa ujenzi wa barabara ni kwamba Serikali itaendelea kufanya kazi hiyo pale itakapoona kwamba fursa ipo kama ambavyo nimesema barabara ziko nyingi.

Kwa hivyo Mheshimiwa naomba kwa hili tuendelee kushirikiana na uweze kuvuta subira kidogo ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ya kukiri kwamba Serikali haijapanga bajeti kwa ajili ya kutunza barabara za ndani za mji wa Tunguu, mimi nataka anisaidie suala dogo tu. Kwa kuwa katika kipindi hichi cha masika imejitokeza *jam* nyingi katika barabara ambazo tunazitegemea na tulikuwa tuna barabara za asili ambazo tumekuwa tunaona zina mitihani yake ambazo zingetusaidia katika kurahisha kuondosha *jam* katika hayo maeneo tuliyoyazoea za barabara za asili.

Kwa mfano kama tungetengeneza barabara ya Mpendae/Jang'ombe ama maeneo mengine mengi yamejitokeza, nilitaka kujua tu bajeti waliyojipangia kwa mwaka huu wanategemea kutengeneza barabara za ndani katika maeneo gani, naomba anitajie hayo maeneo ambayo wametegemea kwa bajeti ya mwaka huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi alitaka kujua ni kwa barabara zipi ambazo tunakusudia kuzijenga katika kipindi hichi cha bajeti, kwa hivyo niombe tu kwa kuwa mkutano huu ni bajeti ya Serikali naomba sana Mheshimiwa avute subira kidogo ili pale bajeti yetu itakapoanza kusomwa tutaweza kubainisha ni barabara ipi na ipi ambayo tutaweza kuijenga. *(Makofi)*

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali za mitaa ni wajibu wake kutengeneza barabara za ndani kwa mujibu wa sheria na kwa kuwa Mhe. Waziri katika majibu yake ametaka wawakilishi washirikiane na Serikali za Mitaa katika metengenezo ya barabara hizo. Swali langu je Wizara yake ina mpango gani kwa zile barabara ambazo tayari zimeshatengenezwa kwa kiwango cha kifusi kwa kushirikiana na Manispaa pamoja na Mwakilishi ili kuweza kutia lami barabara hizo, hasa ikiwemo ya Shakani, Chukwani, Buyu wakati tayari imeshatengenezwa kwa kiwango cha kifusi ili isije ikatokea ile kadhia ya kile kifusi kikaondoshwa na maji.

Ni lini Wizara yake inaweza ikatia lami barabara zilizotengenezwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Naomba kutoa majibu ya ziada ya swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Muwakilishi wa Jimbo la Chukwani kwa kazi nzuri ambayo anakuwa akiifanya katika kutatua kero za wananchi wake, kwa kuwa ni karibuni tu barabara hiyo ambayo ameitaja ametoa mchango mkubwa katika kufanikisha adhima hiyo ya kutatua kero za wananchi amefanya jambo moja zuri sana.

Naomba nimtoe wasi wasi Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali kupitia Manispaa zetu ama Halmashauri zetu tuna malengo mazuri ambayo ya kuweza kuhakikisha kwamba hiyo miundombinu iliyojengwa tunailinda katika kuirekebisha ili iweze kupitika na iweze kuwa na ubora zaidi na kuchukua muda mrefu. Kwa sasa hivi ni kwamba Serikali Mhe. Rais ametoa maagizo mbali mbali ya kuwakutanisha baadhi ya viongozi wakuu wa Wizara ili kukaa kutafuta namna ya kuangalia upatikanaji wa fedha. Kwa hivyo pale ambapo fedha zitapatikana Mheshimiwa nikutoe wasi wasi kwamba kazi hiyo tutashirikiana kama vile ambavyo tumeshirikiana kuweza kuendeleza kuona kwamba tunaifanya kazi hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza kwenye Wizara hii, kwanza nimpongeze sana Waziri kwa majibu yake marefu sana ambayo tukitafuta uhalisia maeneo gani ambayo Serikali imefanya kazi hii pia hatujayapata, lakini niishukuru Serikali kwa jitihada zake kwa kutengeneza barabara hizi za ndani.

Lakini kwa kuwa Mhe. Waziri unaelewa fika kwa majukumu ya barabara za ndani ziko kwenye Halmashauri, Manispaa na Mabaraza ya miji kwenye jukumu la msingi.

a) Sasa nilikuwa nataka kujua kwa bajeti hii 2016/2017 ni Manispaa zipi zilizotenga bajeti ya kutengeneza barabara za ndani kwa ajili ya kuwatengenezea wananchi.

b) Lakini ni maeneo gani pia yaliyonufaika kutengenezwa kwa mwaka huu wa fedha ambao unaishia sasa hivi.

Mhe. Spika: Samahani Mhe. Waziri Waheshimiwa wajumbe nadhani kumuuliza waziri aelezee bajeti ambayo atakuja kutusomea hapa ni kuwahisha shughuli za Baraza, nadhani tungesubiri kwa sababu hii Wizara katika hizi za mwanzo ambazo zitakuwa zinawasilisha bajeti yake tutakuja kujua ule mpango mzima na maeneo yepi ambayo yatakuwa yananufaika.

Kwa hivyo naomba tuendelee swali kwa Wizara hii hii.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashkuru sana Mhe. Spika, na mimi awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukarudi salama hapa Barazani.

Nimuulize Waziri kwamba katika bajeti iliyopita aliniahidi kwamba njia yangu ya Msingini.

Mhe. Spika: Mheshimiwa ni swali la msingi una swali No. 166 sio swali la nyongeza.

Nam. 166

Uendelezaji wa Vyoo Vya Nje Vya Miji

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Katika kuendeleza Miji ya Zanzibar kuna mambo mengi ya maendeleo ambayo kwa kipindi sasa yameondoka kama vile katika Mji wa Chake kulikuwa na vyoo vya Mji vya kujisaidia maeneo mengi kama vile Stendi ya Chake Chake, Banda la taka, Msingini karibu na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Chake Chake, na pia kulikuwa majumba ya starehe kama Sinema na vitu vyote vyengine havipo tena.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvirudisha vyoo vya asili vilivyokuwepo zamani katima Mji wa Chake Chake.

(b) Je, vyoo hivyo maeneo yake bado yapo kama hayapo Wizara inasemaje.

(c) Je, kama Serikali haina mpango tena wa kujenga je, itampa mtu binafsi eneo lingine.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 166 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, naomba kulieleza Baraza lako Tukufu kuwa katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu kama vile stendi ya magari ya Chake Chake, soko kuu la matunda na mboga la Chake Chake, soko la Tibirinzi na soko la matunda na mboga la Machomane, vyoo vya Serikali vipo. Ama kwa upande wa eneo la Bandataka, Msingini na karibu na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hakuna mpango wa kuvirudisha tena vyoo hivyo kwani kwa sasa hakuna mazingira mazuri ya kufanya hivyo na vipo vyoo vya kutosha katika maeneo hayo.

(b) Mhe. Spika, baadhi ya maeneo hayo yako wazi na baadhi yametumika kwa shughuli nyengine za kijamii.

(c) Mhe. Spika, Serikali inao mpango wa kuimarisha huduma za vyoo vya asili vilivyopo na pia inao mpango wa kujenga vyoo vipya. Aidha, Serikali inakaribisha watu binafsi kuwekeza katika sekta hiyo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nataka nimwambie Mheshimiwa kwamba Chake Chake ni mji namba mbili kwa ukubwa au katika upanuzi ambao sasa hivi ndio unakua. Suala la hapo miaka ya nyuma Chake Chake ilikuwa na vyoo vizivyopungua saba katika mji na wakati *population* ilikuwa ndogo sana. Leo Waziri anasema kwamba kwenye soko la mboga mboga kuna vyoo na katika sehemu nyengine.

Lakini nataka nimwambie katika mji wa Chake Chake ulioko *Centre* pale *Stand* hapana vyoo watu wengine wanafika *time* wanakwenda kunywa kahawa kwa kuzuia choo.

a) ninachoomba kumuuliza Waziri kwamba maeneo ya Msingini ambayo ni maeneo yanakua na maeneo mengine ni sababu zipi zilizofanya kwamba pale visijengwe vyoo mpaka ukaombe nyumba ya mtu.

b) Lakini suala la pili ilikuwa Mheshimiwa kama ameruhusu watu binafsi wajenge na yeye ameshakataza je ruhusa hiyo itatoka wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa naomba nirejee majibu yangu kwamba katika maeneo ambayo nimeyataja vyoo vipo na kwa bahati njema sana Mhe. Spika, nimefika katika maeneo hayo na nimeshuhudia mimi mwenyewe, na pale ambapo nimesema palikuwa na vyoo havitumiki Mheshimiwa ni sahihi kabisa vyoo hivyo havipo tena na kwa sababu kutokana na kwamba hakuna haja za kitaalam ambazo zinaonesha kwamba kuna haja ya kujengwa vyoo kwa sababu ni tayari maeneo hususan katika barabara ya Msingini, pana makaazi ya watu ambao hakuna mwelekeo au hakuna viashiria ambavyo vinaonekana kwamba kuna umuhimu wa kuwepo vyoo katika eneo lile pale.

Kwa hivyo Mji ule tunauangalia katika mazingira kama alivyosema mwenyewe Mhe. Mwakilishi mji wa Chake Chake ni mji namba mbili kwa ukuwaji na mimi naomba nikiri kwa hilo, lakini ninachokisema ni kwamba Mheshimiwa tumepata ushauri tumefanya utafiti mbali mbali yale maeneo kama tunahitaji kuongeza vyoo tutaongeza kwa mujibu wa maelekezo. Lakini vyoo katika maeneo hayo vipo kama havijatosheleza tutashirikiana katika kuona kwamba tunatoa huduma hiyo ili wananchi wetu muendelee kufaidika wala asipate tatizo lolote.

Mhe. Spika: Swali la nyongeza kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nitoe majibu ya ziada kwa Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake, kabla sijatoa majibu hayo kwanza nataka nimpongeze sana Naibu Waziri wa Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, kwa majibu mwanana kabisa ambayo ameyajibu na hususan kwa

sababu akijibu masuala yeye huwa anafanya utafiti kwanza kwa kwenda *site* kabla ya kujibu hapa. Kwa hivyo nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri.

Nataka niseme kwamba kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba maeneo anayoyataja ya Msingini maeneo hayo sasa yameshonana sana na hizo nyumba za makazi ya watu. Sasa Serikali inao mpango mkuu wa *master plan* ya miji miongoni mwa miji ambayo ipo katika mpango huo ni mji wa Chake Chake kwa kuzingatia suala hilo hilo suala la kwamba ni mji wa pili kwa ukuwaji wa Zanzibar. Sasa tusubiri hapo *Master Plan* itakapokamilika itatuelekeza katika maeneo gani mengine ambayo yanahitaji yajengwe *public toilet* au vyoo vya wananchi vya nje. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, katika vituo vya daladala vyote hakuna vyoo au asilimia 99.9% hakuna vyoo pamoja na kwamba Mhe. Waziri kasema kwamba tunasubiri *Master Plan* mpya sijui mwaka gani, Je hajui sasa hivi kuna maendeleo yametokea katika nchi mbali mbali kuna vyoo vya muda vya kuwekwa na kuondoka. Haoni kama ipo sababu ya kufanya hivyo hasa tukizingatia maradhi mbali mbali yanayojitokeza na watu wanapokutwa na shida ya kujisaidia wakati wowote ili kuhatarisha maisha yao.

Je, ana mpango gani wa kutafuta vyoo hivyo ambapo hapa hapa Zanzibar ukienda baadhi ya maeneo unavikuta.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa naomba nikiri kwamba nikubaliane nae kwamba umuhimu wa kujenga vyoo katika maeneo ya vituo vya daladala ni jambo la msingi sana ili kuepusha hiyo hali ambayo inaweza kujitokeza hususan katika kipindi hichi cha mvua. Lakini vile vile katika jibu langu la msingi nimesema kwamba au na Mheshimiwa pia ameongezea kusema tunasubiri *Master Plan* ituelekeze namna gani kwamba tuweze kujenga hivyo vyoo, lakini kwa hatua ya haraka haraka Mhe. Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa kwamba Halmashauri ama Manispaa zetu tukishirikana na yeye ni vyema tuwe na mashirikiano katika kulibainisha hilo pale tuoneshe kwamba ni wapi tunahitaji ni *site* ipi tunaweza tukafanya katika ujenzi wa hivyo vyoo ili wananchi wetu waweze kutumia katika maeneo hayo ambayo tumesema yanahitajika.

Lakini kwa kweli niseme mpango kama nilivyotangulia kusema tutajitahidi kwa kadiri inavyoonekana kwamba inafaa tuhakikishe kwamba huduma hizo zinapatikana katika maeneo yote ambayo yanahitajika kupatikana kupata huduma hizo.

Nam. 108

Tija ya Mapato ya Utalii kwa Wananchi wa Kizimbani

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:

Eneo la Kizimbani limekuwa na mashamba mengi ya viungo vya asili vya Zanzibar ambavyo wageni mbali mbali wanafika kutembelea na kuna mapato yanapatikana kutokana na ujio wa wageni hao hasa watalii. Hata hivyo, fedha zinazokusanywa kwenye maeneo hayo ya mashamba ya viungo *(spieces)* haziwanufaishi wanajamii wanaoishi katika maeneo ya Kizimbani ambao wanayatunza mashamba hayo, aidha hazifiki Wizara ya inayohusika na Kilimo ambayo ndiyo inayosimamia shughuli za kilimo.

(a) Kuna utaratibu gani Wizara itauweka kuhakikisha kuwa sehemu japo ndogo ya mapato hayo inanufaisha jamii ya Kizimbani.

(b) Je, kwa nini fedha hizo zinakusanywa na Wizara ya Fedha wakati shughuli zile ni za Kilimo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 108 lenye vifungu (a) na (b) kabla ya kujibu naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ukusanyaji wa mapato ya Serikali unaongozwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na pia inaongozwa na Sheria ya Fedha za Umma, kwa sasa ni Sheria namba 12 ya mwaka 2016. Kifungu cha 104 ya Katiba kimeweka masharti ya (i) kuwepo Mfuko Mkuu wa Hazina na pia kimeweka masharti ya kwamba katika fedha zinzopatikana katika vyanzo mbali mbali kuwekwa katika mfuko huo. Lakini vile vile kifungu cha 20(1) cha Sheria ya Fedha za Umma Nam. 12/2016 kimesisitiza kuwa Mapato yote, ukiacha yale ya Mfuko Maalum au yanayobakishwa kisheria kwa Mamlaka mbalimbali, yaingizwe katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Kwa mujibu wa Utaratibu, mapato yanayokusanywa kutoka vyanzo tofauti hujumuishwa kwa maana ya *consolidation* pamoja na kupangiwa matumizi kwa nchi nzima badala ya Sekta au mahali yanapopatikana mapato hayo.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kujibu swali lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Wizara haina mpango wa kubakisha sehemu ya mapato ya mashamba ya Viungo Kizimbani. Badala yake itasimamia utaratibu wa Kikatiba na Kisheria wa kusimamia mapato ya Serikali, kuipatia fedha za matumizi Wizara inayohusika ikiwemo hiyo ya Kilimo na kuwafikishia huduma mbalimbali wananchi wa maeneo yote, ikiwemo eneo hilo la Kizimbani.

(b) Fedha hizo hazikusanywi na Wizara ya Fedha na Mipango bali zinakusanywa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi lakini zinawasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina kama ilivyoelekezwa na Katiba na Sheria.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako tena kwanza napenda nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa majibu yake mazuri ambayo yatawaridhisha hasa wananchi wa maeneo ya Kizimbani, Dole na mengine yoyote ambayo yanahusika na maswala haya ukusanyaji.

Mhe. Spika, ningependa nimuulize swala dogo la nyongeza lenye vipengele (a) (b).

(a) Mhe. Waziri kweli fedha hizi zinakusanywa na maeneo ambayo yanakusanywa si kwenye mashamba tu, lakini hata pale getini ambapo ukiingia tu, fedha hizi pia huwa zinakusanywa kwa kila mgeni ambaye ameingia katika eneo lile la Kizimbani. Sasa kama kweli fedha hizi zinakusanywa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa nini hawaandai risiti maalum ambayo itatambulisha kwamba kweli fedha hizi zinakusanywa na zinapelekwa sehemu gani?

(b) Mhe. Waziri, kwa kuwa fedha hizi, zinakusanywa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, ambayo tayari niliwahi kuuliza swala wakanambia kwamba wao hawahusiki na fedha hizi, bali ni Wizara ya Fedha ndio inahusika na fedha hizi. Kwa nini Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuwa fedha hizi kweli zinakusanywa hapo. Je, ni kiasi gani ambacho kinakusanywa kwa mwaka ambacho kina takwimu maalum kinawekewa na kinatambulikana kwa hesabu maalum ambayo inakusanywa kwa kila mwaka. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza ni hakika kwamba mapato hayo yanakusanywa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, lakini si Wizara ya Kilimo tu, taasisi zote zenye vyazo vya mapato vimewekewa utaratibu wa kukusanya mapato yao na kuyawasilisha Hazina. Kwa hivyo Wizara ya Kilimo vile vile, mapato hayo yanakusanywa ikiwemo ya getini lakini vile vile yanayotokana na mashamba, yanakusanywa na wao na wanatakiwa kutoa risiti wakati wanapokusanya mapato hayo. Kama risiti hazitolewi sasa huo ni upungufu ambao tutahitaji kuufuatilia kama hazitowi, lakini mimi naamini kabisa utaratibu unafatwa risiti zinatolewa, fedha zinakusanywa na zikisha kukusanywa zinawasilishwa Hazina kama ulivyo utaratibu inavyoelekeza Katiba na Sheria ya usimamizi wa fedha za umma.

Sasa kuhusu kiwango gani, kinakusanywa nitakuomba Mhe. Spika, uniruhusu nimpe kwa maandishi ni kiwango gani kinatokana na makusanyo yanayotokana na utalii katika mashamba ya Kizimbani na geti kwa sasa hivi sina takwimu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwa majibu mazuri ila kwa kuwa jukumu hili katika majibu yake

alisema linabaki katika Wizara ya Kilimo na baadae fedha zinaingia kwenye mfuko ule wa serikali, nilikuwa nataka kujua kwa sababu mara nyingi tunapoingia kwenye bajeti huwa kuna yale makadirio ya mapato yanavyokadiriwa kila eneo, labda kwa mwaka wa fedha uliopita nasema ulioisha sio huu tunaotaka kuanza nao mara sijui nikarejeshwa huko tunako kwenda. Sasa wizara yako kwa sababu ndio inayotoa hayo makadirio, mmekadiria kiasi gani na yale mafanikio kwa sababu utajibu kwa maandishi sitataka kuyapata leo nitasubiri utakapomjibu Mhe. Hidaya, kunako eneo hili tu la Kizimbani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swala lake na nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza vyanzo vya mapato ni vingi mno na sirahisi kwamba nitaweka kwenye kichwa kiwango ambacho tumekikadiria kwa mwaka 2018/2019, lakini tutawasilisha, Hotuba ya Bajeti ya Serikali katika Baraza hili, na hivyo vifungu vyote vitakuwemo katika viambatanisho naomba asubiri muda ukifika Mhe. Spika, ataviona na kama atakuwa na hoja, ataleta hoja yake wakati huo. *(Makofi)*

Mhe. Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa majibu mazuri la suala zima la eneo la kilimo Kizimbani.

Mhe. Spika, eneo lile la Kizimbani lipo ndani ya Halmashauri ya Magharibi "A" na vijana wangu wa Kizimbani, Dole na Kijichi ndio ambao wanachangia kwa asilimia kubwa sana hizi fedha ambazo zinaingia kwenye Mfuko wa Serikali na muda mrefu sana, wananchi wa maeneo hayo huwa wanaomba na wao wapatiwe japo asilimia ndogo ili tufanyie shughuli za maendeleo. Je, kwa sasa huoni wakati kuna ugatuzi chanzo kile cha mapato kisipewe Halmashauri ya Magharibi "A" ili kuendeleza miradi ya wananchi katika wilaya yetu ya Magharibi "A".

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe Spika, naomba kumjibu Mhe. Masoud Abrahman Masoud, swalilake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza upo utaratibu, vipo vyanzo vya mapato ambavyo vinasimamiwa na Serikali Kuu na vipo vyanzo mapato ambavyo vinasimimiwa na mahalmashauri na mabaraza ya miji, upo utaratibu huo lakini pia si sahihi waheshimiwa kwamba pale yanapotoka mapato, kwamba fedha zile zibakishwe pale. Kwa sababu ikiwa ni hivyo tutasema na Kiwengwa kwenye hoteli za utalii. Fedha zinazokusanywa pale zitumike pale, lakini kwenye mashimo ya mchanga kule jimboni kwangu Donge tunasema hivyo hivyo, kwamba fedha zibakishwe kule lakini suala katika uimarishaji wa usimamizi wa fedha za umma, fedha zote zinatakiwa zijumuishwe pamoja na hayo ndio matakwa ya Katiba na Sheria, kwamba tunajumuisha pamoja na baadae fedha hizo zinagawanywa kwa taasisi mbali mbali katika kuwahudumia wananchi wa nchi hii kwa ujumla wake.

Nam. 59

Mashamba ya Eka Tatu Kusimamiwa na Wizara mbili tofauti Kisiwani Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid – (Aliuliza)**:**

Kwa kuwa mashamba ya Serikali ya eka ya minazi na mikarafuu ni mali ya Serikali ambapo kwa upande wa Pemba, mashamba hayo yapo chini ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na kwa upande wa Unguja mashamba haya yapo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati jambo ambalo linaonekana kama kuna mgongano kati ya Wizara hizi katika usimamizi wa mashamba hayo.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuachiwa mashamba kusimamiwa na Wizara mbili ni tatizo.

(b) Je, ni sababu gani iliopelekea mashamba haya kusimamiwa na Wizara mbili tofauti wakati taasisi zetu zina lengo moja la kuwatumikia wananchi wetu.

(c) Je, ni mashamba mangapi ambayo yanasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na mangapi yanayosimamiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati.

Mhe. Spika: Karibu sana Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, karibu sana katika kuwajibu Waheshimiwa maswali yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:

Naongezea macho ahsante sana, Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kujibu swali alilouliza Mwakilishi mahiri sana huyu wa Konde Mhe. Omar Seif Abeid. Lakini kwanza kabisa Mhe. naomba ruhusa yako nizungumze haya yafuatayo:

Kwanza kabisa nakupongeza sana Mhe. Spika, kwa namna unavyoliendesha Baraza hili la Wawakilishi ni Baraza mahiri, makini lenye michango mizuri sana. Mimi hapa nimepata maswali ishirini na sita ambayo nitatakiwa niyajibu na nitayajibu kwa uhasaha sana na mtafurahi. *(Makofi)*

Pili, napenda sana nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Nasema ameniamini na pamoja na wenzangu wengine na imani hiyo tutamuonesha kwa vitendo na tumeshaanza. Sasa kwa kuanza kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake linahusu mashamba ya Serikali. Kwa kweli Mhe. Omar Seif Abeid namjua anapenda sana mambo ya Serikali yote yatambuliwe. *(Makofi)*

Sasa kwa kuanza sasa swali lake la kwanza anasema jee, serikali haioni tatizo, mashamba haya ya serikali kushughulikiwa na wizara mbili tofauti.

Jibu ni kwamba inaona tatizo na sisi tunaliona hilo tatizo na ushahidi ni kwamba Serikali imeshatoa agizo kwamba mashamba yale yote yarudi kilimo, na kwa kuanza tumeanza

Pemba, tumeshaanza Pemba kule karibu tumefikia asilimia sabiini ya mashamba yote kuyaorodhesha na kuyaweka katika *inventory register* ili yatambuliwe rasmi na hatimae tutakuja Zanzibar hapa bado yapo chini ya Wizara ya Ardhi na mambo mengine yaliyomo kwenye Wizara hii.

(b) Anataka kujua sababu iliyopelekea mashamba haya kusimamiwa na Wizara mbili napenda kumjibu kwamba yanasimamiwa na Wizara mbili kwa sababu hizi wizara zilikuwa moja, ilikuwa Wizara ya Kilimo na Ardhi, nafikiri mnakumbuka hivyo. Sasa wakati huo Wizara ya Kilimo na Ardhi ndipo ilipokuwa ardhi inashughulikia mambo haya, ipogawiwa ikawa Wizara ya Kilimo na Wizara hii ya Ardhi mbali yakapelekwa kule yakapelekwa katika Wizara ya Ardhi.

Sasa kama nilivyosema mwanzo kwamba tumeshaanza kuyachukuwa yale ya Pemba na tutamalizia ya Zanzibar, kwa hiyo ndio sababu kubwa.

(c) Anasema kwamba mashamba mangapi ambayo yanasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Hadi sasa hivi tayari kuna mashamba 8,215 kule Pemba na kati ya hayo 5,822 tayari tumeshayatambua, kwa hivyo hiyo ndio hesabu tuliyonayo. Hesabu ya mashamba yaliyopo hapa unguja tutaileta baadae baada ya kushirikiana na wenzetu na kuanza kuyapima tukayaorodhesha tukayaweka katika *inventory register* hapo tutaleta hesabu hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) lakini na mimi natoa pongezi sana kwa Mhe. Naibu Waziri kajibu, kanijibu kwa asilimia kubwa nimeridhika ingawa kuna baadhi ya jibu hakunambia, lakini ahsante sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yako.

Lakini kwa kuwa katika utaratibu mzima wa kukabidhi mashamba hayo kwa upande wa pemba umetekelezwa kwa asilimia kubwa, ambapo umesema asilimia sabini tayari sasa mimi nilitaka nijuwe, jee ni lini utaratibu huu utakamika ili watu wajuwe uhakika kwamba mashamba ya serikali yote yanasimiwa na wizara moja la kwanza.

Na jee ni sababu gani za msingi zilizopelekea kutokamilika hadi leo ukitilia maani kwamba zoezi hili limeanza nyuma zaidi ya miaka mitano nyuma ni sababu gani hasa za msingi. Ahsante sana Mhe.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi Omar Seif Abeid, jibu lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Utaratibu huu, niseme kweli sisi tumeukuta na kusudia kuuhimiza nataka tukamilishe utaratibu huu kabla ya kumaliza mwaka huu wa fedha, kwa sababu kazi yenyewe si ndogo, kazi yenyewe si ndogo ni kazi kubwa kazi ya kuyahesabu mashamba yale kuyapima upya kuyaweka kwenye *inventory register*, halafu uyaeleze yako wapi yana

thamani gani, hiyo si kazi rahisi itachukua muda mrefu. Kwa hivyo tunakusudia mwaka huu wa 2018/2019 usimalizike mashamba haya yote tuwe tumeshayapima.

Kwa nini hajakamilika, hayajakamilika kwa sababu ndo kazi yenyewe ngumu sana kazi yenyewe kubwa si ngumu ni kazi kubwa, kazi kubwa nafahamu wenzetu waliopita wamejitahidi sana kuyaorodhesha mashamba haya, wamejitahidi kweli kweli kuyaorodhesha. Sasa lakini sisi tunaingia na *speed* ya kuharakisha zaidi kuhesabu mashamba haya, kwa hivyo hee hilo ndio jibu lako kwamba hayakukamika kwa sababu hatutaki kuhesabu moja, pili, tatu aa tunataka tujuwe kila kilichomo ndani ya shamba lile. Ahsante sana Mhe. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwanza nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa majibu yake kwa leo siku ya kwanza lakini pamoja na majibu mazuri kwa sababu naelewa ni mtaalamu wa kilimo naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Wananchi wa Shehia ya Mfenesini na Shehia ya Mwakaje wemekuwa na malalamiko makubwa kwa serikali kuhusu mashamba ya Selem na kumekuwa na kauli mbali mbali zinatolewa, je Mhe. Naibu Waziri unaweza kutoa kauli gani kuhusu wananchi hawa wa Shehia ya Mwakaje na Selem kuhusu mashamba ya Selem.

(b) Je, uko tayari Mhe. Naibu Waziri hata likimaliza Baraza la Wawakilishi mimi na wewe kwenda kuongea na wananchi wale ili tujue hatma yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, na namshukuru Mhe. Machano Othman Said kwa swali lake hilo la nyongeza.

Ni kwamba kwa kujibu swali lako la pili, kwamba nipo tayari aa wakati wowote twende ukiwa tayari niambie tu tutakwenda huko tena kwa sababu ni wapya tutakwenda na waziri wangu tukapaone hapo mahala, kwa ruhusa yake lakini. Halafu kuusu malalamiko haya, malalamiko yako mengi sana ya mashamba Mheshimiwa na yanaleta migogoro mikubwa sana, sasa sisi hatua tunayoichukua tunaifatilia migogoro yote iliyopo na tunayatafutia ufumbuzi utakaofaa bila ya kumdhulumu mtu wala bila ya kumuonea mtu. Kwa hiyo tutegemee kwamba shughuli hii ya kuyatatua haya malalamiko itakwenda haraka iwezekanavyo. Ahsante sana Mhe. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi siku ya mwanzo ya maswali waheshimiwa wizara inayofuata sasa katibu. *(Makofi)*

Nam. 175

Mwakilishi wa Kusimamia Biashara za Shirika Nje ya Nchi

Mhe. Asha Abdalla Mussa – (Aliuliza**):**

Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC) linajukumu la kuwa na mwakilishi wa kusimamia masuala ya biashara ya shirika nje ya nchi.

Je, mwakilishi huyo anatakiwa na watendaji wenye sifa gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza naomba nichukuwe fursa hii ya kumshukuru Mwenye Mungu kwa kutujaalia afya na uwezo asubuhi ya leo lakini mbili kukushukuru wewe kwa kuliendeleza Baraza letu tukufu hadi kufikia hapa leo.

Mhe. Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa imani yake aliyonipa ya kuniteua kwa Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda namuahidi niitaifanya kazi hii kwa uaminifu kwa umahiri na kwa uadilifu mkubwa.

Mhe. Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, kwa mashirikiano mema anayonipa katika Wizara ya Biashara.

Mhe. Spika, kadhalika naomba kuchukua fursa hii kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Welezo kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa Mhe. Asha Abdalla Mussa swali lake Nam. 175 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Shirika la Biashara la Taifa linamshauri wa kusimamia masuala ya biashara katika Tawi lake Dubai. Mshauri huyu si mwajiriwa wa Shirika na hufanya kazi zake wakati wa uwepo wa karafuu tawini hapo kwa kuwafatia wateja ambao hupatiwa asilimia maalum ya kamisheni (1.5%) kwa kila mauzo yanapofanyika. Mkataba wa mtaalamu huyo hauna sifa za kitaalam lakini unasema atakuwa ni mtu mwenye sifa za kitaalamu lakini unasema atakuwa ni mtu mwenye uzoefu wa biashara na mwenye kufahamu vizuri mazingira ya Nchi za Ghuba hususan Dubai. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwanza niseme kwamba kwa kuwa tulikuwa na shauku ya kumsikia Mhe. Naibu Waziri wa Biashara mpya mtetezi wa wakwezi na wakulima kwa kujibu swali lake, hata mimi ukasahau kunipa ruhusa ya kuomba Nam. 175 lijibiwe.

Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Waziri, amesema kwamba mkataba wa mtaalamu huyu hauna sifa za kitaalamu. Lakini pia wanasema kwamba mtu huyu anatakiwa awe na uzoefu wa kitaalamu, lakini pia mtu huyo awe na uezofu wa biashara na wenye kuyafahamu vizuri mazingira na nchi husika.

Mhe. Spika, nataka kufahamu kwamba ni utaratibu gani unaotumika katika kusimamia masuala ya biashara ya shirika nje ya nchi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, Shirika la ZSTC linafanya kazi kwa mujibu wa Sheria Nam. 11 ya mwaka 2011, Shirika hili linauwezo wa kununua na kuuza karafuu nje na ndani ya nchi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria hiyo linao uwezo wa kumuajiri mtaalamu huyu ili aweze kuuza karafuu nje ya nchi pale zinapokuwepo pale Dubai kwa mujibu wa msimu wa wakati ule. Sifa kubwa tunayoitizama hapa ni kwamba lazima ajue masuala ya masoko, lakini pia awe mzoefu kama tulivyosema katika swali mama, hususan nchi ya Huba kama Dubai, awe anayajua mazingira ya pale ya *marketing*. Kwa maana mtaalamu huyu mazingira haya anayajua na baada ya kufanya uchambuzi yakinifu, shirika huyu ndie tuliyompa kazi hii na anaifanya kwa umahiri na kwa umakini mkubwa na Alhamdulillahi karafuu zetu anaziuza wakati na msimu na sasa hivi kule hazipo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda, swali langu lina (a) na (b).

a) Imekuwa ni muda mrefu sana limezungumzwa suala la karafuu yetu ya Zanzibar kuipatia *brand*. Je, suala lile limeshakamilika.

b) Unaonaje kuwepo mtaalamu muelekezi katika nchi za Falme za Kiarabu ni kuipotezea fedha Serikali ya 1.5% anayopata kwa vile uzalishaji wenyewe wa karafuu hautoshelezi na wafanyabiashara wanatoka waliko wanakuja kuzifata karafuu hapa Zanzibar lakini hawauziwi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda:

a) Mhe. Spika, ZSTC, tupo katika harakati za mwisho katika kuhakikisha tunaipatia *brand* karafuu ya Zanzibar. Naomba hilo tulitegemee sio muda mrefu kutoka sasa karafuu ya Zanzibar itakuwa na *brand* yenye kujulikana dunia nzima.

b) Mhe. Spika, suala la kupotea kwa fedha, hapa fedha haipotei, kuna msemo wa Kiswahili unaosema “kiuzwachwa ndicho kitokacho”. Kwa maana hiyo ni lazima tuweke Mshauri Muelekezi na tumekubaliana nae kumlipa 1.5% ili aweze kuziuza karafuu zetu zimalize tuweze kupata fedha kwa kuleta maendeleo ya nchi yetu Zanzibar. Kwa maana hiyo siyo kupoteza pesa bali ni kupata pesa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa swali la mwisho la nyongeza nitampa Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kuhusiana na huyu wakala mimi namwita ni

agency. Kwa kuwa anafahamu wakala huyu anabeba dhima kubwa ya kutuunganisha biashara yetu sisi na watu wa Dubai. Ni utaratibu gani unaotumika wa kumpata kwa maombi na kumkubaliana na kumthibitisha ili awe *agency* kabla hiyo kazi hajapewa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakwenda kwa mujibu wa Katiba na Sheria zake. Sheria iliyotumika kumpata ni Sheria ya Utumishi ipo wazi katiba katika masuala ya Utumishi ambayo ya kumpata mshauri huyu ndiyo iliyotumika. Imetumika Sheria na ndiyo maana yupo na anafanya kazi kwa mujibu wa sheria. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Biashara kwa majibu yako. Sasa Wizara inayofuata Katibu.

Nam. 37

Ukarabati na Matunzo ya Nyumba za Vijiji Katika Wilaya ya Micheweni:

Mhe. Ali Khamis Bakar – Alijibu:

Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo kutukutanisha hapa na tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie Mkutano wetu umalize salama na afya njema.

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kutekeleza azma kuu ya kuwajengea wananchi nyumba za makaazi ambayo Wilaya ya Micheweni ni moja ya Wilaya iliyofaidika na nyumba hizi za vijiji. Hata hivyo, kwa sasa nyumba hizo ni chakavu na zimepitikiwa na wakati kiramani.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kinachohitajika kuziboresha na kizifanyia ukarabati nyumba hizo.

(b) Ni kiasi gani cha fedha zilizopatikana katika kipindi chote ambacho nyumba hizo zinakodishwa hadi sasa.

(c) Je, ni lini serikali itatoa kauli ya kuwauzia wananchi wenye uwezo nyumba hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 37 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kiasi cha fedha kinachohitajika kuziboresha na kuzifanyia matengenezo makubwa nyumba hizi za Micheweni ni jumla ya Shilingi Milioni Mia Sita Arubaini na Nane (Tshs. 648,000,000/=), lakini bila ya kuwasilisha nyumba ndogo ndogo.

(b) Mhe. Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo, kodi iliyokusanywa tangu kuanzishwa Shirika la Nyumba Zanzibar ni Shilingi Milioni Nane Laki Nane Tisini na Tisa Elfu (Tshs. 8,899,000/=).

(c) Mhe. Spika, kwa sasa serikali bado haijweka utaratibu wa kuziuza nyumba hizi za Maendeleo kwani bado zinahitajika kuwa sehemu ya Mtaji wa Shirika la Nyumba Zanzibar na kuliwezesha Shirika kukopa katika Taasisi mbali mbali za fedha kwa mipango ya baadae ya miradi ya ujenzi wa nyumba za Shirika.

Ni matarajio yetu kuwa katika siku za usoni baada ya Shirika la Nyumba Zanzibar kuimarika utaratibu mzuri utaandaliwa wa kujenga nyumba kwa ajili ya kuuza na kukodisha. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwandam, naomba nimuulize Mhe. Waziri kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri majibu haya ya Nam. (b) ya pesa hizi ambazo zimetajwa kiukweli haziendani na uhalisia wa nyumba jinsi zilivyo. Nyumba hizi zimejengwa tokea mimi sijazaliwa, kusema ukweli nyumba zimekuwa chakavu, mapaa yamekatika, kiasi ambacho nyumba hizi hata wale wananchi wanaokaa wengine madirisha hamna wameweka mapolo.

Je, naomba nimuulize Mhe. Waziri ni lini mimi na wewe tutakwenda Micheweni twende ukafanye ziara maalum kuzikagua nyumba hizi ili ijue Wizara yako kuziboresha nyumba hizi na wananchi wale waweze kuzitumia. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo, wakati wowote nipo tayari baada ya kupata muda na hasa baada ya kumaliza kipindi cha Baraza. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Namshukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza, nashukuru kwa majibu yake mazuri Naibu Waziri, lakini nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nyumba hizi za maendeleo ambazo kama alivyosema mwenyewe bado hawana mpango wa kuziuza, lakini ni kioo cha Zanzibar. Nyumba hizi takriban kila fleti moja inawezekana Shirika la Nyumba, kuna nyumba zake tatu tu ambazo ndizo zinakuwepo, lakini katika mazungumzo ya nje nyumba hizi zinakuwa ni nyumba za serikali zinaonekana hazijulikani kama ni nyumba za watu binafsi. Kwa hivyo nyumba zile zinaleta taaswira ambayo haijulikani kwamba zitatengenezwa na nani.

Je, serikali ina mpango wa kuzitengeneza kwa makusudi ambao mpango huo utakuwa ni 100% kutengenezwa na serikali au kama haina mpango wa kutengeneza ina mpango gani

wa kuweza kuzungumza na wale ambao wanamiliki nyumba zile ili nyumba zile ziwe kioo kama ilivyokusudiwa katika mji wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Nikweli kama alivyosema kwamba tafsiri iliyokuwepo ni hiyo ya kwamba Serikali inawajibika kwa sababu nia ya serikali ni kuwatafutia wananchi wake makaazi bora na salama. La msingi niseme kwamba serikali itakaa na wahusika wa maeneo hayo wenye kumiliki zile baadhi ya *flat* kusudi kuona ni utaratibu gani. Imani yangu ni kwamba hatuwezi kukosa namna ya kwenda katika kulimaliza suala hili. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambalo limekuja hapa la kuhakikisha kwamba nyumba zile bado zipo mikononi mwetu salama. Swali langu lipo hapa la (a) na (b).

a) Kwanza Shirika la Nyumba lina nembo yake na nyumba hizi zote hatujaona nembo yake. Wizara inampango gani wa kuweka nembo kwamba Shirika la Nyumba ili zieleweke.

b) Kwa kuwa tuna kodi ya Shs. 8,899,000/= kwa miaka yote, ni mwaka gani Shirika limeanza kazi zake hata tukapata kodi hii, naona kiwango cha Chini kabisa ukilinganisha na mazingira ya nyumba zenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kuhusiana na nembo hilo ni suala la kuzingatiwa, tumeuchukua ushauri wako na tutaufanyia kazi.

b) Mhe. Spika, kodi hii itaanza mwezi wa April mwaka wa 2016. Ahsante sana.

Nam. 55

Utoaji wa Mizigo katika Bandari ya Zanzibar Kinyume na Utaratibu

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:

Kwa kawaida Shirika la Bandari Zanzibar moja ya kazi zake kuu ni upakuaji wa makontena ya mizigo, ambapo shughuli hii hufanywa kwa mashirikiano na taratibu za

TRA, ZRB na ZBS. Hata hivyo, imebainika kuwa kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na mtindo wa kutoa magari hayo ya mizigo nyakati za usiku, huku taasisi shirikishi zote zimeshafunga kazi na kuondoka.

(a) Je, Wizara mnataarifa kuhusu jambo hilo.

(b) Ni hatua gani mlizochukua za makusudi kukomesha vitendo hivi visiendelee.

(c) Je, Wizara kupitia watendaji wake hatuoni kufanya hivyo ni kuikosesha mapato Serikali.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii tena kusimama mbele ya Waheshimiwa Wawakilishi kujibu maswali yao. Lakini nimshukuru pia Mhe. Dkt. Shein kwa kuwa na imani na mimi kwamba ninaweza kuifanya kazi hii kwa uadilifu.

Naona mtashangaa kwamba nimesimama hapa leo isipokuwa nataka niwafahamishe tu kuwa Naibu wangu ni mgonjwa, amefanyiwa *operation* kwa hivyo nitakuwa na nyinyi kujibu maswali yenu mpaka hapa atakaporudi. Naomba tumuombee Mwenyezi Mungu ampe nafuu ili tuwe na yeye tena. *(Makofi).*

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Shirika la Bandari huwa linafanya kazi kwa masaa 24 kwa kuteremsha na kupakia mizigo melini. Pia naomba ifahamike kwamba, gari zinazotoa mizigo nje ya Shirika hilo hutoa mizigo kuanzia saa 2:00 mpaka saa 12:00 jioni. Kuna baadhi ya ruhusa ambayo huwa inatolewa pekee kwa ile mizigo kwa mfano saruji, mchele baada ya wao kuomba na kupata ruhusa maalum kutoka TRA, ZRB, ZBC, ZFDB.

Mhe. Spika, aina nyengine za mizigo utaratibu wa kutoa mizigo hiyo kama saa hizo ambazo zilizopangwa na si vyengine. Kwa utaratibu huu ulowekwa na kusimamiwa na Shirika la Bandari, Serikali inapata mapato yake kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri kama ifuatavyo. Pamoja na majibu yake mazuri aliyoyatoa naomba nimuulize swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Je, kwa nini Ofisi zinazohusika na ukusanyaji wa mapato ya Serikali hufungwa wakati mizigo inatoka.

b) Serikali inauhakika gani kwamba magari yanayotokana na mchele, Unga wa ngano na saruji yanakaguliwa kwa uhakika.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, napenda kumjibu swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Ni kweli anachokisema, lakini inategemea na shughuli gani zinafanyika wakati gani. Shirika la Bandari linafanya kazi masaa 24 na huwa wanapeana zamu nani awepo asubuhi mpaka saa 8 nani awepo saa nane mpaka saa 4 na nani anakesha. Kwa utaratibu huo malipo yote yanafanyika kwa hivi vikundi ambavyo vimetajwa. Wengine hawawezi kufanya hiyo shughuli saa hizo, lakini kwa wale wanaofanya usiku kuna watu maalum ambao wanapangwa.

Mhe. Spika, ningependa kumfahamisha kwa utaratibu uliowekwa pale na ulinzi unaokuwepo pale mara nyingi binaadamu hakosi mbinu lakini mara nyingi huwa anajitahidi kuhakikisha kwamba hilo linatendeka. Siwezi kukataa kwa sababu sijawahi kuwepo kule usiku nikaona mizigo inapotoka, kama kuna kitu kama hicho kinaweza kikatendeka nimekisikia kutoka kwako, nitajaribu kufatilia nione uhakika wa jambo lenyewe. Lakini kwa ninavyofahamu kuna ulinzi wa kutosha na nina imani kwa watu waliokuwepo pale nimeshakaa nao na nimewafahamu, nina imani kwamba kama linatokea tatizo kama hilo sio mara kwa mara.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Spika kwa kuniona na mimi nimuulize swali dogo la nyongeza Mhe. Waziri.

a) Mhe. Spika, kwa kuwa ZBS kwa utaratibu pale magari yanapofika Bandarini unahitaji kupata kupeleka gari kwenye ofisi zao ili upate ile *certificate* ya ZBS ambayo ofisi yao ipo Viwanda Vidogo vidogo. Kwa mujibu wa Sheria yetu ya *Road Traffic Act* ya mwaka 2003 Sheria Nam. 7 inagongana na utaratibu mzima ya kutoa gari kutoka Bandarini kutembea njiani bila ya namba hadi uifikishe katika eneo linalohusika kupata hiyo *certificate* na njiani hutokezea pia hawa wananchi kukamatwa na pengine na *traffic* wetu polisi. Sasa je, hatuoni utaratibu huu tunawakwaza wananchi.

b) Kwenye mpango mzima wa ZBS, wamekuwa na utaratibu wa kuwa na Mawakala nchi tofauti lakini nchi mfano kama Hongkong ama Singapore ambapo wafanyabiashara wengi wanafanya manunuzi ya magari, ZBS wameshindwa kuwa na wakala. Lakini pia utaratibu mzima wa kulipa fedha wanatakiwa kulipa dola 125 huko nje. Sasa je, Wizara yako ni kiasi gani ya fedha hichi kinakuja Zanzibar katika kiwango hichi pamoja na baada ya kulipa ada hizi huko nchi za nje. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri hilo swali pili naona kama la Wizara ya Biashara hebu jaribu kujibu hili la mwanzo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali la kwanza ambalo linanihusu, swali la pili sitolijibu kwa sababu halipo kwenye mamlaka yangu.

a) Swali la kwanza linasema watu wa Bandari na watu wa ZBS wanataka wapate Ofisi pale. Wapi Ofisi ya ZBS ilipo siifahamu lakini Bandarini wanapaswa kuwepo na kwa hali ya ufinyu wa eneo lile si dhani kama kuna pahali ambapo ZBS inaweza ikapata pale. Nimetembea eneo lile, hao wa Bandarini wenyewe hawaenei, kwa hiyo wao ni

wajibu wao kuwepo pale kwa saa zile ambazo watakiwa, wanatakiwa wajipange, wakifika pale hayo maeneo ambayo wanapangiwa ndipo wanapopaswa kuwepo. Lakini kuwa na ofisi siwezi kumpa *guarantee* kwa sababu bandari haitoshi.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Je kuna kipimo gani kinachokagua magari hayo yanapotoka nje ya Bandari?

Mhe Spika: Mhe Waziri sijui kama umelifahamu swali.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe Spika napenda kumjibu Mhe Mwakilishi wa Wanawake Salma Mussa Bilal kama ifuatavyo. Pale Bandarini kama umetembelea pana sehemu ambayo kuna sehemu inapima mizigo kama labda umetembea sehemu za Bara utakuta barabarani kuna sehemu za kupima mizigo magari mazito yanapita pale. Kwa hiyo na bandarini ipo sehemu hiyo na magari yote yanapita pale na yanapimwa na nimeona kwa macho yangu kinachotendeka kwa hiyo usiwe na wasi wa mizigo kupimwa *(Makofi)*

Mhe NadirAbdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillahi Rahman Rahyim* Mhe Spika naomba nimuulize masuala ya nyongeza (a), na (b) Mhe Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

a) Kwa kuwa magari yale ya makontena yanayofanya kazi zake asubuhi mpaka usiku wakati mwengine saa nane kuingiza makontena na kutoa makontena na hii ni nchi ya Utalii na Malindi kuna hoteli zisizopungua sita za kitalii katika ukanda ule wa sinema na upande wa kushoto ambapo mimi mwenyewe niko kwenye hoteli *industry* miaka kumi na tatu eneo lile, makontena yale keria ile inobeba nyuma makontena haina kiwango kontena linapiga kelele wageni wanahama hoteli zinaingia hasara na pia zinakuwa Mhe. Waziri wa Utalii anasikia wana-*complain* kwenye makomputa maeneo yale hoteli karibu sita hazipati watalii kwa sababu ya makontena yale.

b) Ni lini sasa wizara yako italipa fidia wenye mahoteli yale kutokana na uzembe wa makontena yale yanayofanya zogo?

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe Spika napenda kumjibu Mhe Nadir Abdul-latif Yussuf swali lake kama ifuatavyo:-

Nimesema bandari inafanya kazi masaa ishirini na nne bandari ni eneo dogo sana pale mizigo iliyopo na meli zinazosimama kusubiri kushusha mizigo inakuwa saa nyengine inachelewa. Sasa kama tutafanya kazi au tunafanyakazi masaa ishirini na nne bandari haitoshi kutoa mizigo tukaweza kupeleka mengine. Leo ikiwa tutapunguza saa tutafanya vipi hiyo kazi. Sisi kufanya kazi masaa ishirini na nne tumewekewa kwa utaratibu kwa hiyo lazima tufanye hivyo ili mizigo itoke na mengine iweze kufika. Masuala ya hoteli kuweko pale chini ya barabara sidhani kama hilo ni kosa la bandari kama wanaona bughudha wahamishe hoteli sisi tutoe mizigo. *(Makofi)*

Mhe Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe maswali yetu yamekwisha, nina tangazo moja. Mhe Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anapenda kutangaza kuwa shughuli ya diaspora ile shughuli yetu ya uzinduzi wa kitabu cha sera ya diaspora ya Zanzibar, shughuli ile inafanyika leo saa 7:30 mchana katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi la zamani. Kwa hivyo, Mhe Waziri alikuwa anawakaribisha wale wote wadau na wapenda maendeleo waweze kushiriki katika shughuli yao hiyo. Baada ya tangazo hilo sasa naomba Katibu shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na hatimae likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Karimu kwa kutujaalia amani na kuweza kukutana tena katika kikao hiki cha Baraza la Tisa la Wawakilishi ili kujadili masuala mbali mbali yanayohusu maendeleo ya nchi yetu. Namuomba Mola wetu Mtukufu atujaalie tutekeleze jukumu letu hili kwa hekima na busara ili tufikie lengo tulilokusudia.

Mhe. Spika**,** napenda kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza na kumshukuru sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake anazozichukua katika kuiongoza nchi yetu. Aidha, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyoendelea kuiongoza nchi yetu ambapo mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi hiki kifupi cha uongozi wake.

Mhe. Spika**,** vile vile, naomba kuchukua nafasi hii kukupongeza na kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wako wote kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa umakini mkubwa. Nawapongeza pia waheshimiwa Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Baraza kwa usimamizi wao mzuri wa utendaji kazi kwa Wizara na Taasisi zetu za Serikali. Aidha, napenda kutoa shukrani maalum kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Konde, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Bi. Panya Ali Abdalla, Mwakilishi wa Viti Maalum na Wajumbe wote wa Kamati kwa kusimamia utekelezaji wa bajeti yetu ya mwaka 2017/2018 na kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya mwaka 2018/2019 na kukubali yawasilishwe katika kikao hiki.

Hali ya Uchumi wa Zanzibar

Mhe. Spika**,** nchi yetu inaendelea kufanya vizuri kiuchumi na kifedha kama ambavyo imeelezwa mara kwa mara na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na kusisitizwa na kuelezwa kwa kina na Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Mipango kuwa uchumi wetu unaendelea kukua mwaka hadi mwaka. Bila shaka tuna kila sababu ya kushukuru mafanikio yetu yaliyotokana na neema kutoka kwa Mola wetu, yaliyongezwa nguvu na jitihada zetu za kujikwamua tulipo na muitikio wa wenzetu hususan wa wawekezaji wa ndani na nje.

Mhe. Spika, kimsingi ningependa uchumi wetu ukue kwa kasi kubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa lakini bado alau unakua kwa kasi nzuri ya wastani wa asilimia 6.8 kwa takriban miaka kumi sasa. Hii sio kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wetu.

Mhe. Spika, katika ukuaji huo, kumeendelea pia kujitokeza mageuzi ya kiuchumi kwa Sekta za kisasa na huduma na uzalishaji viwandani ambazo zimeendelea kuimarika na kuchukua nafasi ya Sekta ya Kilimo katika kuchangia Pato la Taifa. Pamoja na kuwa uzalishaji wa Sekta ya Kilimo nao umeendelea kukua, kwa sasa takriban thuluthi mbili ya Uchumi wetu unachangiwa na Sekta ya Huduma na Viwanda. Haya ni mafanikio makubwa na tunapaswa kuendeleza zaidi.

Mhe. Spika**,** kwa kiasi kikubwa, ukuaji na mabadiliko hayo ya mwenendo wa uchumi wetu ni matokeo ya uwekezaji unaoendelea nchini. Tokea kuasisiwa kwa Sera zilizoruhusu mchango wa Sekta binafsi katikati ya miaka ya 1980, Sekta hiyo imechangia sana katika uwekezaji wa rasilimali nchini hususan katika Sekta ya Utalii. Uwekezaji huo pia umekuwa chachu ya maendeleo kwa Serikali kutekeleza miradi mbali mbali hasa kwa kuwekeza katika miundombinu ya msingi kama vile ya barabara, umeme na maji ili kwenda sambamba na jitihada na Sekta binafsi.

Mhe. Spika, kwa sasa tunashuhudia pia mabadiliko mengine katika tasnia ya uwekezaji ambapo pia kumekuwa na kuimarika kwa ubora wa miradi mipya, ambamo fedha nyingi zaidi zinawekezwa katika idadi ndogo ya miradi. Aidha, tunashuhudia pia sehemu kubwa ya uwekezaji huo kufanywa na wawekezaji wazawa badala ya kuwaachia wawekezaji kutoka nje pekee. Naomba nichukue nafasi hii kutambua, kuthamini na kupongeza sana juhudi za wawekezaji wote hususan wazalendo hapa nchini. Mafanikio haya ya ukuaji wa uchumi kutokana na uwekezaji hapa nchini yamepelekea mafanikio mengine muhimu kwa jamii yetu na uendeshaji wa Serikali kwa jumla; ikiwa ni pamoja na ongezeko la upatikanaji wa mapato na uhudumiaji wa Serikali.

Mhe. Spika, bado hatujaweza kufikia kujitegemea kwa mapato yetu ya ndani kutosheleza mahitaji yetu kwa ukamlifu. Hata hivyo, tulipo leo sipo tulipokuwa jana. Tumepiga hatua kubwa na tunapaswa kujivunia. Leo hii, ruzuku kutoka nje inachangia chini ya Shilingi 8 kwa kila shilingi mia moja tunazotumia. Miaka michache nyuma ruzuku ilichangia hadi asilimia 40 ya Bajeti yetu. Hali ya sasa inamaanisha kuwa tumepunguza sana utegemezi wa misaada ya nje katika *(Makofi)* kugharamia kazi zetu kwa sasa, pamoja na kuimarisha sana mishahara kutumia chini ya asilimia 40 ya mapato yetu ya ndani hivyo kiasi kinachobakia kinasaidia kugharamia kazi za kawaida na kuongeza mchango wetu katika uwekezaji wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika**,** mafanikio haya hayakuja tu yenyewe bali yanatokana na jitihada maalum ya Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kusimamia fedha za umma, matunda mazuri yaliyotokana na Sera zetu za kushajiisha uwekezaji binafsi na kuimarika kwa usimamizi wa Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zetu za ukusanyaji mapato ambazo ni *ZRB* na *TRA*. Mapato yetu yamekuwa yakiongezeka kwa takriban asilimia 30 mwaka hadi mwaka. Naomba kutumia fursa hii kuupongeza sana uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango, *TRA* na *ZRB (Makofi)* kwa kazi hiyo nzuri. Hata hivyo, natoa pongezi hizi nikitambua kuwa bado kuna upotevu wa mapato unaosababishwa na udanganyifu wa baadhi ya walipakodi wakisaidiwa na baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu katika taasisi hizo. Narudia kusema kwamba Serikali haitamvumilia mtu yeyote anaehujumu jitihada za Serikali za kuimarisha huduma kwa wananchi na kuharakisha maendeleo yetu kwa kukidhi tu tamaa zake. Natamka leo hapa kuwa tutawachukulia hatua, iwe muwekezaji, mfanyabiashara au mfanyakazi wa taasisi yenyewe yoyote ya umma. Mapato yetu yakusanywe kwa ukamilifu kwa mujbu wa Sheria na yaendelee kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Miradi ya Pamoja ya Maendeleo ya Muungano

Mhe. Spika, nchi yetu inashirikiana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inaendelea kufuatilia kwa karibu miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa pande zote za Muungano. Ni wazi kuwa miradi kama vile Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III), Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (MIVARF), Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya Pwani na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) imesaidia kwa kiasi kukubwa kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

Hali ya Siasa

Mhe. Spika, nchi yetu imeendelea kujivunia uhuru na demokrasia iliyopo ambayo imewawezesha wananchi kushiriki katika shughuli zao za kuichumi na kijamii bila ya matatizo. Tumeshuhudia viongozi wa kisiasa wakiendesha shughuli zao za kuimarisha vyama vyao huku Serikali ikisimamia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa zinatekelezwa. Wito wangu kwa viongozi wote na wananchi kwa jumla kuendelea kuitunza amani yetu tuliyo nayo pamoja na kudumisha mashirikiano ili tuweze kushiriki kikamilifu katika kuijenga nchi yetu. Nawahakikishia wananchi kuwa Serikali iko makini na haitosita kuwachukulia hatua inayostahili wale wote watakaovunja amani yetu.

Suala la Mafuta na Gesi Asilia

Mhe. Spika, zoezi la utafutaji wa mafuta na gesi asilia lilizinduliwa rasmi na Serikali tarehe 14 Machi, 2017 kwa kufanya utafiti wa njia ya anga au *Full Tensor Gravity Survey – FTG* katika Kitalu cha Pemba - Zanzibar. Madhumuni ya zoezi hilo ambalo lilikuwa lilifanywa na Kampuni ya *BELL GEOSPACE* ya *Scotland* ilikuwa ni kuangalia miraba

yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta na gesi asilia. Zoezi hilo lilichukua muda wa miezi sita.

Mhe. Spika, baada ya kumalizika zoezi hilo la utafiti kwa njia ya anga, utafiti uliendelea kwa kutumia Mitetemo *Seismic* kwa maeneo ya baharini ambalo lilifanywa na Kampuni ya *BGP* kutoka *China* na lilianza tarehe 28 Oktoba 2017 hadi tarehe 28 Novemba, 2017. Madhumuni ya zoezi hilo ilikuwa ni kuangalia maumbile *features* ya miamba yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta na gesi asilia ambapo jumla ya mistari 66 yenye urefu wa kilomita 2,815.6 ilifanyiwa utafiti.

Mhe. Spika, zoezi la Mitetemo kwa upande wa ardhini pamoja na kina kifupi cha maji lilianza rasmi tarehe 8 Februari, 2018 katika Kisiwa cha Unguja. Jumla ya mistari 13 inafanyiwa utafiti ambapo hadi tarehe 20 Aprili 2018 mistari 9 imeshafanyiwa utafiti zaidi. Zoezi hili kwa upande wa Unguja linategemewa kumalizika mwanzoni mwa mwezi wa Juni 2018. Kwa upande wa Kisiwa cha Pemba zoezi linategemewa kuanza mwezi wa Juni ambapo jumla ya mistari 15 inategemewa kufanyiwa utafiti. Zoezi hilo linategemewa kuchukua miezi minne kukamilika kwake.

Mhe. Spika, baada ya kukamilika zoezi la kukusanya taarifa za Mitetemo, Kampuni ya *BGP* itazitafsiri taarifa hizo kazi ambayo inategemewa kuchukua mwaka mmoja hadi kumalizika. Taarifa za mtetemo ndizo zitakazoonesha maeneo ya kuchimba visima vya utafutaji mafuta ambavyo vitathibitisha uwepo wa mafuta na gesi asilia. Wito wangu kwa viongozi na wananchi katika maeneo mbali mbali ambayo zoezi hili linaendelea kufanyika waendelee kushirikiana na wataalamu wetu ili tufikie lengo tulilolikusudia.

Uimarishaji wa Miundombinu

Mhe. Spika, katika kuimarisha miundombinu na huduma za TEHAMA Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa mkonga wa mawasiliano wa taifa unatoa huduma kwa wote ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano hapa Zanzibar ambayo ni chachu ya maendeleo. Aidha, Taasisi mbali mbali za Serikali na Binafsi zimeshaanza kutumia mkonga huo kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma kwa jamii. Sambamba na hilo Serikali inaendelea kuimarisha kituo cha kuhifadhia kumbukumbu au *Data Center* kilichopo Mazizini kwa lengo la kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za kielektroniki za Serikali na taasisi binafsi hapa Zanzibar pamoja na kuanza utekelezaji wa Mradi wa e-*health* na e-*tax* ambapo hadi hivi sasa tayari vituo vya afya 24 Unguja na Pemba zimeshaunganishwa na mkonga huo. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali imeweza kujenga vituo 10 vya TEHAMA vya kijamii *ICT Community Centers* katika wilaya 10 za Zanzibar lengo ikiwa ni kutoa taaluma ya TEHAMA kwa jamii na kupeleka huduma hiyo kwa faida ya jamii.

Mhe. Spika**,** kwa upande wa sekta ya usafiri wa anga Serikali inaendelea kutayarisha upembuzi yakinifu *Feasibility Study* wa Uwanja wa Ndege wa Pemba wa kubaini urefu wa uwanja unaohitajika ambapo kazi hiyo inafanywa na Kampuni ya *Dar Alhandasaa* kutoka Misri chini ya ufadhili kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB). Mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu kazi ya kuimarisha uwanja huo kwa kuongeza

urefu itaanza mara moja na itapelekea uwanja huo kuwa na uwezo wa kuruka na kutua ndege za kimataifa aina ya *Boeing 737*.

Mhe. Spika, serikali inaendelea kuimarisha huduma zake katika viwanja vya ndege ili kuyawezesha mashirika ya ndege ya kimataifa kuweza kutumia viwanja vya ndege kwa safari za moja kwa moja baina ya Zanzibar na nchi zinazotoka mashirika hayo ya ndege. Hivi sasa nchi yetu imefanikiwa kuwa na safari ya moja kwa moja kutoka Zanzibar hadi Urusi, Zanzibar – Poland, Zanzibar – Israel, Zanzibar – Italy, Zanzibar – Ujerumani, Zanzibar – Oman na Zanzibar – Qatar kupitia mashirika mbali mbali ya kimataifa.

Mhe. Spika, katika kuimarisha usafiri wa nchi kavu, Serikali imeanza matayarisho ya ujenzi wa Barabara ya Bububu – Mahonda – Mkokotoni kupitia Kinyasini baada ya kukamilisha ulipaji wa fidia ya vipando na nyumba zitakazoathirika na ujenzi huo. Vilevile, Serikali inaendelea kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali za Unguja na Pemba ili ziweze kupitika muda wote ikiwemo uzibaji wa viraka, uwekaji wa lami pamoja na usafishaji wa barabara hizo.

Huduma za Maji Safi na Salama

Mhe. Spika, katika kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na kutatua kero za ukosefu wa maji katika maeneo mbali mbali ya mikoa ya Zanzibar, hususan maeneo ya Mji Mkongwe na Ng'ambo ya Asili, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*); imo katika hatua za awali za utekelezaji wa kazi ya ujenzi wa matangi mawili makubwa ya Saateni na Mnara wa Mbao na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 68 kutoka visimani hadi matangini na kutoka matangini hadi kwa watumiaji kupitia Kampuni ya *Stecol Corporation Ltd* ya China.

Huduma za Afya

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kupambana na maradhi mbali mbali imeweka Mpango wa chanjo Zanzibar tangu mwaka 1981 ambapo hadi sasa jumla ya vituo vya Afya 175 vya Serikali na binafsi vinatoa huduma za afya za chanjo ili kujikinga na maradhi yanayoweza kuepukika. Katika kuendeleza juhudi hizo, Serikali imeanzisha Chanjo mpya dhidi ya ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi *(Human Papilloma Virus - Vaccine)* inayotokana na mabadiliko ya ukuaji usio wa kawaida wa seli za mlango wa kizazi. Saratani hii inaweza kujipenyeza ndani na kushambulia na kusambaa katika milango wa kizazi na viungo vyengine mwilini.

Mhe. Spika, chanjo hii inatolewa kwa watoto wa kike wenye umri wa miaka 14 ambapo vituo maalum vimewekwa kwa ajili ya kutoa huduma hiyo Unguja na Pemba. Uzinduzi rasmi wa chanjo hiyo umetolewa na Mhe. Mama Mwanamwema Shein, Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 10/4/2018. Wito wangu kwa viongozi wa Serikali, Mikoa, Wilaya, watendaji kutoka vituo vya afya na jamii kwa jumla kuwahamasisha na kuwaruhusu watoto wetu kupata chanjo hiyo muhimu kwa ajili ya afya kwani Jamii iliyochanjwa; ni Jamii yenye Afya**.**

Mhe. Spika, kwa upande wa suala la uchangiaji wa damu salama, Serikali inaendelea kuwaomba wananchi kujitokeza zaidi kuchangia damu kabla ya kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuanza. Katika kufanikisha zoezi hili Serikali imeandaa program maalum iliyoanza tarehe 2/5/2018 na inatarajiwa kumalizika tarehe 14/5/2018 katika maeneo mbali mbali ya Wilaya za Unguja na Pemba itakayowakutanisha watu watakaoweza kuchangia damu.

MASUALA MTAMBUKA

Mapambano Dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto

Mhe. Spika, serikali inaendelea na mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto ambapo kwa kipindi cha hivi karibuni kesi hizo zimekuwa zikiongezeka kwa kasi kubwa katika maeneo mbali mbali hapa nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa miaka mitano wa kupambana na ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mahkama za Watoto 4 Unguja na Pemba Mahkama hizo ziko Vuga, Chakechake na Wete kwa ajili ya kusikiliza kesi zinazohusu watoto walio chini ya umri wa miaka 18. Kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 jumla ya kesi za watoto 129 zimeripotiwa katika Mahkama za Vuga, Kaskazini na Kusini Pemba. Kati ya hizo kesi 45 zimepatiwa hukumu, 8 zimefutwa na 76 zinaendelea.

Mhe. Spika, hatua nyengine iliyochukuliwa na Serikali katika kupambana na udhalilishaji ni kuzifanyia mapitio sheria zinazosimamia masuala ya udhalilishaji ambazo zilibainika kuwa na upungufu. Jumla ya sheria 4 zimefanyiwa marekebisho ili kwenda sambamba na wakati na mazingira tuliyonayo ambazo ni Sheria ya Adhabu namba 8 ya mwaka 2018, Sheria ya Mwenendo wa Adhabu namba 7 ya mwaka 2018, Sheria ya Ushahidi ya mwaka 2016 na Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam.9 ya mwaka 2017. Sheria hizi pamoja na mambo mengine zimeondosha dhamana kwa makosa ya ukatili na udhalilishaji na kuongeza kifungo kwa makosa hayo kwa Mahkama za chini. Aidha, Mahkama ya Kadhi imeimarishwa uwezo wake katika kushughulikia kesi zinazohusiana na masuala ya ndoa, kuachana, malezi ya watoto na ugawanaji wa mali kwa mujibu wa mtu alivyochangia. Sheria ya Ushahidi imekubali ushahidi wa mtoto na ushahidi wa kielektroniki.

Kukabiliana na Maafa

Mhe. Spika, siku ya tarehe 14 na 15 April, 2018, nchi yetu imeshuhudia mvua kubwa za Masika zilizoambatana na upepo mkali ambazo zinaendelea kunyesha. Kutokana na hali hiyo, bado tunatakiwa kuendelea kuchukua tahadhari juu ya madhara yanayoweza kujitokeza ikiwemo miripuko ya maradhi kama vile matumbo ya kuharisha na kipindupindu.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Kanda ya Zanzibar, kiwango cha mvua kilichoripotiwa katika kituo cha Uwanja wa Ndege siku hizo ni milimita 115.3 kwa muda wa saa 24. Mvua hizo zilileta athari kwa wananchi wenzetu katika Mkoa wa Mjini Magharibi hasa katika maeneo ya Sebleni, Kwawazee,

Nyerere, Pangawe,Tomondo Ziwamaboga, Fuoni Jangamizini, Mwera na Bumbwisudi. Aidha, mvua hizi zimesababisha nyumba zipatazo 1,576 kuathirika sambamba na kifo cha mtoto mmoja mwenye umri wa miaka 4 aliyezama katika shimo la karo eneo la Sebleni. Mbali na athari za mvua hizo upepo mkali uliotokea katika Mkoa wa Kusini Unguja ulisababisha nyumba 156 na banda moja kuathirika. Nachukua fursa hii kwa mara nyengine tena kwa niaba ya serikali kutoa pole kwa wafiwa na wananchi wote waliopata maafa hayo na kuwataka kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu.

Mhe. Spika, bado tunaendelea kuwataka wananchi kuepuka kujenga katika maeneo hatarishi ambayo mazingira yake yanaweza kuathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa hasa katika msimu wa mvua hizi kubwa zinazonyesha kama vile mabondeni na njia asili za maji pamoja na kuepuka kulaza mabati katika nyumba zetu kwa kuweka mawe na matofali hali ambayo husababisha kuathiriwa zaidi na upepo mkali unapotokea.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na maradhi mbali mbali hasa yale yanayosababishwa na wanyama kwenda kwa binadamu yakiwemo maradhi ya Ebola, Mafua ya Ndege na Kichaa cha Mbwa, serikali imeanzisha Timu ya Uratibu wa Afya Moja (*One Health Coordination Desk*) ili kukabiliana vyema na maradhi hayo. Mpango huu ambao unaratibiwa na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa utasaidia kuunganisha nguvu za pamoja za wahusika wote katika kupambana na maradhi ya mripiko. Hivyo, tunawaomba viongozi na wananchi wote tuunge mkono juhudi hizi za serikali ili kupunguza athari zinazotokana na maradhi hayo.

Maeneo Yatakayopewa Kipaumbele 2018/2019

Mhe. Spika, kwa mwaka 2018/2019 serikali imeweka maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo kama ifuatavyo:-

i. Kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini, barabara na nishati.
ii. Kuimarisha zaidi utalii nchini.
iii. Kuimarisha viwanda vidogo vidogo kwa kuengeza thamani, bidhaa na ubora wa vifungashio.
iv. Kuimarisha kilimo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji, uvuvi na mifugo.
v. Kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, michezo na upatikanaji wa maji safi na salama.
vi. Kuendeleza tafiti mbali mbali za kiuchumi na kijamii kwa maendeleo ya nchi (*research for development*).
vii. Kukuza uwezo wa rasilimali watu katika fani adimu zikiwemo afya, viwanda, mafuta na gesi asilia ili kukuza ufanisi katika maeneo hayo.
viii. Kuimarisha ajira kwa vijana kwa kuwawezesha pamoja na kuwapatia taaluma na ujuzi stahiki.
ix. Utawala bora, uimarishaji wa taasisi na uwekaji mji katika hali ya usalama.

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI-MACHI) 2017/2018

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zilizo chini yake ilikuwa na programu 12 na programu ndogo 24. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi) 2017/2018, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake imechukua juhudi kubwa katika kutekeleza malengo iliyojipangia kupitia programu zake hizo. Kwa muhutasari utekelezaji wa shughuli za programu hizo ni kama ifuatavyo:

Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Spika, kupitia programu hii yenye programu ndogo moja, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeratibu na kutekeleza ziara moja ya nje na ziara 64 za ndani za Makamu wa Pili wa Rais zikiwa na lengo la kuimarisha uhusiano wa kiuchumi na kijamii baina ya Zanzibar na nchi zilizotembelea pamoja na kuhamasisha shughuli za maendeleo katika maeneo mbali mbali ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Aidha, Makamu wa Pili wa Rais alikutana na viongozi na wanadiplomasia wa nchi mbali mbali ili kubadilishana mawazo juu ya kuimarisha uhusiano baina ya Zanzibar na nchi wanazotoka viongozi hao. Makamu wa Pili wa Rais pia alifanya vikao na viongozi mbali mbali wa serikali ili kufuatilia utekelezaji wa sekta zinazosimamiwa na viongozi hao.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pia imepokea malalamiko, kero na migogoro ya wananchi yanayohusu masuala ya ardhi, nyumba, fidia na kesi za maeneo ya uwekezaji kwa kuyawasilisha kunakohusika na kufuatilia ushughulikiaji wake.

Mhe. Spika, maelezo ya kina ya utekelezaji wa programu hii yanapatikana ukurasa wa 11 – 12 wa kitabu chetu cha hotuba.

Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali

Mhe. Spika, ofisi kupitia programu hii iliyokuwa na programu ndogo tano, imechukua hatua mbali mbali za kuongeza uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa ikiwemo kufanya ukaguzi katika maeneo ambayo kwa kiasi kikubwa yana uwezekano wa kutokea maafa kama vile vyombo vya usafiri vya baharini na sehemu za kuhifadhia nishati ya mafuta na gesi ya kupikia. Aidha, ofisi imeendelea kutoa elimu ya kukabiliana na maafa katika jamii pamoja na kutoa huduma za kibinaadamu sehemu ambazo maafa yametokea.

Mhe. Spika,ofisi imeratibu kwa mafanikio makubwa sherehe za miaka 54 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari, 1964 pamoja na maadhimisho yote yaliyofanyika kwa kipindi hicho. Ofisi imeandaa na kuwasilisha Taarifa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 kwa kipindi cha miaka miwili (Oktoba 2015 – Septemba – 2017). Ofisi pia imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika maeneo mbali mbali ya Wilaya za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Ofis ya Makamu wa Pili wa Rais pia imefuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa kuhakikisha kuwa fedha zinapatikana kwa wakati na zinatumika kwa miradi iliyokusudiwa pamoja na kufuata taratibu zote zilizoelekezwa na Sheria inayosimamia Mfuko huo. Ofisi vile vile imeratibu shughuli za utafiti nchini kwa

kupokea maombi ya tafiti na kuratibu upatikanaji wa vibali kwa watafiti na kuendesha vikao vya kamati mbali mbali zinazohusika na masuala ya utafiti kitaifa. Ofisi pia imeratibu vikao vya mashirikiano baina ya sekta za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na vikao vya Kamati ya Pamoja vya SMZ na SMT.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imesimamia uendeshaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (*TASAF III*) ambao unatekelezwa katika Shehia 233 (Unguja 146 na Pemba 87). Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ofisi ilikadiriwa kutumia shilingi 13,028,827,000 ikiwa shilingi 7,808,592,000 malipo ya Kaya Masikini ni shilingi 5,220,235,000 malipo ya kazi za ajira za muda.

Mhe. Spika, ofisi kupitia Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dar es Salaam imeendelea kukutana na kufanya mazungumzo na Ofisi za Kibalozi zilizopo Dar es Salaam ili kutafuta fursa za mashirikiano baina ya Zanzibar na nchi za nje. Ofisi pia imeendelea kutoa huduma ikiwemo usafiri na *VISA* kwa viongozi na watendaji wa SMZ wanapokuwa Dar es Salaam.

Mhe. Spika, katika kuhakikishakuwa Watu wenye Ulemavu wanapata haki za msingi zitakazowasaidia katika maisha yao ya kila siku, Ofisi imeendelea kuchukua hatua mbali mbali ikiwemo kutoa mafunzo kwa wahusika juu ya usajili wa Watu wenye Ulemavu katika maeneo yote, kuratibu vikao vya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu, kutoa ruzuku kwa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu na kutoa vifaa visaidizi kwa watu wenye Ulemavu wa aina mbali mbali. Ofisi pia imeendelea kuhamasisha suala la kuwepo na kutumika kwa miundombinu rafiki kwa Watu wenye Ulemavu ambao tayari imeshatoa Muongozo wa suala hilo.

Mhe. Spika, maelezo ya kina ya utekeleaji wa Programu hii yanapatikana ukurasa wa 12 – 20 wa kitabu chetu cha hotuba.

Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa

Mhe. Spika, kupitia Programu hii ambayo hivi sasa imehamia katika wizara inayohusika na masuala ya habari, ofisi kupitia wakala wa serikali wa uchapaji, ilichapisha machapisho yote ya serikali na taasisi zake ikiwemo Magazeti Rasmi, Sheria, Miswada, Risiti za Serikali na mashirika na kazi nyengine za binafsi kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 20 wa kitabu chetu cha hotuba.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu

Mhe. Spika, Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi ya Pemba. Miongoni mwa kazi zilizotekelezwa katika programu hii ni kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika ngazi na fani mbali mbali. Ofisi imefuatilia na kufanya tathmini juu ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Idara na Taasisi zilizomo

katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili kubaini maendeleo ya utekelezaji wa miradi hiyo na kushauri hatua za kutatua changamoto zinazojitokeza. Ofisi pia imefanya tafiti mbili zinazohusu Mchango wa Programu ya Maendeleo ya Jamii (*TASAF III*) katika kubadilisha maisha ya kaya maskini na Tathmini ya Mfuko wa Maendeleo Jimbo (*CDF*) kwa jamii 2011-2015.

Mhe. Spika, ofisi kupitia programu hii imeendelea na taratibu za ujenzi wa nyumba ya makaazi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba ambapo tayari hatua za awali za ujenzi huo zimeshaanza. Maelezo zaidi yapo ukurasa wa 20 - 21 wa kitabu chetu cha hotuba.

Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali

Mhe. Spika, kupitia Programu hii Ofisi ya Baraza la Wawakilishi iliandaa na kufanikisha Mikutano Minne ya Baraza kuanzia Mkutano wa Saba hadi wa Kumi, ambapo kati yake Mikutano mitatu ilipitisha Miswada Tisa ya Sheria. Ofisi ya Baraza pia iliratibu kazi za Kamati za Kudumu za Baraza ambazo zilifanyakazi zake kwa mizunguko yote minne na kuwasilisha ripoti zake mbele ya Baraza la Wawakilishi na kujadiliwa. Maelezo zaidi yanapatikana ukurasa wa 21 – 22 wa kitabu chetu cha hotuba.

Programu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi

Mhe. Spika, kupitia Programu hii, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi imeratibu mafunzo mbali mbali kwa wajumbe na watendaji wa Baraza la Wawakilishi ili kuwaongezea uwezo wa kutekeleza majukumu yao. Ofisi ya Baraza pia iliratibu ushiriki wa viongozi na Wajumbe wa Baraza katika mikutano mbali mbali inayohusiana na masuala ya Mabunge ili kuimarisha uhusiano baina ya Baraza na Mabunge ya Jumuiya ya Madola na Kikanda na Kimataifa. Maelezo zaidi ukurasa wa 22 wa kitabu chetu cha hotuba.

Program ya Uendeshaji na Usimamizi wa shughuli za Uchaguzi

Mhe. Spika, kupitia Programu hii Tume ya Uchaguzi ilishiriki katika kikao cha mashirikiano na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika ngazi ya watendaji na kuzungumzia namna ya utekelezaji wa maagizo ya serikali katika masuala ya uchaguzi. Tume pia ilishiriki katika vikao vya Kamati za Kikanda vilivyojadili uimarishaji wa shughuli za uchaguzi kwa nchi wanachama. Sambamba na hilo, Wajumbe na Watendaji wa Tume walishiriki katika mafunzo yaliyohusu ushiriki wa wanawake katika demokrasia yaliyofanyika Pretoria- Afrika Kusini.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi imewasilisha kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ripoti ya utekelezaji wa majukumu yake ya kipindi cha miaka mitano (2013 – 2018) baada ya kumaliza muda wake. Maelezo zaidi ukurasa wa 22 – 23 wa kitabu chetu cha hotuba.

Programu ya Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kupitia Programu hii kwa kipindi cha Machi 2017/2018 imetekeleza kazi za kawaida za kiofisi pamoja na kuzifanyia matengenezo gari 18 za Tume sambamba na kuratibu matengenezo makubwa ya nyumba iliyokabidhiwa Tume na Serikali, ili kupunguza tatizo la uhaba wa maeneo ya kufanyia kazi kwa tume. Maelezo zaidi ukurasa wa 23.

Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Mhe. Spika, Programu hii inatekelezwa na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, kwa kipindi cha Julai - Machi, 2017/2018 ilitekeleza kazi mbali mbali ikiwemo kutoa mafunzo kwa wahusika wa mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kama vile masheha, wasimamizi wa sheria na mahakimu juu ya namna ya kukabiliana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini kwa kila mmoja kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mhe. Spika, tume pia iliendelea kutoa elimu kwa umma wakiwemo wanafunzi na wafanyakazi wa maeneo mbali mbali Unguja na Pemba juu ya madhara ya dawa za kulevya na namna ya kupambana nayo. Maelezo zaidi ukurasa wa 24 – 25 wa kitabu chetu cha hotuba.

Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Mhe. Spika, Programu hii inahusika na shughuli za uendeshaji za tume na kwa kipindi cha Julai – Machi 2017/2018, tume imeendelea kuwasomesha watendaji wake pamoja na kushiriki katika mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa inayoandaliwa ili kuweka mikakati imara zaidi ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Maelezo zaidi ukurasa wa 25 – 26 wa kitabu chetu cha hotuba.

Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI

Mhe. Spika, Tume ya UKIMWI kupitia Programu hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilihusika na kuandaa mikakati na miongozo ya mapambano dhidi ya UKIMWI pamoja na kutoa mafunzo kwa watendaji hasa walioko katika ngazi za wilaya, halmashauri na manispaa ambako shughuli za ugatuzi zinaendelea. Maelezo zaidi ukurasa wa 26 – 27 wa kitabu chetu cha hotuba.

Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI

Mhe. Spika, Programu hii ya Tume ya UKIMWI ilihusika na shughuli za uendeshaji wa Ofisi ya Tume na kuangalia maslahi ya watendaji. Miongoni mwa shughuli zilizofanywa ni kuendesha mikutano ya Bodi ya Tume ya UKIMWI na kamati zake pamoja na kufuatilia utendaji wa wahusika wa masuala ya UKIMWI hasa katika maeneo ya matumizi ya fedha na utekelezaji wa programu zilizopangwa. Maelezo zaidi ukurasa wa 27 – 29 wa kitabu chetu cha hotuba.

UTEKELEZAJI WA KIFEDHA

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kupitia Programu hizo 12 ilizokuwa nazo na Programu Ndogo 24 iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi 30,473,800,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2018 imetumia Shilingi 23,208,571,128 ambazo ni sawa na asilimia 76. Ofisi pia iliidhimishiwa jumla ya Shilingi 14,363,700,000 kwa kazi za Maendeleo na hadi kufika Machi 2017, imepatiwa Shilingi 10,489,390,666 ambazo ni sawa na asilimia 73 *(Angalia Kiambatanisho Nam. 1 na 2)* kwenye kitabu cha hotuba. Ofisi pia imekusanya Shilingi 13,530,000 ambayo ni asilimia 42 ya Shilingi 32,521,000 ilizopangiwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018**.**

MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na taasisi zake kwa mwaka 2018/2019 itatekeleza na kusimamia programu kuu 11 na programu ndogo 25. Itakumbukwa kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilikuwa na Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa ambayo kwa mwaka ujao wa fedha imeondoshwa kwetu. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa 2018/2019 imeongezewa Programu Ndogo mbili za Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mhe. Spika, mipango ya utekelezaji wa kila programu na Programu Ndogo za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake imeelezwa katika kitabu chetu cha hotuba katika ukurasa wa 30 mpaka 50.

MGAO WA FEDHA KWA PROGRAMU

Mhe. Spika, mgao wa fedha kwa programu 11 za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake ni kama ifuatavyo:

Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais, imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 1,291,205,007 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 6,623,884,277 kwa kazi za kawaida na Shilingi 14,182,700,000 kwa kazi za maendeleo ambapo Shilingi 123,000,000 kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shilingi 14,059,700,000 ni mchango wa wahisani.

Programu ya Uratibu na Utawala imepangiwa kutumia Shilingi 3,047,710,716 kwa kazi za kawaida na Shilingi 850,000,000 kwa kazi za maendeleo kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali imepangiwa kutumia Shilingi 7,682,159,250 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi imepangiwa kutumia Shilingi 12,672,640,750 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi fedha zake zinatoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Programu ya Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imepangiwa kutumia Shilingi 1,774,100,000 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya imepangiwa kutumia Shilingi 441,002,000 kwa kazi za kawaida na Shilingi 500,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Programu ya Utawala wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imepangiwa kutumia Shilingi 500,398,000 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI imepangiwa kutumia Shilingi 238,224,500 kwa kazi za kawaida.

Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI imepangiwa kutumia Shilingi 665,275,500 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, jumla ya makisio kwa Programu zote 11 za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni Shilingi 57,142,200,000 ambapo Shilingi 41,609,500,000 kwa kazi za kawaida na Shilingi 15,532,700,000 kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, mchanganuo wa mgao wa fedha kwa kila Programu na Programu Ndogo unaonekana katika Kiambatisho Nam. 3 na 4**.**

UKUSANYAJI MAPATO

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 142,653,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa	59,474,000
Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar	81,000,000
Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar	2,179,000

Jumla **142,653,000**

HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa kumalizia hotuba yangu hii nachukua nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohamed Aboud Mohamed na Naibu Waziri Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mihayo Juma Nhunga kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kunisaidia kuiongoza ofisi yetu kwa mafanikio makubwa. Nachukua nafasi hii pia kuwashukuru na kuwapongeza watendaji na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi yake wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Shaaban Seif Mohamed na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Abdallah Hassan Mitawi kwa jitihada wanazochukua za kuhakikisha kuwa ofisi yetu inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, naomba nirudie kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na kwa namna ya pekee kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa namna walivyoshirikiana na ofisi yangu katika mwaka 2017/2018, ni dhahiri kuwa ushauri na maelekezo yao waliyotupatia yametusaidia sana katika kufanikisha kazi zetu. Aidha, napenda kuwashukuru sana Washirika wa Maendeleo (*Development Patners*) na nchi marafiki ambazo zinaendelea kushirikiana nasi katika progarmu na miradi mbali mbali inayolenga kuwaletea maendeleo wananchi wetu. Miongoni mwao ni: Benki ya Dunia, Mashirika ya Umoja wa Kimataifa ikiwemo UNDP, UNICEF, UNFPA, WHO, WFP, UNAIDS, USAID, FAO na WIPO, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu Malaria na UKIMWI (Global Fund), Nchi za China, India, Finland, Norway, Japan, Marekani, Oman, Umoja wa Falme za Nchi za Kiarabu (UAE), Cuba na nyenginezo. Vile vile naishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Waziri MKuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo tumekuwa tunafanya kazi pamoja kwa mashirikiano ya hali ya juu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali na Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuwahudumia wananchi katika nyanja mbali mbali. Bila ya shaka uwezo, taaluma na rasilimali wanazotumia zimekuwa ni chachu kubwa katika kuiletea maendeleo jamii yetu. Navipongeza sana vyombo vyetu vya habari kwa kuendelea kuwapa habari, kuwaelimisha na kuwaburudisha wananchi pamoja na kutangaza moja kwa moja matukio mbali mbali ya kitaifa ikiwa ni pamoja na Mikutano ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mahonda kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutekeleza kazi zangu za Uwakilishi jimboni humo. Ushirikiano wao kwangu umenisaidia sana kuweza kumudu kufanya kwa ufanisi kazi za Uwakilishi na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Nawashukuru pia watu wote waliosikiliza na kufuatitilia hotuba yangu hii. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya 57,142,200,000 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake kwa ajili ya kutekeleza Programu nilizozielezea hapo awali.

Mchanganuo halisi wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	Shilingi 32,668,400,000
Ofisi ya Baraza la Wawakilishi	Shilingi 20,354,800,000
Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar	Shilingi 1,774,100,000
Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya	Shilingi 1,441,400,000
Tume ya UKIMWI Zanzibar	Shilingi 903,500,000
JUMLA KUU	**Shilingi 57,142,200,000**

Mhe. Spika, nakushukuru sana na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na Makamu wa Pili wa Rais na imeungwa mkono.

Sasa tutakwenda kwenye mijadala. Lakini kabla sijamwita Mhe. Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kiserikali. Kwanza napenda kutoa shukurani zangu za dhati sana kwa mujibu wa kanuni ya 96(2) ambayo inamtaka muwasilishaji kwa maana ya Waziri anaewasilisha hapa Bajeti yake atumie muda wa saa moja na nusu Mheshimiwa ametuokolea dakika kumi na tano katika muda wake ambao tumempangia. (*Makofi*)

Kwa hiyo, huo ni mwazo mzuri sana na wenye matumaini. Kwa hiyo, na litakuwa ni funzo kwa mawaziri wengine kuweza kutumia muda wako vizuri kama ambavyo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameweza kufanya.

Baada ya hapo sasa nichukuwe nafasi hii kumkaribisha na kumwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati wa Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kiserikali ambayo ndiyo kamati inayosimamia hii wizara ili aje awasilishe. (*Makofi*)

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati wa Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa niwasilishe Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayohusiana na Bajeti ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, Awali ya yote naanza kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba wa viumbe vyote ambaye ndiye mwenye kukirimu uhai kwa viumbe ambavyo vipo chini ya milki yake. Pia naendelea kuchukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na afya njema ambayo ametujaalia na kutuwezesha leo hii kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na kuwasilisha hotuba ya Kamati yetu na nyinyi Wajumbe wenzetu wa Baraza hili kuendelea kutusikiliza kwa makini. Hii ni dalili tosha kwamba wajumbe wa Baraza lako tukufu wana nia ya dhati ya kuwatumikia wananchi kwa lengo la kuishauri serikali na hatimaye serikali nayo iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa dhamira ya kupeleka mbele maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Pia, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpa afya njema, nguvu, hekima na busara Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Dkt. Ali Mohammed Shein, na kumuwezesha kuwatumikia wananchi katika utumishi uliotukuka zaidi. Hivyo sisi sote tuliopo chini yake hatuna budi kuiga na kufuata nyayo zake za utumishi uliotukuka kwa wananchi wetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amuongezee hekima na busara zaidi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili aweze kuiongoza nchi yetu na aweze kuifikisha kwenye mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Viongozi wote na hatuna budi kuwatumikia na kuwaongoza wananchi wetu ambao wana imani kubwa na Ssrikali yao, kwani huo ni wajibu wetu sote kuwatumikia wananchi hao kwa utumishi ulio bora.

Mhe. Spika, Kwa namna ya pekee sasa natumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuwa mstari wa mbele kuwatumikia wananchi katika mambo mbali mbali. Ni ukweli ni kwamba kila linapotokea jambo lolote linalohusu mustakabali wa nchi yetu kiongozi wetu huyu anachukuwa hatua za haraka kulitatua. Utaratibu huo wa kazi ambao amejipangia na anautekeleza ndio sababu iliyowafanya wananchi wawe na imani kubwa na Balozi Seif Ali Idd na kuamini kuwa ni kiongozi mchapa kazi na muadilifu.

Aidha, nitoe shukurani za dhati kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kwa utendaji wake bora katika kazi zake za kila siku, sambamba na Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mihayo Juma N'hunga, ambaye ni msaidizi wake wa karibu kwa namna ya pekee wanavyoshirikiana na Kamati hii katika Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa muda wote wa kazi za Kamati. Hadi hii leo hii kufikia kuisoma Hotuba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tumefanya nao kazi bega kwa bega kwa muda wote wa shughuli zote za Kamati kwa mwaka mzima bila ya kuchoka, na pale Mhe. Spika, inapotokea dharura ya kukosea au ya kukosekana kwa ajili ya majukumu mengine ya Kitaifa, viongozi hawa wanaiarifu Kamati yangu na kupanga utaratibu mwengine ulio bora ambao ulikuwa unaiwezesha Kamati hii kufanya kazi zake bila kukosa.

Mhe. Spika, Nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo nitamaliza kusoma maoni haya ya Kamati ya Ofisi ya makamu wa Pili wa Rais ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, bila ya kuwashukuru watendaji wao wakiongozwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo kwa ushirikiano mkubwa waliotupa.

Aidha, nichukue fursa hii pia kuwapa pole Wazanzibari wote na Watanzania kwa jumla na wananchi wenzetu na viongozi kwa namna moja au nyengine katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018, walipata misiba mbali mbali, ikiwa pamoja na maafa yanayotokana na mvua zinazoendelea kunyesha, iliyosababisha vifo au ugonjwa na maafa mbalimbali ya kibinaadamu. Tuseme tu kwa hiyo ni mipango ya Mwenyezi Mungu na tuwaombee wale waliopatwa na majanga haya Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira kwani hiyo ni kazi yake Mwenyezi Mungu Mwenyewe.

Pamoja na hayo tunapaswa kuchukuwa tahadhari na kujikinga na maafa mbali mbali ambayo yanaweza kutokea kwani kufanya hivyo sio tu kusaidia serikali kutekeleza majukumu mengine iliyojipangia bali pia kusaidia familia zenyewe kuepukana na maafa au majanga hasa yanayotokana na mabadiliko ya hali ya tabianchi yakiwemo mafuriko ambayo yamekuwa ni tatizo katika maeneo mengi ya hapa Zanzibar na jambo ambalo huziweka familia nyingi katika wakati mgumu.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa nianze kuanisha kwa muhutasari majukumu ya msingi ya Wizara ambayo kamati yangu inaisimamia yaani Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kimsingi wizara hii ambayo ni uratibu wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shughuli zote za Muungano kwa upande wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na Uratibu wa baadhi ya Miradi ya maendeleo inayosimamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano wa Tanzania ndani ya Zanzibar.

Aidha, majukumu mengine ya msingi ni pamoja na Kusimamia na Kuratibu Shughuli za SMZ Dar es salaam, Kusimamia Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na Kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Kuratibu Masuala ya Kukabiliana na Maafa, Kusimamia na Kuratibu Shughuli za Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Shuhuli za Watu wenye Ulemavu, Kusimamia Masuala ya UKIMWI, Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya, Kusimamia Shughuli za Tume ya Uchaguzi na Baraza la Wawaklishi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa utaratibu wa kibajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh. 57,142,200,000, ambazo zimetegwa kwa ajili ya shughuli zake za kawaida na Miradi ya maendeleo. Kimsingi shughuli zote kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambazo zitakuwa na Mafungu matano, ambazo ni Fungu C01- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Fungu CO2- Baraza la Wawakilishi, Fungu C03- Tume ya Uchaguzi, Fungu C04- Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti Dawa ya Kulevya, na Fungu C05-Tume ya Ukimwi.

Mhe. Spika**,** baada ya kueleza muhtasari huo wa mafungu ya Ofisi ya Makamu wa Pili Rais kwa ujumla, sasa kwa idhini yako naomba nitoe maelezo ya Kamati na yajikite kwa kila taasisi kwa mujibu wa Programu, shughuli na huduma zilizopangwa kutekelezwa ambapo kwa mwaka huu wa fedha Ofisi ya Makamu wa Pili Rais kwa ujumla wake imepanga kutekeleza Programu kuu kumi na moja (11) na Programu ndogo ishirini na tano (25) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kamati yangu imepitia fungu baada ya fungu, kwa ajili ya kupata ufafanuzi na hatimae kuridhia jumla ya fedha zote ambazo zinakusudia kutekeleza katika Programu tatu (3), kama ifuatavyo:

1. Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais,
2. Uratibu wa Shughuli za Serikali,na
3. Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais.

Programu ya Uratibu washughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Spika,Ofisi ya Makamu wa Pili ndio dira ya Serikali yetu kwani ni kiungo kikubwa sana baina ya Serikali na wananchi wake, kupitia Idara hii ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais ambayo, moja ya jukumu lake la msingi ni kupokea na kushuhulikia malalamiko na kutafuta utatuzi wa migogoro mbali mbali inayowasilishwa kutoka kwa wananchi kama tulivyoelezea hapo mwanzo kwamba Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Balozi Seif amekuwa akichukua hatua za haraka sana kutatua migogoro mara tu inapotokeza kwake. Idara hii ni miongoni mwa Idara muhimu kwenye wizara kwa hivyo, Kamati yangu inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushughulikia na kuyapatia ufumbuzi malalamiko 22 kati ya 35 yaliyowasilishwa kutoka kwa wananchi.

Kamati imefurahishwa sana na utatuzi wa migogoro na kwamba matumaini yetu migogoro iliyobaki itatuliwa kabla kumalizika mwaka fedha wa 2018/2019.

Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali

Mhe. Spika, ili kukamilisha utekelezaji wa Programu kuu hii yenye Programu ndogo saba kama ambavyo inaonekana kwenye hotuba ya wizara na kwa mujibu wa fedha ambazo wizara inaomba kuidhinishwa, ili ziweze kutumika kwa ajili ya kutekeleza Programu ndogo zifuatazo:

a) Kukabiliana na Maafa,
b) Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa,
c) Shughuli za SMZ,
d) Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar-Dar-es-Salaam,
e) Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu,
f) Usimamizi wa Mazingira,
g) Uratibu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mhe. Spika, kila Programu kati ya hizo ina umuhimu wake kwa nafasi yake. Hata hivyo Kamisheni kukabiliana na maafa ina majukumu ya kuratibu masuala ya kukabiliana na maafa pamoja na kusimamia utekelezaji wa mipango ya kukabiliana na maafa wakati wa maafa ya asili, ya dharura na pale yanapotokea na kutoa maelekezo yanayofaa katika utekelezaji wa mpango huo. Kamisheni imekuwa ikichukua juhudi mbali mbali kwa kuanzisha kamati za kukabiliana na maafa katika ngazi za wilaya na shehia, kuanzisha maghala na vifaa vinavyotumika wakati wa kukabiliana na maafa, vituo vya uokozi katika maeneo mbalimbali, vituo vya operesheni na masuala ya dharura pamoja na kutoa elimu kupitia vyombo vya habari ambapo lengo la kamisheni hii ni kulinda maisha ya watu na mali zao.

Kamati imeona kwamba bado Kamisheni inakabiliana na changamoto mbali mbali zikiwemo kutosimamiwa ipasavyo kwa sheria na kanuni mbali mbali zinazohusiana na masuala ya kukabiliana na maafa, zikiwemo sheria za mipango miji. Pia kutosimamiwa ipasavyo udhibiti wa vyanzo vya maji na utaratibu wa ujenzi na kupelekea watu kujenga mabondeni, chini ya milima na maeneo mengine hatarishi.

Aidha, elimu ya kukabiliana na maafa kwa jamii inaonekana bado ni ndogo, au kutokuwepo kwa mfumo maalumu wa kukabiliana na maafa utakaosaidia katika kujikinga, kujiandaa kukabiliana na maafa. Pia kamati imebaini kuwa wananchi wana tabia ya kujenga kwenye maeneo hatarishi, sambamba na tabia ya kutupa taka katika mitaro na kusababisha kuziba mitaro inayopitisha maji machafu wakati wa mvua jambo linalosababisha mafuriko kila wakati hasa kwenye kipindi cha Masika.

Hivyo, matumaini Kamati yangu na inatarajia kuona kuwa bajeti iliyoombwa kwa mwaka kwa fedha 2018/2019 itaweza kutatua baadhi ya kero na changamoto hizo ambazo Kamisheni inakabiliana nazo.

Mhe. Spika, suala jengine katika Programu hii ambalo Kamati yangu imeliangalia kwa umakini sana na kulipa uzito wa aina yake ni suala la Uratibu wa Shughuli za SMZ, na hasa ikizingatiwa katika masuala ya changamoto za Muungano. Ukweli ni kwamba licha ya kuwepo kwa Kamati ya pamoja ya Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utatuzi wa kero za Muungano ambapo baadhi ya kero ambazo zimeshapatiwa ufumbuzi wake lakini pia bado kuna baadhi ya kero nyengine ambazo hazijatatuliwa licha ya kuwa Kamati ya pamoja ya pande zote mbili inaendelea kuzishughulikia ili wananchi wa pande zote mbili za muungano waweze kufaidika na matunda ya Muungano huu ambao waasisi wake waliuanzisha na kuturithisha sisi vizazi vyao kwa nia njema na manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, Miongoni mwa changamoto hizi ni kwamba hivi karibu tulisikia mjadala unaohusiana na uingizwaji wa sukari inayozalishwa na kiwanda cha Mahonda cha Zanzibar kupelekwa katika soko la Tanzania Bara na manung’uniko ya baadhi ya wafanyabiashara wa Zanzibar wanaopeleka biashara zao Tanzania Bara kulipishwa ushuru mara mbili na kwamba wapo baadhi ya wana siasa walilichukulia kwa uzito mkubwa Masuala ya wafanyabiashara wa Zanzibar kulipa ushuru mara mbili hasa wanapoingiza biashara zao kule Tanzania bara.

Pamoja nakwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeratibu vikao 19 vya mashirikiano baina SMT na SMZ, bado inahitaji kuongeza kasi ili kuweza kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo zinazohusu Muungano wetu. Kamati kupitia Bajeti ya 2018/2019 inaishauri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhakikisha kuwa vikao vya uratibu wa Masuala ya Muungano vinafanyika kwa lengo la kuendelea kutatua changamoto zilizopo ili kuepusha changamoto kutoongezeka zaidi.

Kamati inatoa wito kwa Watanzania wote kwa pamoja tuiamini Kamati ya pamoja ya mawaziri wa pande zote mbili yaani ya Mawaziri wa SMT na wale wa SMZ, ambayo inafanya kazi nzuri iliyokabidhiwa na Viongozi wetu Wakuu ambao inashughulikia changamoto hizo lakini pamoja na hayo ni vyema ukaandaliwa utaratibu wa mfumo maalumu wa utoaji wa taarifa kuhusu mafanikio yaliokwishafikiwa katika vikao vinavyojadili masuala hayo.

Kamati inaamini kwamba kuwepo kwa mfumo wa kuwapasha habari wananchi wetu utatoa mwanga na muelekeo kwa jamii juu ya Serikali yetu zinavyofanya bidii ya kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazojitokeza na pia zitasaidia uelewa kwa wananchi kuwafamu wapo baadhi ya wanasiasa ambao hawautakii mema Muungano wetu.

Mhe. Spika,Programu nyingine muhimu ambayo Kamati imeifanyia kazi ni suala la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ya TASAF III.

Kamati imeona kwamba katika Mpango wa kunusuru Kaya Maskini (TASAF III), Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ imeweza kuratibu shughuli mbali mbali kwaUnguja na Pemba kwa mafanikio makubwa sana. Fedha zilizopangwa kufika katika Kaya hizo zilifika kwa wakati. Kamati inaipongeza Idara kwa kutelekeza mradi huu kwa ufanisi wa hali ya juu na kuweza kupunguza utegemezi kwa wanakaya masikini ambao wameweza kuibua miradi yao mbali mbali kama vile ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki na upandaji wa miti ya kudumu na kilimo cha mboga mboga.

Kwa ujumla katika mwaka wa fedha 2017/2018 mradi wa TASAF III, umeweza kuwasaidia baadhi ya wanakaya maskini kutoka katika umaskini uliokithiri na kuweza kujitegemea wenyewe hivyo Kamati imepata imani kubwa juu ya kuwepo na kuendelea kuwepo kwa mradi huo.

Kamati inaamini uwepo wa miradi hiyo ni msaada mkubwa kwa wanakaya hao kuweza kujinasua na umasikini uliokithiri kwani imewawezesha kujiajiri wenyewe.

Kamati pia inaamini kwamba katika bajeti ya mwaka 2018/2019, fedha zilizopangwa katika kutekeleza miradi hiyo itazidi kuzishughulikia kwa kina kaya hizo ili ziweze kujitegemea.

Mhe. Spika, Programu nyengine ndogo iliyo kwenye Progamu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, ambayo kamati imeona nayo ni muhimu kupewa mazingatio ya kipekee, ni juu ya Progamu ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar-Dar-es Salaam. Kwa lugha nyepesi tunaweza kusema kuwa Idara ya Uratibu wa Shughuli za

SMZ-Dar-es-Salaam, Idara hii ndiyo kioo cha Serikali yetu kwa upande wa Tanzania bara. Idara hii ina jukumu kubwa la kuziunganisha taasisi na wizara za Serikali zetu za Serikali ya Mapuinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano ambapo kila shughuli za kiserikali zinazofanyika Tanzania Bara, zinapaswa kuratibiwa na Ofisi hii.

Mhe. Spika,Ilikuwa ni changamoto ya muda mrefu ambayo Idara hii ilikuwa ikipambana nayo, kuhusu hali mbaya ya jengo ambalo ni Ofisi ya Uratibu wa SMZ iliyopo Dar-es-salaam, Kamati inaipongeza ofisi ya Makamu wa pili kwa kutumia bajeti ya 2017/2018 kwa kufanya kazi nzuri ya matengenezo ya sehemu ya jengo hilo ili liendane na hadhi ya Idara yenyewe.

Aidha, Kamati yangu imefarajika na inaishukuru Serikali kupitia Bajeti hii kuwezesha kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kulifanyia matengenezo makubwa hadi kuliezeka jengo hilo kama ambavyo ilishauriwa na kamati yetu, ukitilia maanani eneo na mazingira yanazozunguka Ofisi hiyo, hasa ukizingatia, jengo hilo hutumika na kiongozi wetu Mkuu, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, anapokuwa na vikao na mabalozi au viongozi wengine wakuu wa Mataifa mbali mbali.

Mhe. Spika, kutokana na unyeti wa Idara hii, na maingiliano yake yanayotokea baina ya watendaji wa Idara hiyo na idara nyengine za SMZ na SMT pamoja na Viongozi wengine wa kidiplomasia, Kamati inaipongeza Idara kwa kuwapatia mafunzo watendaji wake na ni lengo letu kwamba itaendelea kuwajengea uwezo wa fani mbali mbali. Kamati inasisitiza suala la mafunzo liwe ni la kuendelea kwa watendaji wengine kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa Ofisi hiyo.

Mhe. Spika, Programu nyengine ambayo Kamati yangu inaipa uzito katika Bajeti hii ni Programu ya Kuimarisha Ujumuishaji wa Watu Wenye Ulemavu. Moja katika jambo muhimu kwa watu wenye ulemavu ni ushirikishwaji katika wa mambo mbali mbali katika harakati za kimaendeleo kwa mujibu wa hali na uwezo wao. Kwa kuwa ni jukumu la Idara ya watu wenye ulemavu kufuatilia na kusimamia haki na fursa za watu wenye ulemavu katika jamii, Suala kubwa la kuzingatiwa ni mahitaji maalum kwa watu wenye ulemavu katika upatikanaji wa haki zao za msingi za kibinaadamu kama vile elimu, afya na ajira ni jambo la msingi.

Kamati yangu ilisikitishwa sana na hali ya watu wenye ulemavu kwa namna wanavyokosa mahitaji ya msingi kutokana na kutopewa kipaumbele kwa mambo yao mbali mbali yanayowagusa kama walemavu kwenye sekta za huduma, na hata uapatikanaji wa haki kwenye vyombo vya sheria.

Tukianza na miundo mbinu ya majengo mengi ya umma imekuwa ni changamoto kwa watu wenye ulemavu kuweza kuyafikia na kupata huduma kutokana na kukosekana kwa njia maalum za kupita kwa mujibu wa hali zao.

Mhe.Spika, hata jengo hili tukufu la watunga sheria limejengwa bila kuwazingatia wenzetu wenye mahitaji maalum.Kwa kweli hili hizi ni changamoto kubwa ambazo wenzetu hawa wanakabiliana nazo.

Aidha, Sekta ya elimu nayo imekuwa ni mtihani mkubwa kwa watu wenye ulemavu, licha ya Sera ya elimu ya mwaka 2006 kutambua elimu kuwa ni haki yao ya msingi,lakini hali halisi haiko hivyo, kwani kumekuwa na uhaba mkubwa wa Walimu wenye sifa za kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum na pia kuna upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia, matokeo yake imekuwa mzigo mkubwa kwa walimu wachache wenye kufundisha bila nyenzo.

Vile vile Sera ya elimu imekuwa ikikinzana na Sheria ya Elimu ya Mwaka 1982 ambayo haikuweka mkazo kwa watu wenye ulemavu.

Kamati inaipongeza sana Idara ya watu wenye ulemavu kwa kuandaa mkakati wa kupitia Sheria kwa lengo la kuandaa miongozo itakayosaidia watu wenye ulemavu kupata haki zao za msingi.

Kamati yangu inaishauri Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kuiga mfano mzuri wa skuli binafsi ya JABAL HIRAA ya Fuoni kuhusu namna ya kuwashirikisha walimu wote katika mafunzo ya elimu mjumuisho na hata wanafunzi wasiokuwa na mahitaji kama hayo kwamba wanafundishwa elimu mjumuisho. Kwani kuwafundisha watoto wote hata wasiokuwa walemavu itakuwa ni faraja kubwa hata kwa familia pale inapotokea kuzaliwa mtoto ambaye ana tatizo la kuzungumza. Hali hiyo inaweza kusaidia ufumbuzi wa changamoto nyingine kwa watu wenye mahitaji maalum kama hayo kwa hivyo Mhe. Spika tunaiomba Wizara ya Elimu iliangalie jambo hili la kuwafundisha watoto wetu elimu mjumuisho kutoka mwanzo madarasa ya chini.

Mhe. Spika, sekta ya afya nayo imekuwa ina changamoto ya aina yake kwa watu wenye mahitaji maalum wanapokwenda kutafuta huduma wanasumbuka sana kuzifikia huduma za kitabibu, kutokana na miundo mbinu ya hospitali zetu na vituo vya afya. Lakini hata wale wanaoweza kuzifikia mara nyingine wakumbana na changamoto kutoelewa lugha baina yao na matabibu kutokana na matabibu hao kutoelewa lugha ya alama na pia kutokuwepo kwa mkalimani katika maeneo kama hayo anayefahamu hizo tafsiri za lugha za alama. Jambo hilo ni kikwazo ambacho pia watu wenye ulemavu wanakabiliana nacho na hatimaye kukosa huduma wanayoitegemea. Licha ya kwamba Idara ya watu wenye ulemavu inajitahidi kuwapatia huduma watu wenye ulemavu lakini wamekuwa wakikosa baadhi ya mahitaji hayo ya msingi.

Jambo jingine kwenye sekta ya afya ni kukosekana kwa viungo bandia uhaba wa dawa za kupaka kwa walemavu wa ngozi na kukosekana kwa madakatari bingwa na huduma bora kwa walemavu wa ngozi ambao wamepata SARATANI YA NGOZI na kadhalika.
Kamati inaipongeza sana idara ya watu wenye ulemavu kwa kuanzisha utaratibu wa kuwapatia bima za afya watu wenye ulemavu ukweli ni jambo la kuwapongeza kamati inasisitiza huduma hii iweze kupatikana kwa walemavu wote.

Kamati yangu inaishauri Serikali iongeze nguvu zake za kibajeti kwa Idara ya watu wenye ulemavu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya,Wizara ya Elimu, pamoja na Wizara Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ambopo baadhi ya skuli

na vituo vya afya vimegatuliwa ili kuweza kuisaidia Idara ili iweze kukidhi majukumu na mahitaji mbali mbali ya watu wenye ulemavu.

Suala jingine ambolo ni sugu kwa watu wenye ulemavu ni suala la udhalilishaji dhidi yao. Ni ukweli kwamba suala la udhalilishaji kwa watu wenye mahitaji maalum lilikuwa linaongezeka kila siku. Kamati yangu inaishukuru Serikali sana kupitia Wizara ya kazi, Uwezashaji Maendeleo ya Wanawake, Wazee na Watoto kwa kuyafuatilia kwa karibu sana malalamiko dhidi ya watu wenye ulemavu na kuhakikisha sheria inachukuwa mkondo wake na kwamba hatua kali zinachukuliwa dhidi ya wale wote watakaohusika na tatizo hili la udhalilishaji wa watu wenye ulemavu.

Kamati yangu inaipongeza sana serikali kwa kuona umuhimu kuwa na Baraza la Watu wenye Ulemavu ambalo linaweza kutumika kama Jukwaa lao la kupitishia mahitaji yao ya msingi Baraza limeweza kutumika kama sehemu muhimu ya kujadili na kutatua changamoto mbali mbali zinazohusu mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Kama inaipongeza wizara kwa kuwaongezea bajeti Idara ya Watu wenye Ulemavu katika Programu Ndogo ya Usimamizi ya Watu wenye Ulemavu, ingawa bado kamati inaamini kwamba bajeti hiyo ni ndogo, lakini taratibu tutakwenda tutafika na mahitaji ya idara hiyo *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu yataweza kufikiwa pale tulipopakusudia. Kwa hivyo, bado tunaiomba serikali hasa wizara ambazo tumezitaja kuiangalia kwa jicho la huruma idara hiyo pale yanapojitokeza mahitaji yanayowahusu watu wenye mahitaji maalum.

KAMISHENI YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, kutokana na mabadiliko ya kiwizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeongeza Programu Ndogo mbili ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Kupitia programu hizo ambazo zina lengo la kuimarisha hali ya mazingira Zanzibar na kuiandaa jamii kujihami kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Kamati inaamini kwamba Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA) zina majukumu makubwa ya kuhakikisha kwamba uhifadhi wa mazingira unapewa uzito unaostahiki na kila mmoja wetu. Suala la taaluma kwa wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni muhimu sana na yanahitaji kupewa uzito wa aina yake.

Mhe. Spika, kwa kuwa taasisi hii pia inahusika na tathmini ya hali ya mazingira kabla ya kuanza kwa miradi mbali mbali inapaswa kujipanga vizuri kuhakikisha kwamba kila mradi unaotakiwa kufanyiwa tathmini hiyo unafanyiwa kwa kufuata taratibu na kwa wakati, ili kuepuka athari kwa wananchi wetu na kuhakikisha miradi hiyo inatoa tija badala ya kuleta maafa na athari za kimazingira kwa wananchi wetu.

Aidha, kamati inazishauri taasisi zinazosimamia mazingira zisimamie majukumu yake zihakikishe kuwa utaratibu wa malipo unawekwa vizuri, ili mapato ya serikali yasiweze kupotea ikiwa ni pamoja na kuandaa kanuni za malipo, ili kuwa na utaratibu mmoja kwa

watu wote. Aidha, suala la kuwa na mfumo wa kieletroniki kwa kwa ajili ya kuweka kumbu kumbu za kimazingira ni muhimu sana.

Vile vile, kamati inashauri kuanzishwa vikundi vya kuhifadhi mazingira kuvindeleza na kuvipatia msaada hasa kwa yale maeneo ambayo bahari imekula sehemu kubwa ya ardhi kama maeneo ya Msuka kwa upande wa Pemba na ukanda wote wa utalii wa Mashariki ya Kisiwa cha Unguja. Aidha, Sera ya Mazingira ambayo ni muongozo wa masuala hayo inashauriwa itafsiriwe kwa Kiswahili, badala ya lugha ya Kiingereza iliopo hivi sasa, kwani wengi wa walengwa wetu wananchi wanahitaji kuifahamu sera hiyo na wanazungumza lunga ya Kiswahili.

Pia, kamati inashauri jitihada za makusudi ziandaliwe na kuwekewa mikakati ya usimamizi, ili kuhakikisha kwamba wakandarasi wa ujenzi wa barabara wanapanda miti mara baada ya kukamisha kazi ya uchimbaji wa kifusi kwa ajili ya ujenzi wa barabara, ili kuepusha uharibufu mkubwa wa mazingira na kuwacha mashimo makubwa baada ya kumaliza kazi za ujenzi wa barabara hizo.

Mhe. Spika, kamati inaamini kwamba bajeti ya mwaka 2018/2019 itatumika vizuri na kuweza kufikia malengo tuliyoyakusudiwa.

TUME YA MADAWA YA KULEVYA

Mhe. Spika, suala la madawa ya kulevya ni suala la kitaifa, na ni vita na inahitaji uzalendo wa hali ya juu. Bajeti hii kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, imetenga fedha kwa lengo la kutekeleza utekelezaji wa shughuli zote za tume, kupitia Programu Kuu mbili ambazo ni pamoja na Programu ya Udhibiti wa dawa za kulevya na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Dawa za Kulevya.

Mhe. Spika, kamati inaipongeza serikali kwa kuiangalia Bajeti ya Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti dawa za Kulevya imeongezeka kwa mwaka 2018/2019. Kamati yangu imekua ikifanya kazi kwa ukaribu na ushirikiano mkubwa na tume hii, hivyo inafahamu vizuri na inazielewa vyema changamoto zake ambazo pia zinaambatana na ufinyu wa bajeti ambao ulikuwa ukiikabili idara hii hapo kabla. Hivyo basi, kwa ongezeko hili la bajeti kwa mara hii ni imani yetu wana kamati yangu kuwa, tume itaweza kutekeleza majukumu yake ya msingi, kwa ufanisi zaidi kulinganisha na mwaka wa fedha unaomalizika.

Mhe. Spika, geografia halisi ya Visiwa vya Zanzibar, ni miongoni mwa moja ya changamoto ambazo zinaikabili Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa ya Kulevya, ukilinganisha na uwezo wa kifedha na nyenzo za kufanyia kazi Tume hii ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Tume hii inatekeleza Programu Ndogo ya Udhibiti na Usambazaji wa Dawa za Kulevya ikizidi kuwa ngumu, hali ya kuwa ni ngumu kutokana na kuwepo wa bandari bubu nyingi sana. Mfano Mkoa wa Kaskazini Pemba peke yake una bandari bubu 168, ambazo zinaweza kutumika kwa uhalifu wa aina mbali mbali na hata uingizwaji wa dawa za

kulevya. Ni ukweli usiofichika kupitia bandari hizo bubu ambazo zisizo rasmi, dawa za kulevya zinaweza zikaingizwa na udhibiti wa bandari hizo bado ni mdogo mno. Katika utekelezaji wa bajeti hii, ambayo Programu Ndogo ya Udhibiti, Uingizaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya imeongezewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa asilimia kubwa ukilinganisha na bajeti ya 2017/2018.

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, samahani kidogo. Waheshimiwa Wajumbe, kanuni zetu, kwenye kanuni ya 96 haielezi mwenyekiti yeye atumie muda gani, imeeleza tu waziri atakayekuwa anawasilisha atumie sio zaidi ya saa moja na nusu. Kwa hivyo, kama nitaacha hivi naona tutaelekea kwenye saa nzima ambayo atakuwa anawasilisha Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka nimuombe Mhe. Mwenyekiti, kwamba amalizie halafu aombe kwamba hiyo hotuba yake kama ilivyoiingie kwenye Hansard. Lakini pamoja na hivyo pia nitamuombea Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili ile hotuba yake, kwa sababu na yenyewe inaonekana kama alisoma muhtasari iingie kama ilivyowekwa mezani, iingie kwenye *Hansard* nayo vile vile.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, endelea.

Mhe. Omar Seif Abeid: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, namalizia imebaki page moja. Kamati yangu inaamini kwamba chini ya usimamizi mzuri wa Mkurugenzi wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu wa Dawa za Kulevya, Programu hii itatekelezeka kwa *ufanisi* mkubwa kutokana na ongezeko la kibajeti kwa mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, kamati yangu inaamini kwamba ushindi wa mapambano dhidi ya madawa ya kulevya utapatikana iwapo tu sisi sote tutaondoa rushwa muhali. Wito wa kamati yangu ni kwamba mapambano dhidi ya dawa za kulevya iwe ni endelevu na kwa wananchi wote, ili wajuwe sote katika nchi hii ni waathirika.

Mhe. Spika, programu nyengine Tume ya Uchaguzi inatekeleza programu mbili ya Ofisi ya Tume ya Uchaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Programu hizo ni ya uendeshaji wa shughuli za uchaguzi na kamati imepitia shughuli zote zilizokusudiwa katika utekeleza wa bajeti hii. Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi kwa kupitia programu hizo imeridhia bajeti hii.

Mhe. Spika, Tume ya Ukimwi. Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka 2018/2019 Tume ya Ukimwi ina programu kuu mbili ambazo ni uratibu wa muitikio wa kitaifa wa ukimwi na uendeshaji. Mhe. Spika, kamati yetu imepitia kwa kina na imeridhia kupitishwa kwa fungu hilo.

Mhe. Spika, kwa bajeti ya mwaka 2017/2018 Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kwa mwaka wa fedha

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, naomba uelekee kwenye kuhitimisha hiyo hotuba ili tuweze angalau kuwapa wajumbe wawili basi waweze kuchangia.

Hitimisho

Mhe. Omar Seif Abeid: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa kumalizia katika maoni ya kamati yangu kwa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, naliomba Baraza letu tukufu liweze kuwaidhinishia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais jumla ya shilingi bilioni 59. *(Makofi)*

Jumla ya eee milioni 59. Samahani. bilioni 57 ambazo zimeombwa kwa kupitia Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, mwisho napenda kutoa shukrani zangu kwako wewe Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kuwasilisha hotuba hii. Pia napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wenzangu wote wa kamati hii ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, na kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niwatambuwe.

1. Mhe. Omar Seif Abeid	Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mjumbe
4. Mhe. Ame Haji Ali	Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Mjumbe
6. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	Mjumbe
7. Mhe. Mussa Ali Mussa	Mjumbe

Bila ya kuwasahamu makatibu wangu wawili ndugu Karima Abdulwahabi ambaye ni katibu tumefanyanaye kazi kwa muda mrefu kwa umakini zaidi na msaidizi mwenzake ndugu Talib Enzi Talib.

Mhe. Spika, mwisho napenda kutoa shukrani kwa wajumbe wote wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa umakini. Naomba kutoa hoja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa tuanze kuchangia na moja kwa moja nitamuita mchangiaji wetu wa mwanzo Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Shehe Hamad Mattar ajiandae.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufikia leo na kuichangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Rais wetu za Zanzibar na Mwenyekiti wetu wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia nchi yetu kuwa na amani na utulivu na kuhakikisha kwamba Wizara ya Fedha wanafanyakazi nzuri ya kukusanya mapato na kuweza kufanya kazi zetu vizuri. Lakini nampongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kwa hotuba yake au uwasilishaji wake mzuri. Kwa hivyo,

nampongeza yeye mwenyewe waziri wake Mhe. Mohamed Aboud Mohamed, Naibu Waziri wake Mhe. Mihayo Juma N'hunga, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya na kuleta ufanisi katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi kwanza naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja sina matatizo na hasa nikizingatia kwamba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ni mtendaji mkuu wa shughuli zote za serikali, anafanyakazi zake zake vyema yeye na watendaji wake bila ya matatizo. Kwa hivyo mimi nitasema vifungu vyangu viwili au vitatu tu.

Kwanza Mhe. Spika, niseme tu kwamba Ofisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais inaratibu shughuli zote za mambo yetu ya maendeleo. Kwa hivyo, nakuja kwenye mambo ya miundombinu. Tumeona katika kitabu hiki kwamba kuna mpango mkubwa ambao tunataka kujenga barabara yetu ya kutoka Bububu mpaka Mkokotoni, suala hili nalipongeza sana. Lakini niseme tu kwamba pamoja na pongezi hizo natoa ushauri wa mara kwa mara Mhe. Spika, umefika wakati tubadilike katika ujenzi wa barabara, tuhakikishe barabara zetu zina viwango vya kutosha.

Mhe. Spika, enzi ya zamani kulikuwa na gari ndogo tu hapa, leo kuna magari tani 30 na tani 25. Kwa hivyo zinazidiwa viwango, ikifika mvua basi barabara hazina thamani tena zinakufa. Kwa hivyo, kiwango ni jambo la muhimu kwa taasisi zinazohusika zisimamie vyema.

Lakini pili Mhe. Spika, zuri katika hilo hilo barabara ukiijenga maana yake iwe na michirizi ya kumwagia maji, lakini pia iwe na kingo za kuzuwia mmong'onyoko siku za mvua. Barabara zetu nyingi ukitembea katika baadhi ya maeneo zina misumeno ndani yake, kwa sababu ikija mvua inamong'onyoka inakwenda na maji. Kwa hivyo, tubadilike. Tukitembea kwa wenzetu tunakuta mabadiliko makubwa katika ulimwengu wetu wa barabara zetu.

Jengine Mhe. Spika, niseme tu kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kazungumzia suala la maji, suala la maji pamoja na kuzungumza na mimi naliunga mkono. Lakini niwapongeze sana watu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati Mhe. Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wake wote, hasa Mamlaka ya Maji wanafanyakazi nzuri lakini bado mheshimiwa kuna hujuma za makusudi za kurudisha nyuma mafanikio haya.

Kwa mfano mimi katika Jimbo langu la Kijitoupele nasikitishwa na nalaani kwa nguvu zangu zote, nimelaani na ninazidi kulaani kisima cha mita 80 kimechimbwa, kibanda kimeshajengwa kuweka umeme kufanyakazi. Mimi nawaita maharamia wasiotaka maendeleo katika nchi hii wamekitia mawe, majiti na machakacha mbali mbali kisima kimebakia mita 28, mita 28 maji yapo, lakini kama hakikwenda chini basi maji yake yametuathiri. Nasikitika tena nimesikitishwa na sina imani na wahalifu hao na Mwenyezi Mungu atatulipia hapa hapa duniani.

Jengine Mhe. Spika, ni kuhusu huduma za afya. Sasa hivi tupo katika ugatuzi, niishukuru serikali kwa mpango wake mkuu, lakini najua kazi hii kubwa iko kwenye Halmashauri zetu au Manispaa. Kwa hivyo, niombe sana kama sisi wengine tuna Vituo vya Afya. Tunamshukuru sana Mhe. aliyekuwa Mbunge Mhe. Sereweji na Mhe. Shamsi Vuai wakati alipokuwa Mwakilishi sasa hivi Mbunge wangu katika Jimbo la Kijitoupele walijenga hospitali nzuri na ipo na mimi niliwaahidi wananchi wangu nitaifanyia kila njia hospitali hii imalizwe na imefikia hatua kubwa madirisha, plasta na mambo yote nje na ndani tayari na fitting ya umeme tayari na milango ilitakiwa 16 imebakia 8.

Kwa hivyo, niseme tu kwamba naiomba serikali sana, niiombe Halmashauri zetu kwa kupitia Waziri wetu wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, izifuatilie hospitali hizi ili zimalize kwa wakati na wananchi wetu wafaidike. Hospitali ya Magirisi kama itamalizika Mhe. Spika, itafaidisha watu zaidi ya 40,000, kina mama wajawazito na watoto. Kwa hivyo, watu wa Pangawe, Kwarara, Tomondo, Kijitoupele na watu wa Melinne na kwengineko watakuja kujifugua pale Mwenyezi Mungu Inshaallah atatujaalia muda utafika.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakina mama mtusaidie michango mbali mbali, ili tuisaidie Wizara yetu ya Tawala za Mkoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum tulimalize jengo letu hilo.

Jengine Mhe. Spika, kuna hili suala la mtambuka. Mhe. Spika, kwa masikitiko niseme tendo la udhalilishaji linaendelea siku hadi siku. Mimi juzi tarehe tano nilipigiwa siku kutoka Makunduchi na Makamu Mwenyekiti wangu Salha, akaniambia kuna taarifa kwamba kuna mtoto kaibiwa, mtoto huyo anatoka Fuoni Jitimai. Nikatoka mimi mbio nikafukuzia mpaka polisi Malindi, nilipofika polisi wenyewe wale watu walipeleka haraka taarifa, maana alitokea mama mmoja anaomba kazi jioni, akasema mimi naomba kazi sina kazi natokea Tanzania Bara, alipofika pale katika kuomba kazi akaambiwa hapa kazi hakuna, lakini kwa kuwa huna pa kwenda sasa hivi leo utalala hapa. Kulala pale alfajiri akatoka naye yule mtoto wa miaka karibu miwili mtoto wa kiume lakini, katoka akenda naye huko. Wenyewe waliposhtuka yule mama hayupo na mtoto hayupo wakenda kutoa taarifa polisi. Kwa bahati nzuri na nalipongeza sana Jeshi la Polisi Kituo cha Malindi, nawapongeza kwa ujasiri wao na kazi nzuri waliyoifanya, *OCD* na watendaji wake wamefanya kazi nzuri, wakatoka na wazee wao wakaenda mpaka Boti mtoto akakutikana yuko hivi hiyo kesi imetokea juzi. Kwa hivyo tujue kwamba udhalilishaji na ukatili kwa watoto jambo hili linaendelea, Serikali lazima iwe makini sana kwa hili.

Mhe. Spika, lakini jengine Mhe. Spika, kwakuwa tendo hili ni la ukatili sana kuna kijana wangu wa Jimbo langu la Kijitoupele nimeipata taarifa jana kaibiwa leo ya nane, mtoto wa kiume yuko Form I, kaitwa tu *time* za magharibi, kaitwa fulani njoo utupelekee mzigo kwenye gari fulani hajaonekana mpaka muda huu tunaozungumza hapa. La kusikitisha nilisikia muhalifu huyo ana tabia mbaya anaharibu watoto wa watu, kwa hivyo hilo tendo alilifanya mpaka sehemu nyengine kafikia Mfenesini huko alipokwenda Mfenesini kakamatwa akajanae mpaka kituo cha Polisi cha Kijitoupele, wakathibitisha huyu ndiye tendo anayowafanyia wengine ndio lilelile lakini bahati mbaya lililotokea Mheshimiwa yule muhalifu katoroka katika mazingira yasiyojulikana, mpaka sasa hivi hajapatikana na

mtoto hajaonekena mpaka muda huu. Kwa hivyo nasema kwa uchungu naiomba serikali tuwe makini watoto wetu wapo katika mazingira magumu ya maisha yao. Mtoto yoyote ni wetu kila mtu mtoto hapa mtoto wa mwenzake na yeye ni wake na yeyote hujui atokufaa, kwa hivyo niseme Mheshimiwa serikali iwe makini.

Mhe. Spika, la mwisho naokoa muda, limezungumzwa suala la maafa, tunajua hali ya maafa inaendelea lakini serikali ninaipongeza kwa juhudi zake imo mbioni kutika kulitatua tatizo hili hasa tulipopata taarifa ya Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, kusema kwamba panatafutwa ufumbuzi kama litajengwa Daraja hapa Mwanakwerekwe na Kibondemzungu au patafanyiwa utafiti wowote lakini naiomba serikali tufanye hima tusingojee mpaka masika yajayo. Mimi naona uchungu sana Mhe. Makamu wa pili kila siku anafungua ziara leo katizame maji yamefurika, leo sijui katembelea hapa nyumba zimefunikwa na maji, jambo la aibu tuondokane na hayo,tukate pua tuunge wajihi.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa watu wenye ulemavu wamezunguzwa sana, Mhe. watu wenyeulemavu wana matatizo yao mengi lakini naishukuru serikali kwa juhudi zake mbalimbali mimi natoa ombi moja tu, naiomba serikali kwa makusudi tunao masheha katika maeneo yetu, tunao wananchi mbalimbali, watu wenyeulemavu wapo wengi lakini bahati mbaya hawafikiwi. Kwa hivyo pawe na utaratibu maalum kujisajili ni jambo moja lakini na kumfikia ni jambo la pili, kwa hivyo naiomba serikali ili tushirikiane na sie wawakilishi, wabunge na madiwani tuhakikishe kwamba tunawafuatilia vijana wetu waliokuwamo mitaani nawao waweze kupata misaada yao mbalimbali katika maisha yao.

Mhe. Spika, baada ya hayo niseme tu kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja mimi na wananchi wangu wote wa Kijitoupele walonichagua na wasionichagua. Ahsante Mheshimmiwa. *(Makofi)*

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, Ahsante Mhe. Spika nami kwa kunipa fursa hii kutumia dakika ziliopo kidogo kwa kuweza kutoa mchango wangu. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametujaalia uhai na tukaweza kurudi hapa tukiwa wazima na wale ambao hawakuwahi kurudi Mungu awajalie afya njema huko aliko na tuweze kuungana pamoja.

Mhe. Spika, nami niuungane na wenzangu kwa hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuwashukuru sana na kuwapongeza viongozi wetu hawa wawili, Rais wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zao ambazo wamezifanya kwa nchi yetu kuwa salama na tukaweza kufanya shughuli zetu bila ya matatizo, amani inaendelea na kukemea vikali wale ambao watajaribu kuvuja amani ya nchi hii, mimi nawapongeza sana. Lakini pia niwapongeze pia kwa kusimamia kunyanyua uchumi wetu, nchi hizi mbili sasahivi zimekuwa na uchumi wa hali ya juu kabisa kimaendeleo na mafanikio mazuri katika ukanda wa Afrika Mashariki inaonesha kwamba uchumi wetu unakua siku hadi siku. Niwapongeze sana kwa kusimamia hili pamoja na viongozi wengine.

Mhe. Spika, niungane katika hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi pale anaposema kwamba wale wote ambao kwa njia moja au nyengine wanashirikiana na watendaji wa Taasisi zetu hapa nchini kwa ajili ya kuzoretesha uchumi wetu, awe mtu huyu ni mmoja mmoja, au ni Taasisi watashughulikiwa na mimi naongeza kwamba na wale Wakandarasi ambao pia wanatumiwa kufanya mikataba isiyokuwa mizuri au kufanyakazi isiokuwa nzuri chini ya kiwango na baadae kuitia hasara serikali naomba washughulikiwe mara moja watu kama hawa.

Mhe. Spika, pia vile vile nina faraja sana kusikia taarifa ya kwamba nchi yetu suala zima la utafutaji mafuta limefikia hatua nzuri naomba sana kwamba itakapofika wakati nao wananchi waendelee kujuilishwa hatua baada ya hatua namna gani serikali inafaya juhudi kuona kwamba mafuta au gesi asilia inapatikana hapa nchini kwa faida ya nchi hii.

Mhe. Spika, pamoja na hayo kidogo nina masikitiko katika Baraza letu hili, kama ninavyojua kwamba Bajeti ya serikali, bajeti hii tuliyonayo tunaambiwa kwamba ni bajeti ya wananchi na wananchi wanahaki ya kuchangia, lakini sasa upatikanaji wa vitabu hivi naona hauko katika hali nzuri kwasababu unaweza kupewa kitabu leo kesho uanze kujadili, ni wakati gani yeye mwananchi ataweza kupata kitabu hichi na mkakaa pamoja katika kuchangia halafu nayeye aweze kutoa maoni yake aweze kusikiliza katika Baraza hili, muda ni mchache sana. Naomba sana marekebisho yafanywe uonekane muda gani muwafaka wakuweza kutoka vitabu vya bajeti ili ile zana mawazo kutoka kwa mwananchi ipatikane.

Mhe. Spika, lakini niende tena katika masikitiko yangu ya mradi wa ujenzi wa nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais, nimeona katika kitabu hichi cha hotuba kwamba walipangiwa jumla ya *shilingi milioni mia tano,* katika kutengeneza makao ya nyumba Mhe. Makamu Pili wa Rais lakini hatimae kupatikana *milioni kumi na tatu pointi nane.* Kwa kweli fedha hizi zitaweza kufanya kitu gani mwaka umekwisha haijulikani kwamba fedha hizi zimetumika kwa kitu gani. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja basi anieleze kwamba fedha hizi *milioni kumi na tatu pointi nane* zimetumika kwanini. Na kwanini fedha hizi hazikupatikana ukiangalia bajeti ni nzuri imepatikana katika vifungu mbali mbali si chini ya asilimia hamsini vyote vimepata bajeti nzuri lakini bajeti ya ofisi hii ya ujenzi wa nyumba imekuwa ni ndogo sana, lakini pia vile vile katika suala zima nalo suala la mapato.

Mhe. Spika, Wizara hii ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ilipangiwa mapato ya *bilioni thelathini na mbili pointi tano,* lakini naona ni *milioni kumi na tatu pointi tano,* sawa na asilimia arubaini na mbili sikui ni sababu gani zilizopelekea kwamba mapato kushuka kiasi hichi hata asilimia hamsini haikufikia naomba utakapokuja uweze kutupa maelezo ya kwanini hayakufikiwa malengo, na kwanini kupata asilimia hii ndogo.

Mhe. Spika: ukiangalia suala zima lile la vitabu hapa ni kutokana kwamba nashangaa wakala wa uchapaji wamepata bajeti nzuri lakini kwanini hawakupata vitabu kwa wakati, hapo nimesahau katika kuweka sawa pale, naomba niweke sawa hapo kwamba asilimia tisini na tisa walipata hapa lakini kwanini hawakuweza kupata vitabu kwa wakati. Aidha ninasikitishwa sana katika mgao, katika mgao wa fedha katika *program* ndogo ya

2018/19 kwenye kiambatanisho namba 3 cha kitabu hichi kuona kwamba uongozi wa utawala wa Baraza la Wawakilishi sijaona makisio ya *program* ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba. Jee, wafanyakazi hawa watafanyakazi vipi kazi kule Pemba, hapa sikuona katika makisio wala makadirio yaliyowekwa isipokuwa mwaka 2019/2020 ndio nimeyakuta. Hapa nataka nipate maelezo, hawa watafanya kazi vipi kuna umuhimu gani kuwa na ofisi kule, nini kimepangwa katika kuona kwamba yataweza kutekeleza kazi zao, nayo ili ni ofisi mara wawakilishi wanakwenda kule kama juzi tuliona baraza ilifanya shughuli zake pale sherehe za Mei mosi.

Mhe. Spika, niende katika suala zima la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ninavyoelewa ndio inayoratibu shughuli nyingi za serikali hapa, lakini ofisi hii inatumiwa vibaya wakati mwengine niseme inatumiwa vibaya wakati mwengine niseme inatumiwa vibaya kwamba, mnamo tarehe 19/4/2018 vyama vya wafanyakazi ikishirikiana na ofisi ya *labor* ilikwenda katika taasisi moja kufanya ukaguzi lakini wakasitishwa mara moja wakaambiwa ofisi ya Makamu wa Pili Rais imesema waondoke watu wale sidhani kwamba jambo hili ni ni kweli lakini nilisema nitalileta hapa, kwa hivyo kama ni kweli alitolee maelezo atakapokuja kufanya majumuisho hapa. Kwa sababu vyama vya wafanyakazi ni sehemu moja ambayo inasaidia serikali kuona kwamba waajiri na waajiriwa wanafanya majukumu yao.

Sasa leo kama wanasitishwa na watu hawa wapo kisheria vyama vya wafanyakazi vipo kisheria tokea 2001 na sheria ya *labor* ipo 2005 wanafanya wajibu wao leo wanasitishwa jee, suala hili ni kweli au ni watu tu walikuwa wanalitumia jina hili kwa maslahi yao. Naomba wana watapokuja aweze kulitolea maeleza kwasababu kuenda kule kwa vyama vya wafanyakazi wanapata changa moto nyingi ambayo kwa hivi hivi huwezi kuzipata. Leo wafanyakazi hawapati mikataba ya kazi, wafanyakazi leo katika Taasisi hizo za binafsi wanaondolewa makazini bila ya maslahi yao kupewa. Kwa hivyo vyama vinapokwenda pale tutapata fursa ya kukaa na waajiri kuona namna gani wafanyakazi hawa wanapata haki zao. Lakini pia vilevile tunazilinda vile vyama vya wafanyakazi kwa kuona kwamba wanatetewa kama hawapati utetezi watakuwa hakuna mana kuwepo nahii sheria tuliziona ziwepo kwa ajili ya kuwatetea.

Mhe. Spika, naomba sana atakapokuja anipe maelezo kuona kwamba hicho kitu ni kweli au kimebambikizwa tu.

Mhe. Spika, niende katika suala zima la kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais kwa majukumu yake mbali mbali ikiwemo kukabiliana na maafa nchi yetu mara kwa mara imekuwa ikipata maafa lakini ofisi yake nashukuru sana pamoja na watendaji wake inaweza kusimamia kuona kwamba inatoa faraja.Lakini sasa na serikali pia iwe makini tena kuongeza nguvu kuona kwamba yale yote ambayo yanasababisha maafa tunayafanyia kazi tusingoje mpaka yatokee. Tunaona mambo mbali mbali sasa hivi barabara zinakatika, maji yanajaa watoto wanapotea, vifaa vinapotea, kwa hivyo tusingoje kuzima moto hii itatugharimu sana kila mwaka kwenda kuangalia nani na nani kaangiliwa na maji, kwanza kutengeneza mipango miji na watu kutowaruhusu kujenga sehemu ambazo hazifai.

Mhe. Spika: mimi mchango wangu ni huo naomba sana wizara hii ipewe mafungu yake yote kama ilivyoomba, makadirio yake ya *shilingi bilioni 57* ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, tuna kama dakika saba. Sasa mchangiaji wetu anayefuata labda atumie sehemu ya muda huu halafu tutakuja kumalizia kuchangia jioni. Kwa hivyo, naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kama yupo tayari, kama hupo tayari nimwite Mhe. Machano Othman Said, kama na yeye hayupo tayari basi tuahirishe mpaka hiyo jioni.

Basi nasitisha shughuli za Baraza mpaka saa 11:00 alasiri leo.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea katika kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na sasa naomba nimwite Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Simai Mohammed Said ajitayarishe pamoja na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na uwezo kwa kutufikisha hapa leo. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuwasilisha bajeti ya ofisi yake leo hii asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii ni bajeti kubwa ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo inasimamia utendaji wa serikali, tulitarajia mawaziri wawemo ndani ili wasikie mambo ambayo Waheshimiwa Wajumbe watachangia kupitia wizara mbali mbali. Lakini naomba nianze kwa kuzungumzia Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwenye kitabu hiki kimeelezwa shughuli ambazo Makamu wa Rais amefanya kwa mwaka huu wa fedha 2018 lakini na mipango ya 2018/19, miongoni mwa shughuli ambazo amefanya ni kuwemo la kuisimamia serikali kuonana na mabalozi na kufanya ziara nje na ndani ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, ombi langu watakapokuja kufanya majumuisho ingelikuwa vyema zile ziara za Makamu ambazo amefanya ndani na nje ya nchi ziwe na kiambatanisho tujue moja baada ya moja ili kuona ufanisi na faida ambazo zinapatikana katika ziara hizo. Kwa sababu zaidi ya ziara mia moja na mwaka huu wamesema kama ziara arobaini

pengine ndani ya nchi Tanzania Bara na kwenye mikoa yetu. Kwa hivyo, niliomba hilo liwekwe kesho wakija waje na kiambatanisho cha ziara za Makamu wa Rais.

Lakini baada ya hapo nizungumzie suala la Uratibu wa Serikali. Kama tunavyoelewa kwamba ofisi hii ndio ambayo ni Mratibu wa Shughuli za Serikali, sasa wakati mwengine lugha zinagongana kuhusu uratibu na usimamizi. Kwenye uratibu tungelitaka kujua juhudi za kuratibu shughuli za serikali kwa taasisi nyengine, wananchi wengi wa Zanzibar wanasikitika na kulalamika sana kuhusu suala la maji safi na salama, suala la miundombinu ya barabara zaidi za vijijini pamoja na huduma za vyoo katika maskuli na huduma za afya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa takwimu ya mwaka jana ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira wananchi karibu asilimia sitini, sitini na tano wanapata maji, lakini asilimia thelathini ya maji yanapotea njiani. Ukifanya hesabu hapo inawezekana wananchi wanaopata maji chini ya asilimia hamsini tulitaka kujua mipango madhubuti ya serikali, pamoja na kwamba mwaka jana tuliuliza kiasi gani cha fedha kimetumika kwa miaka kumi katika huduma za maji na tukaelezwa zaidi ya bilioni mia moja sabini zimetumika kwa shughuli za maji kwa miaka kumi. Na pia tuna mradi wa Ras al Khaimah ambao ulikuwepo mwaka jana na mwaka juzi, tulielezwa pia kwamba kulikuwa na visima mia moja na hamsini vya maji kwa Ras al Khaimah, lakini hadi mwaka jana visima ambavyo vilikuwa vinafanya kazi havizidi ishirini na tano. Tujue basi mkakati wa serikali wa kuviimarisha na kuvimaliza vile visima vingine ili kupunguza tatizo la maji kwa Zanzibar. Mimi jimboni kwangu ninavyo visima sita vya Ras al Khaimah na hakuna hata kisima kimoja ambacho kimemaliza na kufanya kazi. Sijui serikali ina mpango gani na visima vile vya Ras al Khaimah. Ukiacha hiyo miradi mingine ya Wachina, ya Wajapan na huu mradi mkubwa tunaoutarajia wa India, huu mradi wa Ras al Khaimah hatma yake ni nini.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu huduma za afya. Afya ni suala muhimu sana kwa wananchi wetu na linaleta matumaini kwa wananchi kama afya inakuwa nzuri. Miezi kama mitatu nyuma iliyopita hadi sasa kisiwa chetu cha Unguja kimeingiliwa na maradhi yanayoitwa homa ya Muungano, homa hii inawasumbua sana wananchi zaidi wa ng'ambo lakini hakuna tamko mpaka sasa la serikali kuhusu homa hii. Wananchi wanazidi kuteketea khofu imekuwa kubwa ukisikia mgonjwa anaumwa homa ya Muungano hata kwenda kumuangalia unapata tabu. Tunaomba serikali kupitia bajeti hii itupe kauli kuhusu hatua na taratibu zote zinazohusu homa hii.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu elimu, bahati nzuri nipo katika Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, tulipata fursa ya kutembelea halmashauri nyingi tu au zote karibu, halmashauri wamegatuliwa elimu lakini bado hawajakabidhiwa yale mambo yote. Lakini kwa taarifa tulizonazo skuli nyingi zina matatizo ya vyoo, wanafunzi ni wengi kuliko vyoo, mahitaji ni makubwa ya vyoo, sasa serikali inajenga maskuli, inasaidiana na waheshimiwa kujenga skuli lakini mradi wa vyoo naona kama umewekwa kichogoni. Kwa hivyo, naomba serikali iweze kuangalia kama itaweza kupata mfadhili wa kutusaidia kujenga vyoo na kupunguza maradhi katika skuli zetu itakuwa ni jambo jema sana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine la barabara za ndani, asubuhi hapa Mhe. Simai Mohammed Said aliulizia kuhusu barabara zake za Tunguu na akaambiwa hazipo katika mpango, ni kweli hazimo lakini kwa sababu kama tutaelekea hivi tutakuja kuilaumu bure Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Tawala za Mikoa hawana fedha za ujenzi wa miundombinu ya barabara kama ilivyokuwa kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Kwa hivyo, hili nafikiri serikali wakae waliangalie waongeze fungu kwa Serikali za Mitaa ili waweze kujenga barabara za ndani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nizungumzie kuhusu maafa ambayo bado ni tatizo na nimefurahi kwamba katika kitabu hiki ofisi imesema kwamba itaendelea kutoa elimu ya maafa kwa waathirika na wananchi mbali mbali. Lakini mimi najiuliza hivi sisi Zanzibar tutakuwa kila mwaka tuna maafa wakati wa mvua za masika. Yaani kila mvua ya masika tunajiandaa na maafa hatuna mpango endelevu wa kusema kwamba hebu tukiwa hivi haya mambo ya maafa zaidi ya mvua za masika yanaondoka. Pengine kama uko mpango huo basi serikali ituarifu kuna hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni kuhusu Tume ya Uchaguzi. Katika kitabu hiki Tume ya Uchaguzi wameombewa fedha bilioni moja milioni mia saba na sabini na nne na laki moja. Mhe. Mwenyekiti, kweli tuna ukomo wa fedha lakini mimi nafikiri ofisi hii wangeliangalia katika fedha za wizara zao watakazopewa waiongezee kidogo Tume ya Uchaguzi fedha na kwa sababu katika mwaka huu wa fedha ambao tutauanza 2018/2019 kwanza tutakuwa na Tume mpya ya Uchaguzi baada ya ile kumaliza muda wake. Hii tume mpya lazima ipate muda wajifunze wapate mafunzo, lakini pia Tume ya Uchaguzi mwaka huu wana zoezi la kuandikisha wapiga kura wapya na hiyo sio kazi ndogo, lakini pia wanatakiwa walihuishe daftari la kudumu la wapiga kura ambalo lipo pamoja na kuwapa elimu, tunalo tatizo la kutokuwa na elimu ya kupiga kura. Kwa hivyo, mimi naomba bahati nzuri Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yupo angalieni kuzihaulisha fedha mafungu mengine angalau hawa wafikie bilioni mbili, hizi bilioni moja nukta saba ni fedha kidogo sana kwa Tume ya Uchaguzi na shughuli zao nyengine.

Mhe. Mwenyekit, naomba pia nizungumzie Tume ya Taifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Hapa nataka kuuliza tu kidogo katika kiambatanisho namba 11 ukurasa wa 61 samahani sijafika huko. Kwanza nataka kuzungumzia Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tiba Kidimni, kituo hiki kinatokezea katika bajeti nafikiri huu mwaka wa tatu au mwaka wa nne, nataka kujua hiki kituo kina gharama gani kwamba na mwaka huu kimetengewa tena milioni mia tano, hizi fedha kwa kituo hiki sio nyingi? Zile za mwaka jana walimaliza zote kituo hakikumalizika kujengwa? Tunataka maelezo kujua kuhusu kituo hiki.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, ukienda katika ukurasa wa 61 kwenye vielelezo kifungu namba 11 kuhusu Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Ukimwi, kifungu cha 24 na 25 hakuna uwazi kwa fedha hizi zote zimeandikwa na tofauti yake mimi siioni. Naomba ninukuu kidogo ambavyo wameandika.

Kifungu cha 61:

"Uratibu wa masuala ya Ukimwi Pemba pesa hizo na Utawala na Uendeshaji Unguja".

Sasa huwezi kujua zipi za Uratibu Pemba na zipi za Utawala Unguja. Lakini pia kuna kifungu chengine cha uendeshaji na usimamizi kuhusu shughuli za mazingira nazo kuna usimamizi na kuna uratibu, sasa nalo hili tulitaka tupate ufumbuzi wake katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka kuzungumza ni kuhusu vikao vya Kero za Muungano, yapo makubaliano na maagizo ya Marais wetu kwamba Kamati za Kero za Muungano zikutane hata kama hakuna jambo jipya angalau wakasalimiane halafu waondoke. Tulitaka kujua kwa mwaka huu wa fedha ambao unamalizika vikao vingapi vya kutatua Kero za Muungano vilikutana na je, katika mwaka wa fedha ujao tumepanga kukutana mara ngapi. Kwa sababu kero zipo na wananchi wanahitaji kero zile zitatuliwe.

Mhe. Mwenyekiti, nije tena katika masuala ya mazingira ukurasa wa 62 fungu dogo hili la 167 kuna mambo mawili kwa pamoja hapa, kuna moja Uratibu wa Mazingira, yaani fungu kubwa linasema Uratibu wa Mazingira wa Mabadiliko ya Tabia Nchi, lakini kuna kifungu kinasema hivi: Mradi wa kukuza uwezo wa kitaifa wa kuhimili athari na mabadiliko ya tabia nchi wametengewa shilingi milioni 33. Halafu kuna mradi wa kuimarisha uhimili wa mabadiliko ya tabia nchi na maisha ya jamii milioni 50. Naomba mtusaidie vifungu hivi viwili tofauti yake ni nini? Maana yake kwa mtu ambaye hayupo kwenye Mazingira anaona kama mambo haya yote yapo kwa pamoja kwa hivyo mkitufafanulia kidogo tutakaa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho ili nisiwanyime wenzangu dakika nizungumzie Baraza letu la Wawakilishi. Baraza la Wawakilishi ni chombo muhimu sana katika maendeleo ya nchi na ni mdomo na sauti yao wananchi, bahati mbaya Baraza hili la Tisa tangu limeingia waheshimiwa wengi hawajapata mafunzo ya uwakilishi. Sisi wenyewe tumeshuhudia Mabunge ya wenzetu kwa sababu Baraza la Wawakilishi lakini ni Bunge sawa katika Jumuiya ya Madola, na sisi ni Bunge tumeshuhudia kupata wageni mbali mbali wa kibunge wanakuja katika Baraza la Wawakilishi kwa ishara kwamba na sisi tunatakiwa tutoke twende tukajifunze katika Mabaraza mengine. Lakini kwa bahati mbaya sana huu ni mwaka wa pili sasa bajeti ya pili tunaipitisha imekuwa hakuna suala hili. Kwa hivyo, naomba kama mwaka huu tumechelewa kuingiza hilo fungu basi mwakani fungu hili liwepo maalum la kuwasaidia Waheshimiwa Wawakilishi kuwajengea uwezo. Na si Wawakilishi tu kuwajengea uwezo pia na watendaji wa Baraza la Wawakilishi, maana yake huwezi kumjengea uwezo Mwakilishi tu kama hukumjengea uwezo na mtendaji wa Baraza la Wawakilishi ambaye anamsaidia Mwakilishi kufanya kazi zake kwa umakini, uelewa na uweledi ili asiweze kufanya mambo ambayo hatakiwi kufanya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi naomba niseme kwamba naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia, lakini naomba yale ambayo tumezungumza tupate ufafanuzi baadae. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Machano Othman Said, sasa namwita Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na baadae atafuata Mhe. Asha Abdalla Mussa. Mhe. Nadir endelea.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana. *Bismillah Rahman Rahiym.* Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi sana isipokuwa ni kuzungumza machache tu, jambo la mwanzo nitaomba nichangie suala la watu wenye ulemavu ambalo ndugu zetu hawa wameumbwa na Mwenyezi Mungu wakiwa na ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, ningeishauri serikali kwanza wakawajengea miundombinu mizuri hawa watu wote wenye ulemavu kuanzia kwenye majengo ya serikalini, barabarani na sehemu nyenginezo ambazo zinawahusu. Kwa sababu nitaweza kutoa mifano baadhi ya sehemu za ofisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hazina miundombinu ya kuweza mtu mwenye ulemavu kupanda juu kufika kwa njia inayotakiwa. Mfano Wizara ya Ardhi atakapotaka kwenda kumuona Mhe. Naibu Waziri au Waziri wa Ardhi hawezi kufika kwa sababu miundombinu ya watu wenye ulemavu hakuna. Lakini vile vile ukienda ofisi ya Mji Mkongwe halikadhalika sehemu ya miundombinu ya watu wenye ulemavu hakuna, ukienda sehemu ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais miundombinu ya watu wenye ulemavu hakuna kuweza kupita na kigari. Hii natoa mifano michache tu ili waweze kufahamu na waweze kuwawekea mazingira mazuri hawa watu wenye ulemavu. Lakini vile vile barabarani tumeona wanapata tabu sana hasa wakati wa kukata barabara na sehemu nyenginezo hakuna sehemu ya kupita na vigari vyao, inamaanisha kwamba labda waje wabebwe au wasaidiwe na watu wengine kuzungushwa katika pande mbili.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ningeomba serikali kwa ujumla ikawatambua watu wote hawa wenye ulemavu hususan wale wazee sana na maskini sana wakaweza hata kuwajengea vijumba vidogo vidogo wakawapunguzia umaskini kwa sababu kufanya kazi kwao ni tabu na kupata ajira ni tabu katika nchi yetu. Vile vile wawapatie vifaa ambavyo vitaweza kuwasaidia waliokuwa hawana miguu wapate miguu ya bandia, mikono ya bandia, mashine za masikio za kusikia,vigari na halikadhalika ambao watu wengine wanavihitaji.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye dawa za kulevya. Suala la dawa za kulevya hivi karibuni nilitembelea jela Kiinua Miguu na sehemu nyenginezo tumekuta watu wanaotumia dawa za kulevya wengi wamo ndani wamefungwa, asilimia tisini na nane ni watumiaji wa dawa za kulevya. Lakini tulikuta kama wawili watatu ambao wanahesabika ni wauzaji unga lakini sio wale wakubwa ni wale wadogo wadogo.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kupitia Wizara yake hawa watu ni vyema wakaenda kutibiwa na sio kufungwa. Kwa sababu hakuna hata mtu mmoja mwanawe anayetaka avute unga, anayetaka akafungwe jela, na si vyema hawa watu kwa sababu wao ni wavutaji wa unga wameshakuwa *chronic* hawawezi kuacha hivi

vitu kwenda kuwafunga kama pale nimewaonea huruma sana. Wamo ndugu zetu wa kike lakini pia wamo ndugu zetu wa kiume, tungeomba serikali ikafanya utafiti wao na utaratibu wakaweza kuwatibu hawa watu waliokamatwa na dawa za kulevya na sio badala yake kuwafunga. Kuwafunga ni kuwazidishia mashaka, kuwazidishia kupata tabu na ukiangalia hali wakishakutoka itaendelea ile ile. Ni vyema kama wanavyoendelea wazidi kupiga vita dawa za kulevya kwa njia ya bandarini, *airport* na zile
bandari bubu waweze kuwakamata waweke sheria kali kama tunavyosema siku zote sheria za kuwaua, sheria za kuwafunga maisha na nyenginezo ndio masuala ya dawa za kulevya yataondoka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kwenye suala la Ofisi ya Baraza la Wawakilishi. Mhe.Mwenyekiti, kwanza nakwenda kwenye suala la bajeti ya safari hii ni 20,354,000,000/= ndio iliyokubalika, lakini mwaka wa nyuma 2017/2018 ukiangalia ni bilioni 18 na kidogo wakati ule fedha ilikuwa *rate* ni 2,130/=, dola lakini safari hii dola ni 2,300/=. Zile fedha zilizoongezeka kwa safari hii ambazo ni milioni 500 kwenye Baraza la Wawakilishi ni sawa sawa na kuwa kumeongezwa fedha kidogo sana kwa mwaka mzima.

Hii itasababisha baadhi ya kazi za uongozi wa Baraza la Wawakilishi kukwama mfano hususan Baraza la Wawakilishi sasa hivi linavuja, kuna sehemu zinataka kutengenezwa, kuna suala la *echo,* kuna suala la *maintenance* mambo makubwa makubwa, kuna suala la safari za wajumbe kwenda kufundishwa mambo tofauti kwenye mabunge kusoma hawatoweza kupata nafasi hizi kwa sababu ya fedha ni ndogo. Tungeomba Serikali kwa ujumla wakaangalia kwamba Baraza la Wawakilishi ni sehemu kubwa na ndio inayoisaidia Serikali katika kupitisha bajeti, katika kukusanya mapato na mambo yote.
Mhe. Spika, ni vyema waliangalie Baraza la Wawakilishi kuweza kuzidisha zaidi na hata kuhitaji fedha basi waweze kuwapa ili mambo yakaenda kupitia Baraza la Wawakilishi, fedha hii siwezi kusema ni ndogo lakini kwa hali ya sasa na dola ilivyopanda ni ndogo sana. Ukipiga hesabu *difference* itakuja ni milioni mia mbili tu kwa mujibu wa *rate* ya dola ambazo zimeongezeka ni milioni mia tano, lakini ukija kwa *rate* ya sasa hivi ya dola na mwaka uliopita inamaanisha watakuwa wamepata milioni mia mbili. Leo Mhe. Spika anasafiri, Mhe. Naibu Spika anasafiri, na mtu mmoja au watu wawili wanaweka *limitation* ambayo hicho kitu hakiwezekani, hadhi ya Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika, na viongozi wa Baraza la Wawakilishi ni kubwa.
Mhe. Naibu Spika wa Bunge anasafiri na watu 12, mimi binafsi nimeshasafiri Bunge la Tanzania wanasafiri na watu 15 kwenda juu ile ndio hadhi yake sio kwamba kuna watu wanataka kufanya ubadhirifu, kuna watu wapo tayari kupanda *economy* kwenye ndege lakini kwenda kupata elimu. Hii yote Baraza la Wawakilishi inajitahidi kufanya *economy* ya kuweza ku-*save* pesa na hii wameweza. Lakini kutonana na fedha tulizonazo waheshimiwa wanapata tabu, kuna waheshimiwa humu ndani hawajapata hata elimu, hawajapata mafunzo ya kuweza kufahamu kazi yao nini, wapo waheshimiwa humu ndani wanafahamu wao kama ni Serikali, leo kuna jambo la ku-*support* wajumbe wenzao nyuma lakini wanakwenda ku-*support* Serikali kwa sababu mafunzo yale hasa ya wawakilishi hawajapewa. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sana hizi fedha tuje tutiliwe Baraza la Wawakilishi tuongezewe.

Nakwenda kuzungumzia suala la Muungano kuna baadhi ya viongozi kwenye taasisi kubwa kubwa ya Jamhuri ya Muungano wamekuwa wakitoa maneno ambayo hayapendezi kwa upande wa Zanzibar, haya tumeyaona sana kuna viongozi wakishakukaa wanazungumza Zanzibar ndio sehemu kubwa ya kupitisha magendo, wizi wa sukari, hatuna elimu tunakwepa kodi Serikali haina uangalifu. Mimi nataka niwaambie Mzee Julius Kambarage Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume wazee wetu walipoungana kuleta Muungano walijua kwamba hizi nchi zote mbili zina maslahi na zina mambo mazuri na zitaunga udugu mzuri, tukiangalia kuanzia Mhe. Mwalimu Nyerere mwenyewe, Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Mhe. Benjamin William Mkapa, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete na Mhe. John Pombe Magufuli wanaheshimu Muungano, wanaheshimiana na viongozi wa upande wa Zanzibar.

Lakini nikizungumza baadhi ya Waheshimia ambao *level* yao ndogo ya chini nikimaanisha hivyo kwenda Waziri, Naibu Waziri na Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakitoa kauli si nzuri kwa upande wa Zanzibar kuidhalilisha, kuitukana na kutoa maneno ambayo hayana maana. Mimi niwaambie Zanzibar ni nchi ambayo inajiheshimu, ina Serikali makini, ina Wawakilishi makini, hapa tuna Serikali yetu, tuna Bunge letu tunajua nini tunafanya. Atakapoinuka mtu mmoja au wanne ambao nidhamu zao sio nzuri kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatutofahamu, niwaambie tu sisi Wazanzibari tuna vyama vingi, siku ya vyama kila mmoja anakuwa mbabe kwa mujibu wa chama chake, lakini tukimaliza siasa sisi sote Wazanzibari ni ndugu hatubaguani huyu ni mtu wa Unguja, hatubaguani mtu wa Pemba, sisi sote ni ndugu.

Mtu yeyote ambaye atatuletea masuala ya kutugombanisha kama yale ya kutuita wezi au tuna njaa, kwanza Zanzibar sio maskini, Tanzania Bara ndio maskini ina watu milioni 48, sisi tuko watu milioni moja na laki nane. Ukifanya tathmini yetu watu maskini Zanzibar ambao wanapata kula yao hatufiki milioni moja na laki tano, Bara si chini ya milioni arubaini na tano ni watu maskini hata sukari hawaipati kama wanavyosema wao.

Lakini tukija kwenye akili mtu mmoja wa Zanzibar ana akili kuliko familia ya yule aliyesema hatuna akili wote katika familia yake. Mhe. Mwenyekiti, nazungumza haya kwa sababu tumeona kuna mawaziri, kuna baadhi ya wajumbe ambao wakubwa wakubwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanatukana na maana yake kwamba wanamtukana Dkt. Ali Mohamed Shein, wanamtukana Makamu wa Pili, wanatukana Waheshimiwa Mawaziri, wanatukana Wawakilishi na wananchi kwa jumla wa Zanzibar. Ni vyema wakaweka heshima zao sawa sawa Zanzibar tuna nidhamu zetu, Zanzibar tunajua nini tunafanya na hata kama tumekwepa hatujakwepa wao wasituletee ushahidi, tumeona Bara kuna vichwa vya treni, kuna magari zaidi ya 200, kuna pembe za ndovu zinakamatwa nchi za Kiarabu, dhahabu zimekamatwa Ulaya, kule ndio kunaongoza kwa wizi kuliko Zanzibar. Sasa ni vyema akaona na kule Tanzania Bara asiingilie mambo ya Unguja, mambo ya Unguja Serikali ya Unguja ipo, sisi wawakilishi tunaona na tunaheshimiana, ni vyema akazungumza vitu anavyovijua, ni vyema akaenda kuwauliza wazee wake, babu yake na mama yake akafundishwa historia ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza hivi kwa sababu tunataka tujengeane heshima tumeona sasa hivi tunatukanwa sana na tumeshachoka kutukanwa, haiwezekani viongozi wa juu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanaheshimu Muungano lakini wale viongozi wenye *statu*s ambayo ya *middle class* wakawa wanatukana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo huku tuna Rais, tuna Makamu wa Rais, tuna Mawaziri na Wawakilishi ambao tunajiheshimu na tunajua kazi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipojiunga na Mhe. Abeid Amani Karume alijua kwamba Zanzibar ni sehemu nzuri ya kujiunga na Zanzibar wakati huo inajiweza imeshasaidia sana Tanzania Bara, hadi hivi leo hata huo utalii wa Tanzania Bara bila ya Zanzibar hauendi. Ushirikiano wetu tunataka ukue na sio uharibiwe, kama wanaona hivyo viongozi wanaona wanazidi kuachilia mambo yanaharibika tunatukanana itakuwa haipendezi. Ningeomba viongozi wa namna hii kwanza wakatafute wale wazee waliojiunga na Muungano wakapata elimu ili wafahamu nini maana ya Muungano na sio kukaa kubwabwaja. Inasikitisha sana kuona Mwakilishi wa CCM anatukana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar halafu Waheshimiwa Wabunge au Waheshimiwa wengine kwa mfano wanapiga makofi kisa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatukanwa na badala yake watu wa upande wa pili nikimaanisha upinzani wakawa wao hawa-*support*, inasikitisha sana.

Nimpongeze Mhe. Jamal Kassim Ali Mbunge wetu, Mhe. Saada Mkuya, akina Mhe. Jaku Hashim Ayoub na wengineo, vile vile waheshimiwa wa upinzani ambao wanai-*support* Zanzibar kuijengea heshima yake. Mimi nawapongeza kwa sababu wanafanya uzalendo siwezi kumpongeza mtu CCM ambaye anatukana CCM ya Zanzibar kabisa, tumeona wanapiga makofi wengine wakati ikitukanwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende jengine nimuombe Mhe. MakamU wa Pili wa Rais kuna kipindi cha nyuma na *document* hizi ambazo …

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika mbili.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana itatosha kuna ndugu yetu huyu anaitwa Anwar Abdalla Juma nimepokea *document* zake na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aliwahi kwenda kutembelea maeneo ya Mlandege, *document* hizi hapa ninayo mpaka *video* na Mheshimiwa wangu Makamu wa Pili wa Rais analifahamu. Ningeomba itumike busara ya yule mtu kuweza kurejeshewa sehemu yake, yeye niseme alikwenda kuzuia watu wasiweze kuweka makontena mbele ya jengo lake, ana nyumba nyuma ya ghorofa mbili aliamua kuivunja kujenga ghorofa sita matokeo yake akavunja, akajenga *foundation* ana vibali ana kila kitu kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais analijua hili suala, Mhe. Rashid huyo hapo, Waziri wa Uvuvi analijua, Mhe. Haji Omar Kheri analijua hili suala lina uhakika na ni haki yake leo kenda kuvunjiwa *foundation* yake ya dola laki mbili ya ghorofa sita mwaka wa tatu huu kazuiliwa. Ningemuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yule jamaa ni mnyonge hawezi kukufikia kila wakati kukuona kama baadhi ya Wajumbe wengine anapata tabu. Hawezi kumuona Mhe. Rais, wala hawezi kukuona wewe kwa sababu ni wakubwa tunaona sana achukuliwe mambo ambayo ya kibinaadam aweze kuendelea na mjengo wake. Na *document* hizi hapa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nitakupatia kwa sababu pale kuna tatizo limetokezea na sio kwa upande wako wewe, bali kwa baadhi ya viongozi wamo ndani ya Serikali wamemuonea na wamechukua eneo lake mpaka leo wameruhusu watu wamejenga milango kinyume na sheria wakati ile ni sehemu ya *Buffer Zone.*

Ningeiomba Serikali iangalie haki tusitie watu katika matatizo mimi kaniletea nimeridhika nazo na ndio maana nimekuja kuongea humu kwa sababu ana ushahidi wa asilimia mia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi badala ya hayo yote nimpongeze Mhe. Makamo wa Rais na Wizara yake nzima kwa kazi zake zote anazozifanya tunaona na ndio maana wakati huu sijataka kuongea sana kwa sababu anafanya kazi ya ziada. Mfuko wa jimbo tumeupata kabla ya wakati tumeweza kufanya mambo yetu juu ya kwamba anahangaika huku na kule, tunamtakia kheri afanye kazi zake vizuri ndio maana safari hii hata nguvu ya kuchangia hatuna kwa sababu anajitahidi kwenye kazi zake.
Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja asilimia mia moja ya ripoti hii, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kwa uchangiaji wako sasa namwita Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajitayarishe.
Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa fursa hii kuweza kuchangia machache katika hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2018/2019.
Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Waziri wake Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote wa ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais.
Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba hii ambayo imeonesha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/2018, lakini pia mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa upande wangu mimi nitachangia machache. Kwanza kabisa niwapongeze Waratibu wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuratibu shughuli zote za Serikali ambazo zipo katika ofisi hiyo.
Lakini pili, niwapongeze Idara ya Maafa kwa kufanya kazi nzuri na kuhakikisha kwamba wanatoa elimu katika kamati zote zilizopo ndani ya Mikoa, pamoja na Wilaya na Shehia. Idara hii ya Maafa ina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba inafanyakazi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 9 na wa 10 katika kitabu hiki cha hotuba hii kimeelezea kwamba maeneo ambayo kwa mwaka huu yametokea maafa makubwa kutokana na mvua zilizonyesha pamoja na upepo ambao ulitokezea. Lakini kwa masikitiko makubwa kuna baadhi ya maeneo ambayo yalitokea maafa makubwa sana na maafa haya yamesababishwa na upepo ambao ulitokea tarehe 4 Machi, 2018 maeneo yaliyoathirika ni maeneo ya Kilombero, Pangeni, Kiwengwa, Upenja na Mgambo.
Lakini cha kusikitisha kwamba hadi sasa wananchi hawa waliopata maafa waliwahi kutembelewa baadhi yao tu, lakini mpaka sasa wananchi hawa bado wanalaumu Serikali kwamba kwa nini wao wamepata maafa mwanzo hawakwenda kupatiwa misaada, waliopata maafa mwisho ndio wamekwenda kupatiwa misaada hiyo. Naomba sana Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wahakikishe kwamba watu hawa nao waweze kupata haki yao, lakini pia naiomba Idara hii ifuatilie zile kamati ambazo zimeundwa katika mikoa yetu ili kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zao ipasavyo.
Mhe. Mwenyekiti, lakini pia katika ukurasa huo wa tisa kuna kifungu cha 31.0 kuna kukabiliana na maradhi mbali mbali ambayo yanasababishwa na wanyama kwenye kwa binaadam. Mhe. Mwenyekiti, kuna wanyama hawa kama mbwa vichaa tarehe 6/5/2018 katika Shehia ya Kilombero kuna watoto watatu na mtu mzima mmoja ambao wametafunwa na mbwa kichaa. Lakini pia niishukuru sana Serikali kwa utaratibu ambao wameandaa sasa kwa kuanzisha timu ya uratibu wa afya, ambayo nadhani timu hii inaweza kuratibu shughuli nyingi ambazo zinaweza kusababisha afya ambayo hatarishi

kwa binaadam. Naomba sana Serikali kupitia Wizara ya Afya iweke kinga maalum ambayo ina unafuu kwa wananchi watakaoweza kupata maafa haya.

Mhe. Mwenyekiti, nije suala la miradi katika uratibu wa miradi ya maendeleo kupitia mradi wa *TASAF*. Niipongeze sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuratibu masuala mazima ya *TASAF*, naamini kwamba mpaka huu mradi ukimaliza utahakikisha kwamba wananchi wetu ambao wapo katika kaya maskini basi wameimarika kaya zao. Lakini vile vile imewezesha wananchi hawa kufahamu na kutafuta njia ya kuweza kujipatia kipato na kuhakikisha kwamba kaya hizi zinaimarika.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye miradi ya maendeleo ya Mfuko wa Jimbo (*CDF).* Niipongeze sana Serikali hii kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini pia niwapongeze sana wale waratibu wanaofuatilia miradi hii kwa kutoa muongozo katika majimbo yetu, lakini pia kuweza kutuhamasisha na kutuhimiza tutekeleze wajibu kama vile sheria zinavyosema. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa na ngumu, kwa hivyo ningependekeza kwamba changamoto ambazo zinajitokeza katika kupitia miradi hii, basi ningeomba sana Mfuko huu wa Jimbo badala ya kuwa milioni ishirini, basi ungeongezwa zikawa milioni ishirini na tano.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika program hii katika ukurasa wa 20 mpaka 21 kuna Uratibu wa Ujenzi wa Nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo inajengwa Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imeonesha kwamba hapa zilitengwa jumla ya shilingi milioni mia tano kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hiyo. Lakini pia fedha zilizopatikana katika mwaka huo zilikuwa shilingi 13,880,000/=. Nilitaka kufahamu Waziri atakapokuja kutoa majumuisho hizi shilingi 13,880,000/= zimetumika kwenye hatua ipi ambayo imefikia hivi sasa.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba niungane mkono na Wajumbe wa Kamati hiyo ambayo inasimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mapendekezo yao ambayo wamependekeza. Niseme kwamba naamini watendaji wote watashirikiana pamoja na Waziri husika wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutekeleza bajeti ya mwaka 2018/2019 kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hotuba hii nilivyoisoma na nimeitazama vizuri nimeipitia, basi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Asha Abdalla Mussa, sasa nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukrani za dhati sana kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lakini na Mawaziri wake wote pamoja na watendaji katika uwasilishaji wa ripoti hii. Lakini vile vile niwapongeze Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na hususan nimpongeze kwa uwasilishaji wake mwema, lakini niwapongeze wajumbe wote ambao wametangulia katika kuichangia ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ripoti hii sina wasi wasi nayo naiunga mkono asilimia mia kwa mia, ripoti ni nzuri, kazi imefanywa vizuri, lakini kwa kuwa na mimi ni mjumbe na mimetumwa na wananchi kuwawakilisha, ningependa nichangie machache yenye nia ya kujenga ripoti hii muhimu ya bajeti ya wizara au ofisi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, tume hii ina kazi kubwa sana na tuipongeze kwa kazi zake ambazo inafanya pamoja na changamoto mbali mbali ambazo inakabiliana nazo. Changamoto zipo nyingi zikiwemo za upotevu wa vielelezo vya kesi za madawa, kuna changamoto vile vile za kukosekana takwimu halisi katika idadi ya vijana wanaoingia katika *Sober House,* lakini kuna changamoto nyengine mbali mbali.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ili kuifanya tume hii kuweza kufanya kazi zake vizuri na hususan katika kuweza kudhibiti janga hili la dawa za kulevya ambazo zinaathiri nguvu kazi za vijana wetu, basi tuipe mkazo sana tume hii katika bajeti yake ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa umakini zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa 26 wa bajeti hii tume imezungumzia kuzipatia ruzuku *Sober House* 9. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri sana lakini la kushangaza katika changamoto inazungumzia kuna kukosekana kwa takwimu halisi ya idadi ya vijana wanaoingia na kutoka katika *Sober House.* Sasa huku tunazipa ruzuku lakini idadi ya vijana wanaoingia na kutoka hatuijui, hii ni changamoto hatuwezi kutia ruzuku na kuweza kupima mafanikio vizuri katika mazingira namna hii. Lazima tume hii iwe makini sana ili hizi pesa ambazo tunazipitisha hapa basi ziweze kufanya ile kazi ambayo tunakusudia, na sio kuweza kuwatajirisha wale ambao wanamiliki nyumba hizi ambazo lengo lake ni kuweza kuwapa nafuu vijana wetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, tume vile vile imewadhamini vijana hawa wa *Sober House* katika mafunzo ya ujasiriamali, kuna vijana wamepelekwa kuchukua mafunzo ya ukulima wa uyoga Dar es Salaam na kuna vijana ambao wamepelekwa kuweza kujifunza mafunzo ya ufugaji nyuki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika hili nipendekeze tu kwa sababu hawa vijana ambao wapo *Sober House* nyingi zipo katika maeneo ya mjini, sasa tuweze kutazama vijana hawa wanatokea katika mazingira gani, tunaweza tukawapa mafunzo ya ujasiriamali lakini yakawashinda kutumia, unamfundisha ukulima wa uyoga huyo mtu katoka Kikwajuni au Miembeni, sasa ukulima huo wa uyoga sijui atakwenda kuutumia wapi. Au katoka Shangani halafu unakwenda kumfundisha mafunzo ya ufugaji nyuki, sasa tuweze kutazama hawa tunaowapa mafunzo katika *Sober House* wanatokea wapi na hizi kazi tunazowafundisha kama ni kweli wanaweza kuzitumia vizuri. Kwa sababu iwe mtu huyu anatokea Charawe unaweza ukamfundisha mafunzo ya kufuga nyuki, sasa hili tulitazame sana tusije tukawa tunatoa mafunzo lakini kumbe mafunzo yale sawa sawa na kumwaga gunia la sukari katika bahari.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Tume ya Uchaguzi. Mhe. Mwenyekiti, hii ni tume muhimu sana tuipongeze kwa kazi zake, uongozi mzima tunaupongeza kwa sababu kujigamba kwetu sote humu basi ni Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na tumpongeze sana Mhe. Mwenyekiti Mstaafu.

Mhe. Mwenyekiti, katika Tume ya Uchaguzi kuna changamoto mbali mbali, kuna changamoto ya upungufu wa pahala na majengo ya ofisi, wana changamoto wenzetu ya

vyombo vya usafiri, wana changamoto vile vile ya upungufu wa wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, tume hii inapaswa kuangaliwa kwa umakini sana ili kuweza kuona kwamba changamoto hizi zinaondoka. Kwa sababu ufanisi wa Tume ya Uchaguzi ndio unaoweza kuifanya serikali kuwa tulivu, bila ya Tume ya Uchaguzi kuwa ufanisi na hususan vitendea kazi pamoja na maslahi yao vizuri basi hali ya nchi hii inawezekana isiwe tulivu kwa sababu uchaguzi ndio kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Tume ya Uchaguzi na nimuombe sana Mhe. Waziri atakapokuja katika malengo ya Tume ya Uchaguzi ya mwaka 2017/18 ukurasa wa 46 nimuombe sana ayatazame yalikuwa katika kifungu (a) mpaka (f) hayaendani na yale mambo ambayo yalitekelezwa katika kitabu chetu cha bajeti. Sisi hapa tunazungumzia kule tumewapitishia pesa kwa ajili ya malengo haya ambayo watayafanya, sasa katika shughuli ambazo wametekeleza ni kinyume kabisa na yale malengo ambayo tuliwapitishia fedha. Sasa malengo ambayo yalipitishwa mwaka jana ndio ambayo yamepangwa kwa ajili ya bajeti hii na sisi tunataka tuwapitishie fedha. Mimi ningeomba sana malengo au kazi ambazo tumepangiwa, ndio kazi ambazo sisi tunataka kuona tathmini yake sasa katika bajeti hii, ili kuweza kupitisha fedha kwa ajili ya kazi nyengine kwa mwaka huu wa bajeti.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutoa ufafanuzi turidhike juu ya malengo yaliyopangiwa mwaka jana lakini utekelezaji wake ambao haumo katika kitabu hichi cha bajeti, hii ndio itatufanya tuwe na nguvu ya kuweza kupitisha bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka katika Tume ya Uchaguzi sasa nimalizie na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa. Mhe. Mwenyekiti, kamisheni hii ina kazi kubwa, kuna Programu ya Maafa, Zanzibar kama nchi nyengine inakabiliwa na maafa mbali mbali na wenzangu wametangulia kusema na kuna karibu zaidi ya milioni 800 zimetengwa kwa ajili ya programu hii ya maafa, sio pesa nyingi lakini ni pesa za wavuja jasho.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majukumu yake na tunaipongeza sana tume hii, au programu ndani ya kamisheni hii kwa kazi zake. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nije katika kuliona hasa hili neno maafa tafsiri yake. Mhe. Mwenyekiti, nimetazama kamusi mbali mbali, nimetazama kamusi ya Kiswahili kwa Kiingereza, Kiingereza kwa Kiswahili. Lakini nimeitazama mpaka kamusi ya Kitaliana kwa sababu hili neno kwa Kiswahili tunaita maafa, kwa Kiingereza tunaita *disaster,* kumbe *disaster* ni neno la Kireno, ni neno la Kitaliana ambalo linasomeka kama *disastro,* sasa kwa mustakabali wote huo maana yake maafa ni matukio yanayosababisha madhara katika jamii.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa katika visiwa vyetu tuna maradhi haya tunaita homa ya Muungano. Hii homa maana yake mimi naizungumzia kama ni tukio ambalo linasababisha madhara katika jamii yetu ya watu wa Zanzibar na kuna madhara ya aina mbili, kuna madhara ya kiafya lakini vile vile kuna madhara ya kiuchumi. Sasa ningependa Mhe. Waziri atakapokuja atwambie kwamba homa hii ni maafa au si maafa, kwa sababu katika jimbo langu ukihesabu nyumba kumi, basi nyumba saba zimeingiwa na maradhi hayo, na haya ni maradhi mageni kwa hiyo mimi naita maafa. Lakini waziri

atakapokuja anaweza kusema kama si maafa ni kitu chengine basi wananchi angalau wapate elimu juu ya hilo kama ni maafa au si maafa.

Lakini tukitazama katika ukurasa wa 7 huduma za afya imeelezwa humu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kupambana na maradhi mbali mbali imeweka mpango maalum wa chanjo mbali mbali. Ni suala zuri lakini hadi leo hali iko namna hiyo juu ya madhara haya ambayo mimi nayaita *disaster*. Kwa hiyo, ningependa sana Mhe. Waziri atakapokuja aje na mpango utakaoonesha tafiti juu ya maafa haya ili wananchi wawe na imani na sisi kwa sababu hali za kiuchumi kwa kweli hivi sasa kwa wananchi wetu na hususan katika jimbo langu la Magomeni sio nzuri, sio shwari na nina imani vile vile katika majimbo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie na suala la tafiti. Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii inaratibu tafiti mbali mbali, hapa tumeona kwamba imepokea maombi mbali mbali na imetoa vibali karibu mia moja na thelatini ni moja (131), hii inaingizia fedha serikali. Lakini suala la tafiti sio la leo, suala zima la kujiuliza kwamba tafiti zinazofanywa katika nchi hii zinaleta tija gani katika nyanja mbali mbali za kiuchumi, kijamii na za kimaendeleo kwa sababu tafiti ni nyingi, lakini kila tukikaa tunaona kwamba zile tafiti kama vile hazitumiki vizuri. Kwa sababu wenzetu katika nchi mbali mbali wanatenga asilimia kubwa sana katika kufanya tafiti ili kuweza kupiga hatua za kimaendeleo. Suala hili Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi analisisitiza sana na ndio maana katika wizara zetu mbali mbali basi kuna vitengo mbali mbali vinavyoshughulikia tafiti. Sasa tuweze kujiuliza tu kwamba tafiti zetu hizi zinaleta manufaa na tija gani katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, mimi kwanza nipongeze hotuba hii kwa mara nyengine na naiunga mkono kwa asilimia moja moja na niwaombe wajumbe wenzangu tuichambue, tuipitishe ili wenzetu waweze kutekeleza majukumu ambayo wamejipangia. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Rashid Makame Shamsi, sasa namwita Mhe. Suleiman Makame Ali akifuatiwa na Mhe Salha Mohamed Mwinjuma.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kabla ya kuchangia kwanza niwapongeze sana watendaji wote waliokaa na kuichambua bajeti hii ili kuhakikisha kwamba tunapata maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze pia watendaji wote wa ofisi hii akiwemo mtendaji mkuu husika Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ndio kiongozi kwenye ofisi hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 44. Mhe. Mwenyekiti, wamesema kwamba kuweka mazingira mazuri ya majengo na kumbi za mikutano pamoja na kutoa huduma za Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba sana na ule

ukumbi wa Pemba hapa usisahauliwe. Mhe. Mwenyekiti, ipo haja ya kuufanyia marekebisho ukumbi ule wa Pemba na ikiwezekana pia kuweza kufanyika mikutano kule. Mhe. Mwenyekiti, hili pia litasaidia kwamba sisi Wawakilishi tunaotoka Pemba kuweza kubakia kule majimboni mwetu kwa baadhi *time* nyengine ili kuweza kufanya shughuli nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, hilo litakuwa ni jambo zuri sana na pia naomba hilo kwa sababu nilipata kuambiwa kwamba sio pesa nyingi zinazohitajika ni kama shilingi milioni mia nne. Kwa hivyo, naiomba sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais waangalie ukumbi ule wa Baraza la Wawakilishi Pemba kufanya marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende moja kwa moja ukurasa 38, Mhe. Mwenyekiti ukurasa 38 umesema kwamba kuhusu masuala ya mazingira, Mhe. Mwenyekiti mazingira ni uhai Mhe. Mwenyekiti bila ya mazingira kusema la ukweli ni mtihani, lakini Mhe. Mwenyekiti wametenga hapa jumla ya shilingi milioni mia nne na tisini na tatu, Mhe. Mwenyekiti kama utakumbuka hapo zamani kulikuwa na zile sinema zikioneshwa vijiji kwa vijiji, shehia kwa shehia, lakini Mhe. Mwenyekiti katika mpango wao wamesema kwamba watatoa taaluma kwa wananchi ili kuhakikisha kwamba vipi wanakabiliana na masuala ya mazingira. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo zuri sana kwa sababu mazingira bila ya mazingira hapa pangelikuwa hapakaliki.

Mhe. Mwenyekiti, mazingira kuyatunza ni wajibu wetu lakini mimi nashauri sana kwamba pia wawashirikishe na ikapendeza zaidi kuchukuwa vile vikundi vya sanaa vya akina kashara na wenzake ili kupita kwenye shehia kuelimisha masuala haya ya mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye ukurasa 37, Mhe. Mwenyekiti usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu, niwapongeze sana Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa maelezo yao kwamba wametowa vifaa vingi, watu wenye ulemavu, lakini Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wengi wameshasema hapa kwamba kuna baadhi ya majengo sio rafiki sana kwa watu wenye ulemavu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hata mlemavu ukimpa kigari kuna miundo mbinu hususan ya barabara baadhi ya sehemu nyengine zina mashimbo, hasa Mhe. Mwenyekiti hata kile kigari mlemavu unampa tabu, kwa sababu itakua hawezi kwenda ataendeshaje atasukumwaje, mashimo mengine makubwa barabarani kwa hivyo naliomba sana na naiomba sana wizara kwamba wahakikishe kwenye kutowa vifaa, lakini wahakikishe na miundo mimbu ya barabara iko vizuri ili kwamba hawa wenzetu, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti kila mtu ni mlemavu mtarajiwa, hasa ukimpa kigari lakini sasa barabara siku nyengine itakuwa haiendeki baadhi ya barabara nyengine Mhe. Mwenyekiti tutawajengea mazingira magumu.

Mhe. Mwenyekiti nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye shughuli za SMZ, ahadi za viongozi Mhe. Mwenyekiti hapa ofisi imesema kwamba utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Mhe. Mwenyekiti hizi ahadi za Viongozi baadhi ya taimu nyengine kusema za ukweli zinasahaulia. Mhe. Mwenyekiti

jimboni kwangu kuna kijiji kinaitwa Michungwani Rais aliyepita wa Awamu ya Sita Mhe. Abeid Amani Karume aliahidi mambo manne pale, aliwahidi umeme, akaahidi maji, akaahidi barabara na akajengea msikiti mambo matatu yamefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la barabara kilo mita 3.2 limesahaulika kabisa, ambao kwamba ni kilio kimefikia mie nikenda kule Mhe. Mwenyekiti niukumbusho, kwa hiyo naomba sana hapa kwamba hizi ahadi za viongozi Mhe. Mwenyekiti zisisahauliwe mpaka ikapita tena miaka ishirini, thelathini, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, Rais aliyeondoka ni wa Chama cha Mapinduzi na huyu Rais tuliyenaye ni wa Chama cha Mapinduzi na vile vile Dkt. Amani alisema kwamba mimi naondoka ahadi zitakuja kutekelezwa na Rais anayefuatwa hiyo naomba sana kwamba hizo ahadi za viongozi hususan wa kitaifa zisisahauliwe, kwa sababu itakuja kwenda tena ahadi ziwe nyingi wananchi hatufahamu huko majimboni.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana sana kwamba zile ahadi zile za viongozi pia zilizopita basi ziweze kutekelezwa Mhe. Mwenyekiti nikitoka hapo niende moja kwa moja niende kwenye suala la bahari bubu, Mhe. Mwenyekiti katika ripoti ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati alisema kwamba, Mkoa wa Kusini Pemba una kama bandari bubu 100 na Mhe. Mwenyekiti mimi najiuliza hizi bandari bubu, anayehusika na hizi bandari bubu ni nani?

Mhe. Mwenyekiti, huko kwenye vijiji kuna shehia, kuna viongozi kama Mhe. Mwenyekiti tuko tayari kuhakikisha kwamba hizi bandari bubu tunazikomesha basi paundwe kamati tuhakikishe kila sheha kaunda kamati ya kukomesha bandari bubu, Mhe. Mwenyekiti hakuna lisowezekana, kwa sababu bandari bubu zipo kwenye watu nam Mhe. Mwenyekiti tunapata aibu kubwa kuambiwa kwamba sisi Zanzibar ndio kitovu cha masuala ya madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, yanatokea huku huku kwenye bandari bubu. Kwa hiyo, mimi naomba sana kwamba wananchi pamoja na viongozi walioko huku ngazi za chini za shehia wahakikishe kushirikiana kwamba bandari bubu hizi wanazikomesha. Mhe. Mwenyekiti, tukishirikiana hilo linawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye kitengo cha kukabiliana na maafa. Waswahili wanasema kwamba “Kimbia ubwe kabla hujaona ng’ombe”. Kitengo hiki cha kukabiliana na maafa kinakabiliana na maafa na alisema kwamba kuna sehemu nyingi walitembelea ili kuhakikisha wanakabiliana na hayo maafa.

Mhe. Mwenyekiti, kama utakumbuka kipindi kilichopita cha ripoti za kamati nililizungumzia suala la Uwanja wa Ndege. Pale Uwanja wa Ndege hapana maji, bwawa lipo, umeme hapana. Sasa ile kimbia ubwe kabla hujaona ng’ombe ndiyo hii, kama haya maafa tunataka kuyadhibiti pale Uwanja wa Ndege tatizo lipo kubwa sana, maji hapana, Mwenyezi Mungu atunusuru mbali, ikija ikitokezea ndege kuripuka hayo ndio maafa yenyewe. Naomba sana kitengo hichi cha kukabiliana na maafa pia waende Uwanja wa Ndege.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha Mhe. Rais ameshatoa ahadi sisi Wajumbe wa Kamati tulikwenda, lakini bado suala hili halijatekelezwa. Samahani Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais alitoa amri kwa sababu Mhe. Rais anachokisema huwa ni amri kwamba fanyeni hivi. Sasa leo kusema la ukweli amri ya Rais inapuuzwa itakubalika ya nani, sasa likija likitokea tatizo pale tena tuje kukamatana mashati, haya ndio maafa yenyewe.

Naomba sana Kitengo hichi cha Kukabiliana na Maafa waende pale *Airport* wahakikishe kwamba suala lile la upatikanaji wa maji ya uhakika pale kwa sababu pana roho za binaadam, kama leo itakuwa mtu anadharau, mimi niseme huyo hafai hata kuwepo kwenye hiyo taasisi kwa sababu hajali zile roho za wenzake.

Leo umeme wa shilingi milioni mbili panapopatikana bilioni ya mapesa kweli inashindikana Mhe. Mwenyekiti. Aah! mambo mengine kusema la ukweli yanasikitisha. Naomba sana Kitengo hichi cha Kukabiliana na Maafa ili kama tunakubaliana na maafa basi waweze kufika Uwanja wa Ndege pale wakahakikishe kwamba suala hili la maafa yasije yakatokezea, yakitokezea yale ya Mwenyezi Mungu mwenyewe yaliyokuwa hayazuiliki basi, lakini hili tunalo kwenye mikono yetu tunaliweza. Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Suleiman Makame Ali. Waheshimiwa Wajumbe, naomba mpunguze minong'ono yenu imekuwa mikubwa na ukumbi wetu mnajua una tatizo la *echo,* kwa hivyo tafadhalini mpunguze minong'ono ili Mjumbe anayechangia asikilikane katika vyombo vinavyohusika.

Baada ya hapo namwita Mhe. Simai Mohammed Said na baadaye atafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said, ahsante karibu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi mimi, lakini pia nichukue fursa hii pia kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Waziri wake na Naibu wake na watendaji wote kwa kazi nzuri waliyoifanya. Lakini pongezi za ziada ziende kwa mwenyewe yeye Makamu wa Pili wa Rais kwa jinsi alivyokuwa ameonesha ukaribu wake na sisi *back bencher* amekuwa anatusikiliza mawazo yetu na pia kuyafuatilia.

Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Tunguu kwa kunichagua mimi kuwa ndio msemaji wao hapa na naamini kadri ya uwezo wangu katika Kikao hichi cha Bajeti ili niweze kuwapa yale ambayo nahisi yataweza kuwasaidia.

Pia nimpongeze au niwapongeze Waheshimiwa Manaibu Waziri wote ambao wamechaguliwa Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa kuchaguliwa na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi kwa kupata nafasi ya kuweza kusogea mbele ili kuungana na serikali. Naamini Mhe. Rais hajakosea ni watu mahiri, wana uwezo, natumai ule ukali wake Mhe. Hassan kule mbele utaendelea vile vile kama alivyokuwa nyuma ili tuweze kuleta maendeleo kwa kasi kabisa kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mawazo yangu nataka nitoe masikitiko yangu leo asubuhi wakati wa kipindi cha maswali na majibu. Leo asubuhi niliuliza swali la *ZBS* lakini kuna Mjumbe mmoja aliongelea juu ya kero ya wananchi katika eneo la Bandari na juu ya hoteli. Kwa masikitiko sana majibu yaliyotoka ni kwamba yeye hawezi kuyajibu Waziri kwa sababu serikali haipo na kwa sababu sio mwenye dhamana. Lakini niseme kwamba wananchi wana haki ya kusikia majibu kwa sababu Mawaziri wengine walikuwepo. Haipendezi sana kwamba wakati majibu yanatoka juu ya maswali tunayouliza, halafu tunaambiwa kwamba Waziri hana dhamana kwa sababu Waziri husika hayupo, lakini serikali ipo na ufahamu wangu kwamba serikali inafanya kazi kwa *collective dispensability* na kwa kusaidiana.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya hili Waziri alijibu wakati mmoja hapa kwamba katika kero ya wananchi katika eneo la Bandari kwamba hoteli zihame, basi akasema mwenye hoteli ahame na Mawaziri walipiga makofi kushangilia. Nilishangazwa sana kwa sababu majibu yale hayaendani na mawazo ambayo wananchi wanayatarajia. Ikiwa serikali inafurahia majibu kama haya basi nahisi na sisi pia ma-*back bencher* tutakuja kukwaruzana huko mbele juu ya maswali tutakayouliza ikiwa majibu tutayoyapata kutoka sekalini yatakuwa hayaendani juu ya wananchi na matarajio yao. Mimi niombe sana serikali inapofurahia majibu yaliyokuwa hayaendi basi tuwe makini.

Baada ya hapo naomba sasa nianze na mchango wangu kuendelea kuzungumzia maeneo kadhaa. Nitaongelea maeneo machache tu. Kwanza nataka nigusie juu ya suala la Muungano. Mhe. Mwenyekiti, ukiwa mwana CCM safi mambo mawili ni lazima uyatambue na uyathamini. Kwanza ni Muungano na pili ni Mapinduzi yetu Matukufu ya mwaka 1964. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani yake kwa mujibu wa Katibu yetu kuna serikali mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni SMT na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo ni SMZ, nawapongeza wote kwa upande wa Zanzibar pamoja na Jamhuri ya Muungano kwa kushirikiana vizuri katika kutatua zile kero za Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika kuwashirikisha wadau mbali mbali ili kuhakikisha kwamba zile kero au mapungufu yaliyokuwepo tunayapunguza, nizidi kusisitiza kwamba karibuni kumekuwa kuna watu wamekuwa wanatumia Muungano wetu kuongelea yale mapungufu au kero kuyageuza kama sehemu ya chambo katika kuwachanganya wananchi. Mimi niombe tu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais waendelee kujenga ushirikiano mkubwa na yale mazungumzo ambayo faida zinapatikana ndani ya Muungano basi yazidi kusemewa na kusemewa. Kusemewa kwake yasianze kwa nafasi za kisiasa katika maeneo tofauti hapa mfano katika Baraza la Wawakilishi au wanasiasa wanapozungumza, lizungumzwe katika maskuli yetu, yazungumzwe katika vyuo vyake.

Muungano una faida zake uzungumzwe mpaka katika boti ya Bakhresa inapoondoka Dar es Salaam kuja mjini. Matunda ya Muungano ambayo wananchi tunafaidika nayo, wale ambao wanaojaribu kutuchanganya sisi basi na serikali isikae kimya na kutoa majibu kwamba wale madhalim au wabaya wa Muungano wetu wanapojitokeza. Wapo wana

CCM ambao ni viongozi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano nitamtolea mfano Mhe. Kessi ambaye ni Mbunge.

Mhe. Mwenyekiti, ni aibu kumuona kiongozi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatwambia sisi Wazanzibari hatuna fedha ya kutumia sukari kwa ajili ya chai. Hajawakejeli Wazanzibari, hajawakejeli Watanzania, amewakejeli viongozi pamoja na Rais na Serikali yake yote. Mimi niombe Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hasa Makamu wa Pili mwenyewe yeye ni kiongozi pia katika chama chetu, basi watu kama hawa wachukuliwe hatua zilizokuwa stahiki. Haipendezi kutoa maneno ya kifedhuli, wanamtambua na sio mara moja, ni mara nyingi Mbunge huyo amekuwa anatoa maneno kama haya. Nimwambie tu Mhe. Mwenyekiti, hata sisi Wazanzibari tunao mdomo wa kuzungumza, lakini tunaheshimu chombo chetu, tunaheshimu Muungano. Nampelekea salamu kutoka chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi kwamba na yeye pia atambue kwamba na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunao uwezo wa kuzungumza tukamuongelea na tukamchambua mpaka huko katika jimbo lake anakotoka, mpaka watoto wake, mpaka wake zake na mambo mengine yote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nataka nizungumze suala la Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya SMZ iliyokuwepo Dar es Salaam. Nichukue nafasi hii kumpongeza Makamu wa Pili, lakini naomba kusisitiza mara hii kwa vile Mhe. Rais John Pombe Magufuli ameamua sasa kuihamisha serikali yote kuipeleka Dodoma. Ukiangalia katika mpango mzima wa kufanya kazi sasa hivi inaelekea huko mbele watendaji wengi wa serikali watakuwepo Dodoma.

Umuhimu wa ofisi hii ya Dar es Salaam ni kuhakikisha kama wanakuwa na watendaji wa kutosha na wale watakaokuwa na uwezo wa kuongea lugha za kigeni kama Kifaransa, Kichina ili kufanya kazi na ukaribu pia na Ofisi za Kibalozi na Taasisi nyengine za Kimaifa kuhakikisha na SMZ na wao katika utendaji wao na kazi zao za kila siku wenzetu hawawi mbali sana. Tunapowapeleka katika ofisi hii tuhakikishe isiwe ni chaka la kujificha, pale ambapo watu wamepata uhamisho Dar es Salaam basi mume au mke na yeye anaomba kwenda kupelekwa pale ili awe karibu na mwenza wake. Hii iwe ni sehemu ya ofisi ambayo inayotambulika, inayoheshimika na iwe na watendaji wa kutosha hata sisi wenyewe Wajumbe tunapotaka taarifa tuwe tunapata msaada wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niongelee Tume ya Uchaguzi. Naomba sana katika Bajeti ya Tume ya Uchaguzi inayoelekea mwaka huu katika mpango umepata uratibu wa kazi basi bajeti yao wasicheleweshewe, watiliwe kila pale wanapohitaji ili kazi zao ziweze kwenda vizuri na waweze kufanya mpango wao. Kwa sababu uchaguzi haupo mbali ni mwaka wa 2020 watakuwa na mipango mingi ambayo wanataka iende kwa wakati, basi waweze kuyatimiza yale ambayo wameyakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niongelee suala la maafa. Mwaka jana nilizungumza umuhimu wa serikali kutoa taarifa kwa wananchi kwa kutumia Kampuni ya Simu ya *Zantel*. Nimeeleza mara nyingi kampuni hizi za simu wana uwezo wa kutoa *messages* pale panapokuwa na vimbunga, upepo mkali au mvua kubwa. Tunajua kwamba serikali ina hisa katika Kampuni ya *Zantel,* ni vizuri *Tanzania Meteorological Agency (TMA)* yaani

Mamlaka ya Masuala ya Hewa Tanzania wanapotoa taarifa kama kutakuwa kuna kimbunga kikali au mvua kubwa basi tunaweza kutumia ujumbe mfupi wa simu wakatumiwa wananchi. Kwa mfano, Mkoa wa Kusini na ndugu zetu kule Pemba ambao wengi wanatumia bahari kuwa sehemu ya kwenda kuvua, pia kutafuta rizki zao basi wapate kujua kwa sababu sio wote wanaopata taarifa za redio, unapomtumia mtu ujumbe wa simu alfajiri na mapema pengine hajawahi kusikiliza redio basi akipata ile *message* itamsaidia.

Mhe. Mwenyekiti, katika kulizungumza suala hili mchango huu nimetoa tangu mwaka 2016 nimezungumza 2017 na 2018 sijapewa majibu, sijui kama serikali imekuwa inapata ugumu au mawazo yangu pengine sijafahamika vizuri. Namuomba Waziri mwenye dhamana ambaye ni Mhe. Mohammed Aboud Mohammed (Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais) ili wazo langu hili ninalolisema na kulirudia kila mwaka nipate kujua kwamba limepokelewa au laa au niweze kuliboresha ili wananchi waweze kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nichangie masuala ya dawa za kulevya, bado Zanzibar tukiangalia jinsi wageni wanavyoingia suala la dawa za kulevya ni muhimu kuliangalia hasa katika maeneo ya bandari zetu ndogo. Hizi bandari ambazo kama mfano zinatumika na vyombo vya kawaida. Lakini pia Bandari zetu kubwa pamoja na *Airport* ni muhimu kuhakikisha ulinzi unakuwa mzuri, ni muhimu sana kuhakikisha kwamba tunaweka *CCTV*. Mtu au mgeni tangu anaposhuka katika boti au ndege tunaangalia mwenendo wake, kijasho kinachomtoka, khofu aliyokuwa nayo kama huyu kweli amebeba, hivi ndivyo wenzetu wanavyotumia katika maeneo ya nchi za nje. Unapotembea tangu unapoingia *point of entry* unakuwa unaanza kufuatiliwa kuangaliwa kama wewe wanakutilia wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa mtu anashuka kwenye ndege au boti anatoka mbio humjui amebeba mzigo gani. Ni muhimu watu kuwa na uwezo na kuwafundisha ile elimu lakini pia wana uwezo wa kuangalia kwa kupitia kamera ili kuwa-*monitor* kama hawa wamebeba mzigo wowote ambao ni mbaya kama dawa za kulevya au jengine lolote ambalo litakuwa linaleta ubaya katika visiwa vyetu au katika nchi yetu pamoja na kuwaumiza wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya hayo machache niliyoyachangia leo kutokana na afya yangu naomba niishie hapo. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Mhe. Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote. Ofisi yao ni mfano, tunafurahi sana wanapoonesha ukaribu na sisi. Naunga mkono mawazo ambayo aliyatoa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwamba *issue* ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi waendelee kuiangalia hasa katika masomo na Wawakilishi kupata nafasi angalau kutoa matongo na kuweza kusafiri katika nchi za jirani na nyenginezo ili kwenda kujifunza.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja mia juu ya mia, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Simai Mohammed Said, sasa baada ya hapo namwita Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Abdalla Maulid Diwani ajitayarishe pamoja na Mhe. Hamad Abdalla Rashid ajitayarishe.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika salama hapa, lakini pia kuendeleza Baraza letu tukufu. Pia nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika jitihada zake za kuiletea maendeleo Zanzibar na watu wake.

Pia nimpongeze Makamu wa Pili wa Rais katika jitihada zake za kuisaidia Zanzibar katika sekta zote za masuala ya Wizara na Mawaziri wote wanaofanyakazi kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Manaibu Waziri kwa kujitahidi kufanya kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nianze tena kwa kumshukuru Makamu wa Pili wa Rais katika kutoa hotuba yake hii ambayo imesheheni kila kitu, isipokuwa tunaongezea na kukazia kwa yale ambayo tunahisi yanaweza kuendeleza zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na masuala ambayo kwa upeo wa Zanzibar. Zanzibar katika miaka ya nyuma ilikuwa ni kitovu kizuri sana cha kuja watu kusoma au kuja watu kuiga katika masuala mengi yakiwemo masuala ya maendeleo lakini pia masuala ya dini, masuala ya michezo, masuala ya utamaduni na masuala mengi ambayo watu wengi wa kanda hizi na hata naweza kusema nchi za Ulaya na Arabuni walikuwa wengi wanakuja kuchukua taaluma kutoka kwetu. Lakini katika miaka ya karibuni taaluma hii imeondoka na sisi tumekuwa waigaji wakubwa wa kwenda kuiga zaidi kuliko taaluma tuliyokuwa nayo ya kutoa.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tumekuwa waanzishaji wazuri wa kila sekta lakini matokeo yake inabakia njiani watu wanatupita wanakwenda kuyafanyia kazi yale tuliyoyabuni na baadaye wanatupita mara mbili yake na kutuchupa katika ule mtindo. Sasa hivi Zanzibar tuna ukosefu wa dini tunakwenda kusoma nje wakati Zanzibar ilikuwa inasomesha. Zanzibar ilikuwa ina maendeleo makubwa, watu wameyachukua wamekwenda kuyafanyia kwao. Zanzibar michezo ilikuwa ni mikubwa sana lakini leo hatuna tena tunaanzisha sasa hivi. Utamaduni ulikuwa mwingi leo haupo, haidhuru taarab imeondoka imekwenda Bara, hapa hatuna tena taarab. Mambo mengi hapa yameondoka isipokuwa sasa hivi tumebakisha sisi tunaiga, ukimuuliza mtu atakwambia unaona nchi fulani, watu fulani wanavyofanya wakati sisi tumeshafanya miaka ya nyuma.

Hili tunataka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Makamu mwenyewe aifanyie utafiti ni sababu gani Zanzibar ilikuwa inaigwa leo tunaiga. Ningeomba sana Waziri atakapokuja atoe sababu angalau kwa nini tunafika hivi. Juzi tunakuja hapa kufanya Kombe la Mpira la Afrika Mashariki tunaona fahari kutokea mshindi wa pili, wakati timu za hapa zilikuwa timu bingwa Tanzania Bara na kwengine tulipokuwa tukienda. Sisi tulikuwa tunapiga taarab mpaka Bi Kidude anapiga Ujerumani na kwengineko, lakini leo hakuna kitu kama hicho ambavyo vitu hivi vyote ni moja ya kuweka changamoto katika uchumi. Watu wanakuja hapa kama utalii ndio sababu zenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilikuwa namuona Mkurugenzi mmoja Bagamoyo anasema hasa kwamba tunajaribu kuweka vitu sawa kuipokonya Zanzibar utalii. Kwa hivyo, wao wanaanza kujipanga kutupokonya utalii, sisi sijui tunakaa wapi kwamba tumeshajipanga kwa utalii, au bado na sisi tumelala tukisubiri kwamba tuje tuige tena Bagamoyo. Juzi nilimsikia kabisa kwenye *TV* mfano alioutolea ni Zanzibar kwamba anafanya jitihada aweze kutupokonya watalii kutoka Zanzibar. Ninachotoa tahadhari watu wameshatuona tumepewa uzuri wa utalii tukaze kamba tusiregeze.

Mhe. Mwenyekiti, nalizungumzia suala la *Sober House* ikiwa ndio sababu ya dawa za kulevya. Mimi humu kwenye kitabu zamani *Sober House* ilikuwa ni moja, zikaendelea zikawa 10, zikawa 20, kila siku zinazalishwa *Sober House.* Mimi nilifikiri zitapungua na kila siku tunapiga vita suala hili la dawa za kulevya, jitihada kubwa zinafanyika lakini bado *Sober House* ndio zinaimarishwa. Sasa wapi tunakwenda kuimarisha au kupunguza.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba hili suala la *Sober House* litazamwe kwa macho mawili, isije ikawa ni mradi huu, maana yake lazima tuangalie inakuwa matatizo kumbe ni mradi. Kwa hivyo, tuangalie zaidi Mhe. Mwenyekiti, hilo nilikuwa naweza kulisema.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la athari ndogo ndogo, suala la wagonjwa wa akili. Mhe. Mwenyekiti, wagonjwa wa akili huku mitaani kwetu hasa Pemba utawakuta wamelala barabarani, wamekaa, kila mtu unayemwambia anakwambia sio peke yangu, sio mwenyewe, polisi sio wa kwake, madaktari sio wa kwao, sijui wizara gani sio wa kwao, Mkuu wa Mkoa sio wa kwake, Mkuu wa Wilaya sio wa kwake hajulikani huyu. Mimi ningeomba Mhe. Mwenyekiti, katika suala la kuweka mambo haya moja ni suala ambalo lipo hapo wagonjwa wetu wanapelekwa Kidongochekundu na Pemba wajengewe wapate kijisehemu wawekwe. Usafiri huu Mhe. Mwenyekiti, wengi wanajitupa baharini wakiletwa huku, wengi wagonjwa wa akili wanamalizia Nungwi hawafiki wengine. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akaweza kuwajengea kisehemu ambacho kidogo kikaweza kukidhi haja na pia kupunguza baadhi ya hasara ambazo zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwa sababu muda haupo lakini zaidi ni katika sekta ya usafiri. Mhe. Mwenyekiti, katika suala la uchumi bila ya usafiri au miundombinu uchumi haukui. Mheshimiwa bado Pemba usafiri ni mgumu sana na ni suala ambalo litazamwe kwa sekta kweli kweli ikiwezekana. Mhe. Mwenyekiti, Pemba juzi nimeona angalau imeruka ndege usiku kuanzia saa moja ya *As Salaam* hata mimi nilikuwemo, watu walifurahi kwa sababu wengine hawajawahi kuruka na ndege wakaona taa. Mimi nilikuwa nimekaa na bibi mmoja wa miaka isiyopungua sabini akaniuliza dereva anaona, maana yake yeye anafikiri labda kuwasha taa ni kama barabara, nikamwambia aaa yule anatumia vifaa. Ah! alipotua hajaamini. Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine si lazima raha wakupe watu raha jipe mwenyewe. (*Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Pemba una taa nzuri, una *facility* zote na wafanyakazi wake wamejitahidi vizuri wameturusha katika hali nzuri sana pamoja na mawingu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna haja sasa hivi uwanja kwa muda huu usogezwe angalau saa mbili za usiku, kuna wafanyakazi hapa au Mawaziri wanakwenda Pemba

wanatakiwa asubuhi lakini kazi yao inamaliza saa kumi na moja au kumi na moja na nusu, wacha saa mbili iruke ndege warudi waje watufanyie kazi. Bila ya kufanya maendeleo kama haya Mheshimiwa hayawi, kuna Wawakilishi wanatakiwa katika majimbo yao, lakini mpaka kesho saa nne, saa sita siku imekwisha. Mheshimiwa hatuna umri miaka yetu thalathini, ishirini na tano mtu ana maradhi tele na nchi yenyewe tunaendelea hivyo, lazima usiku tuufanyie kazi. *(Makofi)*

Wakati wa kulala umekwisha wenzetu Wachina wanafanyakazi masaa yote unalala masaa manne, sisi tunafanyakazi masaa sita au masaa manane, tunalala masaa kumi na sita, sijui masaa kumi na sita tunafanya nini, tunazidi kuzaana halafu hatuna cha kufanya tatizo limekuwa kubwa.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tutazame mambo ya sekta ambayo yanaweza yakatusaidia katika kukuza uchumi moja ni usafiri. Mhe. Mwenyekiti, Pemba haijawahi kufanyiwa kazi, Pemba ina pesa, Pemba ina mambo mengi tatizo ni usafiri. Mheshimiwa nimeuza karafuu Pemba pesa zote zimeishia huku huku kwa sababu kule vitu vyao havinunuliki, kitu unachonunua Unguja, unachonunua Dar es Salaam, unakinunua mara mbili Pemba. Ni tatizo la usafiri hakuna boti zinazokwenda kwa kasi, hakuna ndege zinazotosheleza, ndege zenyewe zote hakuna unayotia hata boksi, ukiingia wewe upenye ndio lazima na ile nchi iweze kuendelezwa. Pale ni kisiwa cha pili ambacho kingeleta manufaa makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ningeendelea hapo lakini kwa sababu muda ni mdogo. Lakini Mheshimiwa nataka nizungumze kitu kimoja samahani sana naingia katika sekta hii ya dini kidogo. Mheshimiwa sekta ya dini tunasema kwamba hapa karibuni tulimuona Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam amechukua wajane na kuwaleta watu akiwaambia huyu ni mwanao, huyu si mwanao. Hii sekta nataka Makamu wa Pili wa Rais, Waziri aje aniulize na Zanzibar inakuja? Maana yake sasa hii tuangalie taratibu za kwetu sisi tumeweka talaka na ndoa, Mufti, Mahakama kila kitu wale waende kule wakapeleke ripoti zao sio tuitane kwenye magazeti kila mmoja aoneshwe mtoto wake inakuwa aibu, wengine Mawaziri humu wakubwa itakuwa aibu haifai. Lazima tuangalie tusije tukauchukua utaratibu ule tukawapa *power* Wakuu wa Mikoa na wao wakaja wakafanya kama vile, tuweze kuwazuia kabisa lazima tuangalie hii hali, *DNA* tu hapa tumeikataa kwamba isitumike kwa mambo ya ndoa kwa hivyo lazima tuangalie.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niongeze zaidi kwenye masuala ya uchumi. Mheshimiwa vitega uchumi vya viwanda vidogo vidogo vimetajwa humu. Mheshimiwa Pemba masuala ya viwanda vidogo vidogo vya matunda na mambo mengine bado bado kabisa havijatiliwa mkazo, matunda mengi tunayaharibu, mengine watoto wanacheza mpira kama maembe ukienda maeneo yale ya Mchangamdogo. Mheshimiwa lazima tukubaliane viwanda vidogo vidogo vinasaidia uchumi wa aina zote watu wanapata ajira, Serikali inapata mapato inakuja ile nchi inakua, lakini sasa viwanda hatuna, tuna ndizi za kila aina sasa hivi tunakaanga ndizi wenyewe tunauza, wakati kungekuwa na viwanda vya ndizi ambavyo vinazalisha kama chipsi, ndizi zinaanguka zikiharibika ovyo, tuna ndizi za kuweza kuzalisha sana lakini wapi viwanda hatuna. Mimi ningemuomba Waziri

wa Viwanda na Biashara bado ajikaze na Naibu Waziri mpya bado alikuwa na kasi kubwa sana sasa atuletee viwanda kule Pemba lazima tuweze kwenda hapo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nilizungumzie tena suala hili la mambo madogo madogo tuliyonayo ambayo zaidi tumeyatega sana kwenye masuala ya sekta ambazo kama ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mufti sekta hizi ambazo zinajulikana kama sekta za Muungano. Mheshimiwa tumezidharau, Mkuu wa Mkoa anakwenda ofisini kwake, ofisi mbovu, Mkuu wa Wilaya ana kibanda, Mufti ana jengo zuri, nimekwenda juzi kochi la nje la Mufti lile wanalosubiria wageni unaingia mpaka unakaa kitako chini. *(Makofi/Vicheko***)**

Mufti wa mwenzetu akija kwenye nchi basi nchi nzima inaneemeka na Mufti wetu hata kumwita kwenye chuo unaogopa, hana *personality* yoyote, hana uwezo wa pesa, mimi sifikiri kama hata *OC* anatiliwa yule, hana pesa, hana chochote labda aombe msaada wa kupelekwa tunafanyaje? Huyu ana sekta kubwa ya dini akenda kwa wenzetu watu wanamuonaje, huyu lazima Mheshimiwa tumsuke kwanza tumvalishe, avae vizuri, apewe pesa za kutosha sekta kubwa hii, lazima tuiangalie. Lakini unakwenda kochi la nje, nimekwenda juzi nina shida pale naambiwa kaa kitako, *wallahi* Mheshimiwa nenda kesho nimekaa chini lile kochi unapita mpaka chini, nataka kunyanyuka mpaka nifungwe jeki hivyo, kochi la Mheshimiwa wanakuja watu wa Mufti kutoka nje.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kuna sekta hizi kubwa kila mmoja akifikwa na tabu yake Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mufti hizi sekta kubwa watu wengi wanakuja kutuangalia, watu wanatumia vipaji mbali mbali nakwenda kumuangalia Mkuu wa Mkoa, ofisi ndio hii unanitapeli au ni kweli ofisi ndio hii. Kwa hivyo, ningeomba sana ofisi kubwa kama hizi ambazo wanazitumia watu wa aina zote zitazamwe kwa hali ya juu sana tusitazame maofisi yetu mengine. Tunajenga maofisi yetu sisi ya mawizara tu, lakini wale watu ambao wanashughulika na watu ofisi zao hazifai. Kwa hivyo, ningeomba sana Mheshimiwa katika utaratibu huo zaidi ni suala hilo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze suala la ubakaji bado hasa Pemba tatizo nini. Kwa nini wizara haifanyi utafiti ikatuelekeza tatizo hasa la Pemba tumefikwa na nini hili suala limekuwa zito maana yake halina matamanio, ingekuwa kama angalau watu wanabaka wenye mizigo mikubwa basi tungesema yale matatizo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mtoto wa miaka miwili, mtoto wa mwaka mmoja huu si uchizi na bado sisi tunakaa tukiulizana tunasema kitu gani. Zile ni tafiti za kitaalamu za kuwapima watu Mheshimiwa, watu ni wagonjwa wa akili mambo mengine lazima tutazame yale hayaji tu hivi hivi kwa sababu ya kusema kwamba hili hapana hili suala ni la uchizi lazima hawa watu si wenye akili zao.

Mhe. Mwenyekiti, mtu mwenye akili zake akitaka kumuingilia mtu lazima ajipime kwanza huyu ananifaa hanifai mbona ana hili. Lakini wewe unachukua mtoto mchanga yule hata kumla anaweza, anaweza akampika Mhe. Mwenyekiti, akamla yule. Lazima tuwapime hawa watu. Kwa hiyo, lazima tuwe makini kuhusu kitu hicho tusikae tu tukasema kuna matatizo haya inawezekana kuna *element* fulani ya uchizi imetuingia kule Pemba, haiwezekani namna hii lazima tuwe katika hali nzuri ya kuangalia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka niangalie masuala ya barabara. Mhe. Mwenyekiti, barabara moja hivi sasa kama Mkoani mwaka uliopita barabara imekatika imedidimia chini, mara hii imeshakatika tena imeshadidimia yote chini watu wanakwenda pande mbili. Mhe. Mwenyekiti, pale pahala kumbe kwa historia niliyosikia hata hao watu wa zamani waliotengeneza barabara ile walipakimbia pale kuna shimo la asili chini linadidimia. Lakini kesho itajazwa tena pale na mwaka huu itajazwa tena na mwakani litadidimia tena, tuondokane na pale hatuna utaalam wa kupaweza. Kuna maeneo ya zamani hatukuwahi kupata athari hata siku moja tumeshayawacha yameshajengwa nyumba sasa hivi, sasa tukazivunje halafu tulipe maana yake ndio imekuwa sababu hiyo. Sasa Mheshimiwa pale tuondokane kwa sababu hatupawezi tupajaze tupaweke katika sehemu papandwe miti tukate kona nyengine tuelekee.

Mhe. Mwenyekiti, suala kama hili Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anajenga nyumba kule Pagali, lakini katika mtoko wake wa kutoka katika sehemu ya barabara inayokwenda Wesha anatoka karibu na daraja. Daraja lililoko pale sasa hivi limeshazidiwa ukimwambia Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji anabisha, ngoja iondoke halafu atakuja kutwambia kwa nini imeondoka imeshang'oka. Sasa mimi ningeomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa jitihada zao ni wasikivu sana hasa Mhe. Mohammed Aboud Mohammed. Barabara inayotoka Pagali isipite nyuma ya daraja ipite mbele ya Skuli ya Wesha ili tuje tutokezee tupate salama, iking'oka daraja ile hatupati umeme Pemba, hatupati mafuta Pemba, hatupati chochote ile barabara imeshazidiwa imeshachoka.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais barabara ambayo ataitoa ya Pagali asirudie tena kuja nyuma ya daraja la Pondeani apite mbele ya Skuli ya Wesha au kati kati ya Skuli ya Wesha wataalam watamwambia ili tunusurike pakitokea dharura ile sisi watu tuweze kufanya mambo yetu kwa *Taqwa*.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nizungumze hilo zaidi, lakini suala ambalo zaidi nalichukulia la masuala ya mvua, juzi kidogo tena suala la Tibirinzi mambo yaongezeke kidogo tu maana yale ile Hoteli ya Archipelago ilishaanza kuingia maji tena mara ya pili. Lakini Mhe. Mwenyekiti, masuala haya tuna nyumba ambazo tayari tumeshazipiga X katika kila sekta katika kila Wilaya hizi ni hatarishi. Lakini tunachukuaje kuzivunja tukachukua maamuzi kama yaliyochukuliwa maamuzi ya Dar es Salaam kuziondoa nyumba zile, sisi mpaka tusubiri ushahidi kamili, nyumba hazifai kila mwaka zinaingia maji kwa nini tuchukue makosa ambayo kila siku yanajirudia.

Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar hapo zamani ilikuwa haina utaratibu wa masika kuweza kuingia maji. Lakini tunatazamana tunaoneana haya hatujui tufanye nini. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeshauri sana mvua za mara hii zimeshapita basi ndio mwa mara hii tayari lakini serikali imejitahidi kweli kweli kufanya kila jitihada kuokoa maisha ya watu. Kwa nini itumie pesa nyingi kwa masika, serikali ikifika masika tayari imesha-*panic* kwa nini wala haijatokea maafa ni mvua tu ni suala la maji basi bahari tunazo, maeneo tunayo lakini kuondoa nyumba moja, kuondoa nyumba

mbili bado tunabakia kuwa kila mtu hawezi kuweka sahihi ya kuondoa nyumba. Sasa serikali inaoneana hivyo basi iwafidie waondoke lakini wasituletee maafa.

Mhe. Mwenyekiti, Ziwamaboga, hapo Mwanakwerekwe na mambo mengine ambayo maeneo chungu nzima yanakuwa ni tatizo kubwa sana barabara haipitiki tena watu tunawasumbua. Lazima tuseme mtu huwezi ukamtoa maeneo ya hapa kati kati ukamzungusha mpaka Mwera, ukamzungusha mpaka maeneo fulani kwa kukimbia maji ya barabarani. Hili suala serikali lazima itazame, hapo Mwanakwerekwe kama tunaamua kuvunja nyumba kwa upande wa pili tuzivunje vyumba tupate nafasi ya upande wa hapa kwenye kidaraja kidogo sijui kinaitwa kidaraja cha Mhe. Shamsi Nahodha, sijui kama ndicho lakini kile kidaraja kidogo, ndicho kinachotuokoa. Lakini tutakuja kufanya hasara zinapita gari za tani kumi pale, tani kumi daraja lile, tani kumi kwenye nyumba zile. Kwa hivyo ni lazima tuangalie mustakbali ambao lazima suala kama hili lijulikane.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimeona humu katika masuala ya Afya madaktari karibu kumi na tano wanapelekwa Cuba kusoma. Mheshimiwa Pemba tuna tatizo la madaktari, Pemba maradhi yamekuwa makubwa, Pemba hospitali tunazo, Pemba tatizo ni madaktari bingwa hatuna, tatizo la madaktari bingwa wewe ukimwambia mtu tu una tatizo gani, akikwambia tu nina tatizo la maradhi makubwa anashika kichwa Hamadi nishakufa! Kwa sababu hawezi kwenda kukaa Dar es Salaam, atakaa Dar es Salaam kwenye nyumba ya nani, atakaa Dar es Salaam hoteli gani, matibabu atafanyiwa na nani, lakini hesabu zote hizi Mheshimiwa zinakuja kwa sababu ana hiari auze nyumba, ana hiari afanye kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, kwetu Pemba ukiumwa umefilisika hata uwe tajiri na akiumwa ndugu yako umefilisika hutomuacha ndugu yako anaumwa wewe usiuze nyumba, usiuze gari, usiuze kila kitu. Tatizo la madaktari bingwa Pemba pamoja na vifaa bado tulifanyieni kazi kuokoa ndugu zetu wale, na tatizo kubwa Mheshimiwa linalojitokeza ni tatizo kwamba madaktari bingwa hamna kitu kinaanza kidogo, kinaanza kipele tu lakini kwa sababu mtaalam hapana basi linakuwa donda ndugu anakwenda kumalizikia mbele kwa mbele. Kila siku sisi tunapokea majeneza *Airport* pale ameshakufa kwa sababu gani. Huko Dar es Salaam mimi nafikiri ni bora tuwekewe sehemu maalum ya kuzikana maana imekuwa sasa watu wote wanakufa Dar es Salaam eh! kwa sababu ya matatizo makubwa.

Kwa hivyo ni lazima Mheshimiwa sasa hivi sekta ya afya ikiungana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ofisi yake ijitahidi kwa hali na mali. Mhe. Mwenyekiti, Pemba suala la homa ya ini imeshakamata kweli kweli sijui sababu yake nini. Lakini pale Chake Chake kuna wagonjwa wasiopungua watano wamekufa juzi kwa homa ya ini na wengine ninao hivi sasa, ini sijui tatizo liko wapi. Lakini nataka kwamba yeye kama Waziri aje akague nimuoneshe makaburi na watu wake na wengine wapo hai wa homa ya ini imekamata Pemba sijui sababu nini.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna haja kunambia nimeshasalimu amri nashukuru naunga mkono hoja. Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nilikupa muda wa ziada sio kwamba nimekosea, nimekupa muda wa ziada kidogo lakini ahsante kwa kuutumia vizuri. Sasa namwita Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Hamad Abdalla Rashid ajitayarishe.
Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa na mimi kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Pili, namshukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais juu ya usomaji wake, alipowasilisha hotuba yetu hiyo kwa ufasaha na kwa umakini mkubwa zaidi.

Vile vile nawashukuru watendaji wote wa ofisi hii kwa umahiri wao na utendaji kazi uliotukuka na kuleta matumaini kwa Wazanzibari walio wanyonge wale alipenda kuwa nao mwenzangu wakwezi na wakulima wa nchi hii.

Niende moja kwa moja katika mchango wangu ukurasa wa 16 (xiii) Ofisi ya Mratibu ya Utekelezaji wa Kaya Maskini *(TASAF).* Napenda sana kupongeza *TASAF* hususan miaka hii miwili umeiona kule *TASAF* iko makini kunusuru kaya maskini, nakumbuka kwamba *TASAF* mradi huu umekuja *TASAF I, TASAF II* na *TASAF III.* Lakini hizi zote nathubutu kusema kwamba walikuwa wababaishaji tu hii miaka miwili tumeona kweli na sitokuwa mkosefu wa fadhila kama sitompongeza yule Mratibu wa Shughuli za *TASAF* Zanzibar, Mkurugenzi Khalid anafanya kazi vizuri sana Mwenyezi Mungu amjaalie na uzalendo aliokuwa nao juu ya nchi hii na watu wake.

Kama si imani yake na uzalendo hizi sifa zisingeweza kutoka, zinatoka sifa hizi kutokana na uzalendo aliokuwa nao wa kutumikia wananchi wa nchi yetu hii, wanyonge wasiokuwa na uwezo wale ndio watu waliolengwa katika *TASAF* hii. Imekuwa somo kwa baadhi ya nchi nyengine duniani kuja kusoma kwamba Zanzibar *TASAF* mmefanya vizuri na mmefanikiwa kwa misingi gani, kumbe ni usimamizi mzuri wa Mratibu akisimamiwa na Makamu wa Pili wa Rais wa nchi hii, napongeza sana katika hilo. *(Makofi)*

Vile vile niende katika ukurasa wa 22 Tume ya Uchaguzi. Wenzangu waliotangulia kusema walisema na mimi nitakazia. Nimeona kwamba katika Tume ya Uchaguzi pamoja na kazi kubwa wanayofanya lakini hiki kiwango ambacho kilichotengewa kwa Tume hii ni kidogo ukilinganisha na kazi ambazo tulizokuwa nazo mbele. Mwenzangu mtangulizi wangu Mhe. Machano Othman Said akazungumza na wengineo, ningeomba basi wapunguze baadhi ya fungu ili kuipa nguvu Tume ya Uchaguzi kwa sababu ndio roho ya nchi hii, bila ya Tume ya Uchaguzi sisi sote humu tusingekuwepo. *(Makofi)*

Tumekuwepo humu ndani kwa hiyo Tume ya Uchaguzi kufanya kazi zao vizuri, lakini tusiwape wakati mgumu watu wale wakawa wanafanyakazi kama yatima, kwa sababu ya fungu lao lililotengwa hapa la bilioni moja na sabini na sita ni pesa ndogo sana ukilinganisha ni bajeti ya mwaka mzima na bajeti yenyewe hawezi kupata hata asilimia 80. Tumeona bajeti iliyopita alipata kiasi cha asilimia 76 sihaba, sasa angalau basi juu ya bajeti hii ndogo iongezwe iweze kuwa kidogo ivute ili waweze kujikidhi na mambo mbali mbali. Wana masuala ya uandikishaji wa wapiga kura wapya, kulipitia daftari upya ili ikifikia mwaka 2020 tusipate shida. Ningeomba sana Tume ya Uchaguzi fungu lake liangaliwe. Najua Mhe. Makamu wa Rais chini ya uongozi wako na majemadari wetu Mhe. Mohammed Aboud Mohammed hilo kalisikia na atalifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele na mchango wangu niweze kuchangia Tume ya Madawa ya Kulevya. Nimesema maalum nichangie hili kwa sababu mimi katika jimbo langu eneo la Kidongochekundu nina *clinic* pale ya *methadone* ya wale vijana ambao wana *control* kuacha kutumia dawa za kulevya. Cha kusikitisha vijana wale bado wanakwenda katika suala la kupunguza matumizi ya dawa za kulevya lakini imekuwa kero kwa wananchi wakaazi wa eneo la Kidongochekundu kwa sababu wale pale wanasambaza kuanzia asubuhi saa 12:00 mpaka saa 5:00 asubuhi hawana eneo maalum walilotengewa mle ndani ya *Mental Hospital.* Ningeomba sana bajeti yao hii watengenezewe angalau banda mle ndani waweze kukaa asubuhi wanapokwenda pale ili wasizagae nje.

Imefika wakati hata watu wanalalamika wanafanya mambo hata mnyama hawezi kufanya wakati wa asubuhi na mchana katika vichochoro vya Kidongochekundu. Nimekwenda kuongea na Sheha anasema hawezi mara mbili kuhusu suala hili amekwenda mpaka kupeleka taarifa zake polisi kidogo wakaja kutiwa mikwaju pale kwa namna ambavyo wanazagaa katika maeneo yale pale na hawatulii na kwenda katika vichochoro vile. Tena kinachoonekana ikionekana nguo imechukuliwa, ikionekana baiskeli imechukuliwa kwa sababu wanashindwa kuka-*control* katika eneo lililotengwa la *clinic* ya *methadone* mle ndani ya hospitali.

Ningeomba sana mheshimiwa suala hili lichukuliwe kwa umakini ili likatizamwe namna ya kuwadhibiti wale vijana. Nashukuru sana wameamua kwa ridhaa zao kuacha kutumia dawa za kulevya na wanakwenda pale kila asubuhi kwenye *clinic* ile kupata ile dawa, lakini maeneo ya kusubiri zamu zao za kupata dawa hamna katika eneo la *Mental Hospital.* Nafikiri nyinyi nyote mkitembea pale asubuhi mnaona vijana wanazembea zembea kuanzia mlango wa Bomani mpaka *Mental Hospital* imekuwa ni kero kwa wakaazi wa maeneo yale. Ningeomba tena Mhe. Waziri katika suala hilo ulichukue na ulifanyie kazi ili kuona ile changamoto iweze kuondoka.

Lakini vile vile nikiendelea mbele nazungumzia juu ya suala zima la Kituo cha Kurekebisha Tabia Kidimni ipo katika ukurasa wa 47. Nashukuru kwamba hii leo inakuwa bajeti ya tatu tunakizungumza kituo hichi, mara iliyopita tulianza kuleta kelele ilitengewa *1.5 billion* ya ujenzi wa kituo kile kwa kweli hakuna kilichofanyika imekuwa ni jipu. *(Makofi)*

Imekuwa ni jipu ambalo kidogo sasa hivi inafanyika. Lakini leo mmetuletea kwamba mmetenga tena milioni mia tano sijui zile za *one point five* zilizotengwa mwanzo zimefanyiwa kazi gani. Ningeomba sana mheshimiwa katika hivyo ili tukabili zile *one point five billion* zilizotengwa katika miaka miwili iliyopita nyuma mpaka miaka mitatu kipindi kile ilikuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, fedha zile zimefanyiwa kazi gani hata leo bado zitengewe milioni mia tano kwa ajili ya ujenzi wa kituo kile pale.

Imekuwa ni jipu kila siku tukizungumza katika masuala kama yale imekuwa sawa sawa na kupepea uporo. Ningeomba tu ili kuondoa wasi wasi kwa watu wetu basi tuletewe

maelezo ya *one point five billion* zilizotumika mwanzo zimetumika kwa kazi gani mpaka hii leo bado tunatenga milioni mia tano kwa ajili ya ujenzi tena wa kituo kile cha Kurekebisha Tabia pale Kidimni.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nikiendelea mbele nakwenda katika ukurasa wangu wa 31 kifungu cha tano (ii) hapa nakutana na suala zima la sherehe za Maadhimisho ya Kitaifa na Kuwaenzi Viongozi Wakuu lakini nakwenda katika suala la sherehe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana mimi ni mshabiki sana wa mpira na katika sherehe zetu za Mapinduzi kila mwaka kunakuwa na mashindano ya *Mapinduzi Cup.* Nimeshuhudia kwa macho yangu mtu kama Naibu Waziri wa Katiba na Sheria anadharaulika kukaa pale *VIP* hana *status,* Naibu Waziri anawekwa chini pale, juu *VIP* anakaa mtu maarufu tu kwa sababu pengine anajulikana sana mjini, pengine ana pesa kidogo anakaa pale. Lakini *status* ya Naibu Waziri haijulikani sembuse sisi wengine hatujali tumekumbana na changamoto mbali mbali katika kipindi cha mashindano yale na wakati wenzetu waratibu hawa wa SMZ katika suala la Sherehe na Mapambo wapo.

Imekuwa dhararu kwa viongozi wa Baraza la Wawakilishi zimekuwa kubwa nathubutu kutamka hayo bila ya kimeme kwa sababu ni kweli tumekumbana nayo kila tunapokwenda katika hata shughuli mbali mbali za sherehe au shughuli mbali mbali zilizofanyika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Wawakilishi hawana nafasi. Kwa kweli inasikitisha sana sisi ni wawakilishi wa wananchi katika majimbo yetu na zile sherehe zinazofanywa ni sherehe za nchi yetu, lakini leo hii utakuta mualiko wanapatiwa watu wamo kwenye *status* za chini, samahani tunazungumzia mualiko ule wanapatiwa ma-*lesbian,* ma-*gays* wanapewa mialiko anaachwa mwakilishi wa jimbo ambaye yeye kachaguliwa na huyo ambaye kachaguliwa na huyo aliyempa mualiko sijui kuna taratibu gani ambapo unapita mpaka ikawa hivyo.

Mheshimiwa kwa masikitiko sana naomba sana hii Taasisi ya Sherehe na Mapambo iangalie *status* za Mwakilishi ni kubwa sana katika nchi hii yupo katika mhimili ambao unatunga sheria katika sherehe za serikali mwakilishi yule hana thamani kwa kweli kidogo hapa panatia walakini. Ningeomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hili suala waliangalie ili haya malalamiko yasiwepo, lazima wawakilishi wapewe nafasi yao hata kama zinakuwa kidogo lakini wapewe na wao wajisikie kwamba wanatambulika katika nchi hii, sio kutambulika katika Baraza la Wawakilishi tu, bali katika shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwakilishi lazima awepo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapofanya ziara katika majimbo au katika wilaya mbali mbali tunamuona jinsi anavyoambatana na wabunge wa maeneo yale. Lakini kwa Zanzibar iko tofauti Mhe. Mwenyekiti, tumethubutu kuona sehemu zote anazokwenda Makamu wa Rais, sehemu zote anazokwenda Rais wa Muungano anawasimamisha wabunge wa maeneo yale pale waweze kuzungumza yale ambayo waliyoyafanya au hata kumpongeza Rais, lakini kwa Zanzibar halipo suala hilo. Ningeomba sana mheshimiwa hili lichukuliwe ili hizi changamoto zetu zisiwe tena changamoto bali upatikane ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele nakwenda katika suala la Tume ya Ukimwi. Tumeona jinsi inavyofanya kazi inashajihisha namna gani watu kupambana na dawa ya ukimwi. Lakini pongezi tu jana tumeona wenzetu Tanzania Bara wamezindua dawa kudhibiti kupata maambukizo ya ukimwi, nashukuru sana hongera. Je, kwa Zanzibar sijui tunafaidika vipi na ile dawa ambayo imepelekwa kule Tanzania Bara tayari wenzetu wameshaanza jana wame-*launch* rasmi dawa ya kuzuia maambuzi ya ukimwi sasa na Zanzibar kama ni sehemu ya Muungano na wao najua watafaidi tu.

Lakini hata niliposema mbele nimekuta hawa wametengewa milioni mia sita na sitini na tano ni za kazi za kawaida tu hakuna kazi hata moja ya maendeleo ndio maana hata kujenga jengo hawa wanashindwa, hawawezi kufanya kazi yoyote hii *just* mishahara tu. Je, tupo kweli tunataka kudhibiti maambuzi ya ukimwi au tumeweka kile kitengo kwa ajili ya kuratibu kuna walioambukizwa ukimwi wamekuwa wangapi tufanye nini, namna gani. Ningeomba sana basi tupate maelezo tutakapokuja kwenda hapa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa niaba yako Mhe. Mohammed Aboud Mohammed.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea namalizia mchango wangu sina makubwa sana niende katika suala zima la uratibu wa shughuli za SMZ na SMT. Tunajua mheshimwa kwamba kila muda wameambiwa watendaji wetu hawa kuanzia ngazi za mawaziri wakutane na wenzao wa Tanzania Bara kuzungumiza changamoto au matatizo mbali yaliyopo katika Muungano wetu. Tunaona au tunasikia kila siku kukicha kila mtu sasa hivi amekuwa na nguvu kuzungumzia Muungano wetu anavyotaka yeye mwenyewe kujisikia kuzungumza na kudhalilisha upande mmoja wa Muungano huu si kitu haki kwa kweli, imekuwa ni tatizo kubwa sana na sijui serikali yetu ya Zanzibar ukimya wake huu inakuja na jibu gani.

Kukemea baadhi kuanzia watendaji wetu wanavyosema au hata viongozi wa ngazi ya ubunge kuzungumza vibaya Zanzibar kwa kweli inatosha, inatosha mtu wa Chama chetu cha Mapinduzi anaingia kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini anabeza upande mmoja wa Muungano huko kulikozaliwa Chama cha Mapinduzi.

Chama cha Mapinduzi kimezaliwa Zanzibar mwaka 1977 leo hii unakwenda pale unaizungumza vibaya Zanzibar huoni haya. Kwa kweli inatia simanzi na tungetegemea Mhe. Mohammed Aboud Mohammed basi na sisi angalau basi tujibu tuone yale anayosema kwamba Serikali yetu inakereka lakini tukiona tumenyanza kimya tunaona mbona serikali hai-*react* katika hicho, labda khofu inaogopa kwamba mwendawazimu akisema ukimjibu unaonekana mwendawazimu wewe unafikiri naogopa kufanya kitu kama hicho lakini pongezi.

Lakini hata vile vikao vya kutatua kero za Muungano vimekuwa havitoi *input* nzuri kwa wananchi tukajua kilichotatuliwa kipi. Toka tunazungumza mwanzo tumeweza kuzungumza kero mbali mbali za Muungano, Zanzibar kukosa kutumia fursa katika Muungano. Kwa mfano mzuri sisi tupo katika *East Africa Community* tumeingia kwa Tanzania, lakini wenzetu wa *East Africa Community* wanafaidi Muungano ule wa *East Africa* kuliko Zanzibar tumekosa nini.

Nathubutu kutamka hayo mambo mazuri mambo yale yale ya kawaida ina vyereje Wazanzibari hatuna fursa kutoka hapa kwenda upande wa pili wa Muungano kutembea na magari yetu tatizo liko wapi, hii changamoto mpaka lini itaondoka. Siku hizi *Alhamdulillah* meli za Bakhresa hizo hapo siku zote zinakwenda Dar es Salaam tunaweza kwenda kupakia gari zetu tukafanya *declaration* pale tunafanya mambo yanayotakiwa tukaondoka na gari zetu tukaenda Arusha, Mbeya tunakotaka kwenda tukenda kwa sababu ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi hatuna fursa ile lakini gari inatoka Kenya, gari inatoka Burundi, gari inatoka Rwanda wanafaidi utaratibu kulikoni na utaratibu huu uko *option* katika *custom* mpaka kuna fomu ya *CA 65* ya *Temporary Transportation*, iweje fomu ile iwe haramu kutumika kwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana katika hiyo tumeshasema sana si mara moja, si mara mbili mimi tokea nimeanza kuingia katika Baraza hili kesi hiyo naizungumza kila mwaka lakini bado imekuwa ni tatizo. Ningeomba sana Mheshimiwa kama hizi kero mnakaa mnazizungumza basi na hili litatuke hayo mengine hatuwezi kusema tunajua siku zote kila siku tunaona wanatuambia kwamba masuala ya sukari, lakini tusizungumze sukari hata haya maji ambayo kuna viwanda zaidi ya vitano Zanzibar leo hii imekuwa haramu kwenda Tanzania Bara, ni kero ambazo wananchi wetu hawapati majibu moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa haya yangu machache naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani, sasa namwita Mhe. Hamad Abdalla Rashid na Mhe. Said Soud Said ndiye mchangiaji wetu wa mwisho hadi sasa. Mhe. Hamad Abdalla Rashid karibu sana.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini kwanza na mimi sina budi kutoa shukrani zangu za dhati na kuwapongeza mwenyewe Makamu wa Pili wa Rais, Waziri wake na watendaji wake kwa ujumla kwa hotuba hii maridhawa kabisa ambayo mimi ninaiita hotuba ya funga kazi. Kwa sababu kama hotuba hii itatekelezwa kwa mujibu ilivyoandikwa basi hatuna sababu za mwananchi wa Zanzibar kusema anakosa huduma kutoka Serikali yake ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitatumia muda wako mdogo na nataka kuchangia sehemu tatu tu, kwanza kifungu cha 22 Huduma za Maji Safi na Salama. Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika hotuba hii kwamba katika kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na kutatua kero za ukosefu wa maji katika maeneo mbali mbali ya Mikoa ya Zanzibar hususan maeneo ya Mji Mkongwe na Ng'ambo ya asili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika imo katika hatua za awali za utekelezaji wa kazi ya ujenzi wa matangi mawili ya Saateni na Mnara wa Mbao na ulazaji wa mabomba na maji hayo kutoka kwenye visima. Niipongeze Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na niseme kwamba kuna haja sasa basi utafiti ufanyike kuhakikisha kwamba matangi hayo yatapata maji kwa sababu haitokuwa vyema kujenga matangi na mabomba kusambaza lakini huku chini visima vya maji havipo. Lazima tuwe na uhakika wa visima vya maji yaani utafiti wa maji ufanyike kikamilifu kupitia kwa

Mhe. Waziri wa Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati ili tuhakikishe basi baada ya kujenga matangi haya na mabomba kutandikwa maji yatakwenda kadri inavyotakiwa katika matangi yale ili wananchi wetu wanufaike na maji hayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende kifungu cha 23 ambacho kinaeleza Huduma za Afya. Mhe. Mwenyekiti, huduma za afya katika hotuba hii Ofisi ya Makamu wa Pili imetamka wazi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kupambana na maradhi mbali mbali imeweka mpango wa chanjo Zanzibar tangu mwaka 1981. Niipongeze serikali kwa kuweka mpango huo ambapo hadi sasa jumla ya vituo vya afya 175 vya serikali na binafsi vinatoa huduma za chanjo ili kuhakikisha wananchi wetu wanapata kinga ya maradhi haya ambayo yanaweza kuepukika.

Mhe. Mwenyekiti, chanjo hizi na kwa sababu sasa hivi kuna ugatuzi ningependa kutoa tahadhari kabisa kwa sababu ugatuzi wenyewe unaelekea katika kipindi cha majaribio au awamu ya kwanza. Kwa sababu vituo hivi sasa hivi vimegatuliwa kutoka Wizara ya Afya na vimekwenda Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar sasa kuna haja kama Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alivyotamka humu, kuna haja sasa Wakuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na watendaji wa vituo vya afya hivi kupata mafunzo sahihi ya kuhakikisha chanjo hivi zinatoka. Mfano hai Mhe. Mwenyekiti, chanjo ambayo imetangazwa rasmi humu imetolewa sasa hivi ni chanjo hii ya saratani ya shingo ya kizazi ambayo serikali imefanikiwa kupata chanjo inayoitwa *Human Carcinoma Virus Practice* ambayo itatumika na hususan watapewa vijana wa kike wa miaka kumi na nne.

Mhe. Mwenyekiti, kuna haja sasa basi Wizara hii ya Tawala za Mikoa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa sababu vijana wenye umri wa miaka kumi na nne mara zote wanapatikana katika skuli zetu za Unguja na Pemba, kuna haja sasa elimu kutolewa kubwa kabisa kupitia skuli zetu za msingi na sekondari ambayo yana vijana wenye umri huu ili waweze kuwa na muamko wa kuhakikisha wanawapatia chanjo hii ili kujikinga na maradhi haya. Nishukuru tu kwamba wenzetu wa kike sasa wamepatiwa chanjo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tenzi dume mimi ninavyojua si ugonjwa tunatishika sana tu kwamba ni ugonjwa. Mhe. Mwenyekiti, tezi dume kila mwanamme yeyote aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu anayo kwa kitaalam inaitwa *prostate gland* inakuwa ugonjwa pale linapokuja tatizo la kukua kwa haraka hii tezi dume ambayo tunasema *enlargement.* Baada ya kuuwa *deprose resrus* inapeleka kupata haja ndogo kwa urahisi na kwa sababu nyama kule zimeshajikusanya *cells* nyingi sasa hapo inakuwa ugonjwa ambao sijui kwa nini unaitwa tezi dume. Tezi dume ni *prostate gland* ambayo kila binaadam anayo si ugonjwa kabisa lakini matatizo yanayotokana tezi dume baada ya kuvimba hapo utaitwa huo ugonjwa sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya tezi dume inapoteza nguvu yake kutokana na ule ukuaji mkubwa *enlargement* ya hii tezi dume ambayo inasababisha sasa mwanamme kukosa nguvu za uzazi, kupata matatizo ya kutokukojoa kwa ukamilifu lakini baadaye ina *lead* kuwa *cancer* au wataalam wanaita *carcinoma*.

Mhe. Mwenyekiti, hii nafikiri mimi hakuna haja ya kushtuana na hata wenzetu wa kike washukuru wamepata chanjo lakini hata shingo ya uzazi kila mwanamke anayo si ugonjwa, lakini ukuaji ambao si wa desturi unapokuwa kikamilifu unasabisha ugonjwa wanapata saratani ya shingo ya uzazi. Sasa kuna haja basi ya serikali kutoa mafunzo ya uhakika kwa watendaji wetu wa afya, narudia tena mafunzo ya uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ananisikia kwa sababu vituo vimetengwa kutoka kwao na ugatuzi huu nashukuru wakurugenzi hawamo wapo hawa *DHMT's* na *DMO's,* kuna haja sasa Waziri wa Tawala la Mikoa kushirikiana na watendaji hawa walioko kwenye vituo vya afya na hawa *DHMT's* na *DMO's* kukaaa kwa uhakika kabisa. Lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Afya bado narudia ugatuzi huu hatujauweza, bado washirikiane na Wizara aya Afya kwa sababu wataalam wengi wako Wizara aya Afya kuweza kusukuma gurudumu hili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata kama tunaposema ni uzazi mzuri kwa sababu unapopata huu ugonjwa uzazi unapungua. Lakini ndugu zetu wa kike wasipate hii saratani ya shingo ya uzazi ili afya njema ipatikane kwa wananchi wetu waweze kuzalisha na kukusanya mapato ya serikali hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda hiki kifungu cha 3 ambacho nimshukuru kwanza Mama Mwanamwema Shein kuzindua hii chanjo ambayo Serikali niipongeze kwa bidii yake ya kuweza kufanya kazi na kuhangaika kupata chanjo hii ambayo itatusaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wa chanjo hii bado kabisa kuna haja sasa tukishapata elimu ya watoto wetu wa kike wenye umri wa miaka 14, tukipata elimu ya wafanyakazi wetu, narudi wafanyakazi lazima wawe na elimu kwa sababu hii chanjo inaonekana si kongwe sana bado ni mpya. Kuna haja ya wataalam wetu watakaotoa chanjo hizi kujua vituo vimeshatengwa wajue sasa nini maana ya hii chanjo ni matatizo ya ugonjwa huu kwa sababu wagonjwa wetu kuna kila sababu ya kuwaeleza huu ugonjwa waujue, mtu anapoelewa ugonjwa ndio anapopata sababu ya kwenda hospitali haraka.

Mara nyingi tunafeli kwenye chanjo kwa sababu hatuwapi wananchi wetu elimu ya kutosha kujua matatizo ya ile haja ili kupata kutoka hii chanjo. Sasa ni muhimu kabisa elimu ya afya itolewe kwa wingi kama nilivyosema Mhe. Waziri Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ushirikiane na Wizara ya Afya, haidhuru mmegatuana lakini bado kuwe na mashirikiano makubwa. Wizara ya Afya kuna Wakurugenzi wengi, kuna watendaji wengi ambao wanajua hii ni matatizo bado utawapata wachache ambao wanaotoka huko kwenye *DHMT's* na *DHM's* kuna haja kabisa ya kuhakikisha elimu hiyo inapatikama Mhe. Waziri, ili kuweza kukitimiza kitabu chetu hiki. Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwamba nampongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na watendaji wake kwa kitabu hiki, mimi nakiita kitabu funga kazi ambacho kama tutakitekeleza basi hakuna haja mwananchi wa Zanzibar kulalamika kuwa hajapata matunda ya Mapinduzi ya serikali hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais asilimia mia kwa mia. Naunga mkono hoja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamad Abdalla Rashid. Waheshimiwa Wajumbe, kuna mabadiliko kidogo ya wachangiaji wameongezeka na sasa kuna wachangiaji Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma na baadae atafuatia Mhe. Ali Khamis Bakari.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipa nafasi na mimi ya kuweza kuichangia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa pongezi za dhati kabisa kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na watendaji wake wote wa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia niwapongeze na nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wake wote kwa mashirikiano mazuri na ushiriki wao wa kuweza kuandaa vyema bajeti hii. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenda kwenye michango yangu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye kesi ya usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, kwenye ajenda hii naomba nianze kusema ifuatavyo.

Kwanza nianze kuipongeza wizara kwa kuweza kuona na kujali mahitaji ya watumishi wake kwa kitengo hiki, tukiamini kwamba kitengo hiki kina kazi ngumu sana na wanafanya kazi nzito na katika mazingira magumu sana. Kwenye hilo nipongeze kwa kuweza kujali na kuona kwamba mazingira ambayo wanafanyia kazi ni magumu na kuweza kuwaongezea na kuwaboreshea mazingira yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika mipango yao waliyoeleza wametwambia kwamba wanataka kusaidia jumuiya za watu wenye ulemavu kwa kuwapatia visaidizi na vikundi vya watu wenye ulemavu. Kwa maana hiyo, visaidizi hivi ambavyo vitatolewa hapa ni kwa ajili ya vikundi lakini pia kwa mtu mmoja mmoja. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naiomba sana wizara kwenye ugawaji wa visaidizi hivi waone umuhimu na waangalie na wazipe vipaumbele skuli ambazo zinaanzishwa elimu mjumuisho.

Mhe. Mwenyekiti, hili nimeona niliseme kwa sababu katika ziara zetu ambazo tumepita tumekuta baadhi ya skuli kuna changamoto nyingi sana hasa kwa vifaa vya kuweza kuwapatia elimu ndugu zetu wenye mahitaji maalum. Lakini niiombe sana wizara na idara hii iwe karibu sana na kitengo cha elimu mjumuisho, kwani watakaposhirikiana wataweza kufanya kazi zao vizuri na kuweza kusaidia jamii hii kwa upana mzuri sana.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende kwenye Tume ya Kitaifa ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye jambo hili naomba sana niipongeze tume kwa kazi zao nzuri ambazo wanazifanya, lakini Mhe. Mwenyekiti, nipende kusema sana kwamba tume hii

haileti mrejesho moja kwa moja katika jamii ili kuona kazi zake zinafanya vipi. Jengine tathmini hii ikifanywa maana yake ni kuona na tutawapa fursa wananchi kujua hali halisi ya matumizi ya madawa ya kulevya katika nchi yao, lakini hali halisi na *situation* inavyoongezeka au kupungua katika kesi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, hili tunatambua kwamba wahanga wakubwa wa madawa ya kulevya ni vijana, lakini vijana hawa sasa hivi kwa asilimia kubwa imeongezeka katika maeneo ya shamba sio mjini, na maeneo hayo ya shamba ukigusia Mkoa wa Kusini Unguja na maeneo ya Mkoa wa Kaskazini. Kwa hiyo, mimi nashauri kuwepo na tathmini halali na ya ukweli inayoonesha tatizo hili katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Tume ya UKIMWI na hapa pia nitoe pongezi zangu za dhati katika sekta hii. Niipongeze serikali kwa kuamua kwa dhati kabisa kutokomeza janga hili na faida yake tunaanza kuiona, kwa sababu tatizo ambalo lilikuwa linaikabili taifa letu kwa asilimia kubwa sana na ongezeko hili lilikuwa linaongezeka kwa kasi sana. Lakini kutokana na tathmini iliyofanywa na wataalamu mwaka 2019 kipindi cha Disemba inaonesha kwamba sasa hivi ongezeko la magonjwa haya lipo chini ya asilimia moja kama ilivyokuwa awali. Kwa hiyo, kwenye hili tuipongeze sana serikali yetu na tathmini hii imetolewa na *Tanzania Healthier Empathy* ya 2017. Kwa hiyo, kwenye hili serikali na wizara tuipongeze sana jitihada yao imeonekana. Lakini jambo jengine ni kwamba elimu hii inatolewa kwa baadhi ya watu tukiamini kwamba vijana wengi sana ambao wanaathirika na janga hili ni hawa vijana ambao wapo skuli ikiwemo kwenye vyuo vikuu. Kwa hiyo, niiombe serikali na niiombe wizara iende moja kwa moja kwa wahusika ili ikatoe elimu ambayo itaweza kuwasaidia na hatimae kutokomeza janga hili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niipongeze na niiunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Salma Mohamed Mwinjuma sasa anafuatia Mhe. Ali Khamis Bakar.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha siku ya leo tukakutana hapa tukiwa wazima wa afya njema, vile vile tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tumalize shughuli zetu za mkutano huu wa Baraza, tumalize salama sote tukiwa wazima.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika bandari bubu. Kwanza naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuratibu shughuli hizi za kuzindua hizi bandari bubu ambazo zinaingiza mambo ya madawa ya kulevya, vile vile zinaleta uhalifu katika nchi yetu na sehemu wanazoishi wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni shuhuda katika Wilaya yetu ya Micheweni huu mpango upo katika Wilaya yetu kwenye bandari ambayo imeambiwa itajengwa pale Shumba Mjini. Kwa kweli bandari hii ikijengwa pale Shumba Mjini basi kwa kiasi kikubwa itaweza kuondoa zile kero na mahitaji ambayo wananchi wanakuwa wanayapata kwa masuala mazima ya dawa za kulevya. Vile vile itaweza kuondoa yale matatizo ya usafiri kwa wale wenzetu ambao wanakwenda Kenya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze sana serikali Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikuja pale Wilaya ya Micheweni katika Jimbo la Micheweni, kijiji cha Shumba Mjini akenda akaona hali halisi zaidi inavyokuwepo na wageni wanaoingia na hata wale wenyeji ambao wanaitumia bandari ile na akasema kwamba si kipindi kirefu ile shughuli itaanza. Mimi nilikuwa niulize tu Mhe. Mwenyekiti, sijui katika mpango huu wa bajeti hii 2018-2019 ndio hii bandari itajengwa ama vipi?

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe tu Mhe. Waziri atakapokuja nipate jawabu kuhusiana na bandari hii ni lini itaanza kwa sababu bado ile kadhia ya upitishaji wa madawa ya kulevya katika zile bandari bubu basi na ukanda wetu ule wa Micheweni tumeona zaidi kule Tumbe, na pale Micheweni, Shumba Mjini vile vile Kiuyu Maziwa Ng'ombe na sehemu nyenginezo. Ni vyema maeneo haya yakaanza kudhibitiwa mapema kabla ile hali haijaendelea siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niipongeze tena Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuratibu shughuli hizi za masuala ya *TASAF*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika kipindi ambacho nasoma skuli nilikuwa nasomea mabuku mawili yalikuwa yanakatwa vipande ili naweza kupata kwa ajili ya kuandikia. Mhe. Mwenyekiti, katika kuja habari hizi za masuala ya *TASAF* zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza hali halisi ya umasikini katika majimbo yetu. Mimi nimetembelea katika jimbo langu la Tumbe nimepita katika skuli zangu zilizomo ndani ya jimbo nimeangalia wanafunzi waliopo katika skuli nimekuta asilimia 85 basi matatizo ya wanafunzi yameondoka. Kwanza kwa kuanza kupata viatu vile vile kuweza kupata sare pia hata masuala mengine ya mabuku. Kwa kweli suala hili ni zuri na nalipongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mimi napata masikitiko kidogo katika suala hili la *TASAF III* ambayo imekuja kuwasaidia zile kaya masikini. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo zuri pesa zinaletwa kwa ajili ya kupewa wale wazazi wetu kwa kweli zinawafikia wale wanaostahiki wanapewa. Lakini kuna tatizo moja ambalo mimi nimeliona naiomba niishauri serikali hapa kutokana na hizi pesa jinsi zinavyotolewa.

Mhe. Mwenyekiti, wazee wameambiwa waunde vikundi ambavyo vitawasaidia kama ujasiriamali. Lakini ujasiriamali ule Mhe. Mwenyekiti wameambiwa wapande kama mikoko ama masuala mengine ili kuweza kupata pesa. Kwa mfano, kama mtu atakwenda kwenye upandaji wa mikoko labda kwenye wiki atahesabiwa siku zake alizokwenda atakuwa anaekewa zile pesa kwa ajili ya kuweza kufanikisha lile suala ambalo anaendana nalo labda pengine kwenye ule mradi kuweza kukamilisha. Mhe. Mwenyekiti, masikitiko

yangu hizi pesa kupitia hivi vikundi vingeundwa kwa vijana ambao wana uwezo na nguvu za kuweza ile mikoko, sio wazee ambao wameshafikia miaka 70 na 80 na wengine wana miaka 100 ukawaambia wakapande mikoko hali zao ni wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, zile pesa zimeletwa katika mazingira ambayo zitawasaidia kuwakwamua na matatizo, leo wazee wanaondoka kipindi hiki cha mvua na masuala mengine wanakwenda kwenye mikoko wanatafuta zile mbegu wanakwenda kupanda na vizee. Najua wanataka zile pesa kwa ajili ya mambo yao yaende vizuri na familia zao ziweze kupata mahitaji. Sasa mimi hapa nilikuwa naishauri serikali hizi pesa kama kuna namna nyengine yoyote ya kufanya wangeambiwa wakashauriwa hawa wazee wakaweza kuingiziwa hizi pesa zikawasaidia katika mazingira yao yanaonekana kwamba haya hayatokuwa matatizo na hayatokuwa hatarishi ili kuweza kuzipata zile pesa na badala yake isiwe ile kwamba waunde vikundi kwa ajili ya kupanda mikoko na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika suala zima la maafa. Mhe. Mwenyekiti, mimi napata masikitiko sana siku hadi siku zinavyoendelea Zanzibar imekuwa kama ni kioo watu tunaitana hasa jamani mvua tayari twendeni tukaangalie Tomondo, jamani twendeni tukaangalie Mwanakwerekwe yaani imekuwa kama maonesho.

Mhe. Mwenyekiti, kuna haja sasa ya kujipanga serikali kuona kwamba yale maeneo hatarishi najua inajitahidi serikali yangu siku hadi siku kuweza kupunguza, lakini kuna baadhi ya maeneo yamekuwa ni kero hadi siku zinavyoendelea imekuwa hata usafiri sasa hivi mtu anayetoka Bububu kuja mjini kufika kwake basi inakuwa ni mtihani. Vile vile watu wanaotoka Fuoni kuja mjini kufika kwake inakuwa ni mtihani masaa yanakuwa mengi kiasi ambacho yale maafa yamekuwa makubwa mpaka barabara hazipitiki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na ushauri tu kwamba kama itawezekana hata hizi daladala pamoja na gari zetu za *private* maeneo ni mawili. Kuna eneo la Nyarugusu kupitia Kijitoupele kwa Mhe. Ali Suleiman Ali labda ningesema kwamba daladala zipitie kule, ili gari za *private* zinazotoka Fuoni kuja mjini basi zipitie Nyumbambili. Mhe. Mwenyekiti, lakini tunapoteza muda pale Nyumbambili kuja mjini au kuja makazini masaa yanakuwa mengi, daladala humo humo, gari za *private* humo humo, baiskeli na wanaokwenda kwa miguu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa napendekeza hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nikitoka hapo nije Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba. Kwanza naipongeza sana serikali na nipongeze sana jambo hili kuona kwamba katika kipindi hiki cha 2017/2018 kumetengwa pesa ambazo zilitakiwa kujenga ile ofisi na mara hii vile vile kumetengwa pesa kwa ajili ya kuiboresha.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo zuri kwa sababu mimi ni shuhuda nakaa kule Pemba na nakwenda katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa kweli ile hali ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hairidhishi hata barabara ukitoka pale eneo la hospitali kuelekea Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilipo, kwa kweli sio nzuri lakini vile vile miundombinu rafiki ya ile ofisi sio mazuri. Nashukuru sana kwamba kusikia katika bajeti hii kumetengwa fedha ambazo zitaendeleza lile jengo ni jambo zuri, lakini hata vile naona

imani kwamba litakapojengwa lile na hata miundombinu bora inayohusiana na barabara najua itakuwepo. Hata wananchi ambao itapita barabara hii kuelekea katika ofisi hii basi watafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye suala zima la masuala ya barabara ambayo itajengwa kutoka Mjini kuelekea Bububu. Mhe. Mwenyekiti, jirani yangu hapa alisema kuhusiana na barabara ile kwamba izingatie kiwango kikubwa kuona kwamba kuna baadhi ya magari ambayo yanapita katika barabara zile yanakuwa mazito kiasi ambacho barabara ile inabomoka. Mhe. Mwenyekiti, lakini mimi nataka nisijikite hapo niende katika suala zima la masuala ya fidia.

Mhe. Mwenyekiti, najua serikali ina adhma nzuri ya kusaidia wananchi wake waondokane na matatizo ambayo yanajitokeza katika hali zote zinazokuwepo kuanzia afya, elimu, barabara na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, lakini mimi nashauri jambo la mwanzo lizingatie masuala mazima ya ulipaji wa fidia, kwa sababu imekuwa kero kwa baadhi ya sehemu nyengine ambazo zinapita barabara wananchi wanalalamika barabara imemalizika lakini fidia za wananchi wale mtu anafika pahala ya kutaka kujiua.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nimemsikia Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf anasema kuna mtu katika jimbo lake alifikia hatua ya kusema anataka kujiua kwa sababu hakupata zile fidia na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana serikali kwa jambo hili lakini nasema tu kwamba tuangalie miundombinu rafiki ambayo itawasaidia wananchi hawa kuweza kupata zile fidia zao ili kuondokana na matatizo haya ambayo yanajitokeza siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye masuala ya watu wenye ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika barabara zetu ambazo zitajengwa na mimi nawapongeza wenzangu na naungana nao mkono kuona kwamba katika maeneo haya yaliyotajwa na wao wamechangia, lakini na mimi kwa upande wangu nachangia kwamba watu hawa wenye ulemavu waangaliwe na hususan kuwe na elimu maalum ambayo itakusanya. Mhe. Mwenyekiti, nimwambie Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kaka yangu Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kwamba kuna haja hasa ya hawa madereva kufanyiwa elimu wiki hadi wiki au mwezi kwa siku moja kuweza kuitwa hasa kama mkutano kuambiwa kwamba jamani katika barabara zetu tunazotumia kuna wenzetu wenye mahitaji maalum tuwaangalie tusiendeshe tu magari yetu au vespa zetu kwa mwendo wa kasi na vile vile tuzingatie katika yale maeneo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi tulipokwenda Dodoma kwa kweli nilipata kujifunza tunakwenda katika maeneo ambayo yamewekwa zile zebra basi gari inasimama, nikajiuliza hivi inasimama hii gari kwa maana gani na hapana mtu anayekatisha. Lakini wenzetu wanajali kama mazingira haya au maeneo haya kutapita watu wenye ulemavu au kuna ng'ombe watakatisha yaani ni sehemu ambazo zilizowekwa alama maalum kwa matumizi ya wenzetu au viumbe hai basi wenzetu wanajali. Lakini hapa mtu anaziona zile alama za barabarani yeye vile anavyoiona basi ndio anakoleza vespa yake au gari yake. Kwa hiyo, kuna haja Mhe Mwenyekiti ya madereva yetu pamoja na sisi ambao tunatumia vyombo tuangalie mazingira halisi ya kuweza kujua wenzetu hawa wenye mahitaji maalum

kuweza kuwasaidia, vile vile kujua kama hapa wanaweza wakakatisha kuweza kupunguza ule mwendo wa kasi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikimalizia nije katika suala la afya. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza serikali kwa adhma yake kubwa ya kuwaondoshea wananchi matatizo. Nipongeze tu kwamba katika Jimbo langu la Tumbe hususan Shehia ya Sizini nimebahatika kujengewa kituo cha afya pale kizuri ambacho kitatoa huduma kwa wananchi wa Sizini wote. Mhe. Mwenyekiti, lakini nilikuwa niulize tu katika kipindi hiki cha 2017/2018 na 2019 sijui ni lini kituo hiki kitakamilika ili kuondoa ile kero ambayo wanaipata wananchi wa Sizini kwa sababu lile jengo ambalo tunatumia kwa kweli hali yake sio nzuri na haina mazingira rafiki kama hayo tunayosema kwa watu wenye ulemavu, lakini hata sisi ambao tuko wazima basi hali hairidhishi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Ali Khamis Bakar sasa namwita Mhe. Hidaya Ali Makame na kwa muda wetu uliobakia atamalizia Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuichangia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nianze kwa kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa juhudi zake kubwa anazozifanya. Lakini pia nimpongeze kwa dhati Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wao wote kwa kazi kubwa wanazozifanya na kusaidiana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kufanya yale yote ambayo yanahusika katika wizara hii lakini pia katika Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi, Mwenyekiti na Makamu pamoja na wajumbe wake wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kushirikiana bega kwa bega na ofisi hii, lakini na kazi zote zile ambazo wamepangiwa katika kamati yao. Niwapongeze na niwaambie kwamba wahongere sana kwa kazi kubwa waliyoshirikiana kukamilisha mpaka kufikia kuandaliwa kwa hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wakiwa bega kwa bega na wao.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenda kwenye mchango wangu moja kwa moja nainze kwenye Tume ya Madawa ya Kulevya. Kwanza niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuhakikisha kwamba suala hili linafanyiwa kazi, lakini pia kwa kuona kwamba suala la madawa ya kulevya ni janga kubwa hususan kwa sisi vijana.

Mhe. Mwenyekiti, suala la madawa ya kulevya wanaoathirika zaidi ni vijana, asilimia kubwa ukiangalia katika watu ambao wanaathirika na madawa ya kulevya vijana ni wengi zaidi wa kike na wa kiume.

Mhe. Mwenyekiti, tunaweza kudhibiti madawa ya kulevya ndani ya nchi yetu na niwapongeze pia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuliona hili na kulizungumza ndani ya kitabu hiki kwa upana zaidi na kwa ufanisi. Lakini pia niseme kwamba bado suala hili ni changamoto hususan ukiangalia katika mikoa yetu ya Unguja na Pemba, lakini hasa nitauzungumzia Mkoa wa Kusini na Kaskazini Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kudhibiti maeneo ambayo yanapita madawa haya ya kulevya basi suala hili kwetu bado litakuwa ni changamoto na litaendelea kutuathiri kila siku tukawa tunalizungumza hapa.

Mwaka uliopita kama sijakosea pia niliwahi kulizungumza suala hili kwa kupitia bandari bubu ambazo zimo ndani ya vijiji vyetu, shehia zetu au ndani ya wilaya zetu. Katika mkoa unaoongoza kwa hizi bandari bubu ikiwemo na Kaskazini hususan katika maeneo yote ya ukanda wa mahoteli ikiwemo Nungwi, Kiwengwa, Matemwe na kwengineko. Mheshimiwa hizi shughuli huko ndiko zinakofanyika kiufu pia na hizi njia ndiko zinakotumika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutoa mafunzo tu kwa tume au kwa watu mbali mbali hapa itakuwa hatujafanya dawa, dawa ni kuzidhibiti hizi njia ili madawa haya yasiweze kupitishwa kuingia ndani ya nchi yetu. Sasa hivi hazitumiki ndege ambazo zinakuja *airport* au maboti ni asilimia chache sana, sasa hivi zinazotumika hasa ni bandari bububu. Kwa hivyo, ili tudhibiti suala hili na hizi bandari tuzidhibiti na pia tuwe makini muda wote kuhusiana na suala hili la uingiaji mchana, usiku, jioni, magharibi na muda wote. Tuwe makini na tuhakikishe kwamba usalama upo katika ulinzi na kufuatilia juu ya suala hili la uingiaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja moja kwa moja kwenye suala la mabadiliko ya tabianchi. Mhe. Mwenyekiti, mabadiliko ya tabia ya nchi ni suala ambalo linaendelea kila siku tofauti miaka ya 1960 ambapo wengine hata ilikuwa hatujazaliwa na sasa hivi tulivyo ndani ya nchi yetu. Ukweli ni kwamba mabadiliko ya tabia ya nchi ni kitu endelevu kinachoendelea kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kumeonekana mazingira ndani ya miji na vijiji hayako vizuri na yanahatarisha afya zetu, yamezungumzwa maradhi ya kila aina ambayo yanapatikana ndani ya nchi yetu sasa hivi ambayo mengine hata hatuyafikirii, majina yake hata kuyataja mdomoni huwezi. Sasa hivi yanapatikana ndani ya nchi yetu hii kwa kupitia mazalio ya mbu na vitu vyengine ambavyo haviko kwenye mazingira mazuri. Lakini pia sasa hivi mvua ndogo ndani ya nchi yetu inakuwa athari yake ni kubwa zaidi tofauti na hapo mwazo ilivyokuwa.

Mhe. Mwenyekiti, ukiachilia mvua hata jua kali pia linaathiri zaidi kwa miundombinu na vianzio vyengine tafauti vinavyoleta mahitaji maalum kwa binadamu. Sasa hivi mvua ikinyesha kukiwa na umwesa na radi kidogo basi utasikia hali zimeshabadilika na mtu keshazikwa pengine kashituka kwa mshituko wa radi. Kwa sababu radi inapopiga ule mshituko ukigonga juu ya bati kama una maradhi ya *pressure* inakuathiri unaweza kupata mshituko unaanguka unapoteza maisha na hii yote inakuja kutokana na hali ya tabianchi

kutokuwa na kwamba ndani ya miji yetu hatuna miti ambayo inazuia baadhi ya vitu. Lakini pia mazingira ambayo tunaishi nayo sasa hivi kiufupi ni ya hatarishi kwa sababu miti tunaikata ovyo lakini pia miundombinu ya kila kitu tunaharibu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niligusie pia suala la miundombinu. Hivi karibuni tunatarajia kupata barabara mpya nadhani, Mkoa wetu wa Kaskazini kutoka Bububu mpaka Mkokotoni.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana likaangaliwa suala hili wakati wa utengenezaji wa hii barabara miundombinu ikaimarishwa zaidi kwenye maskuli lakini pia kwenye sehemu ambazo kama kuna masoko yaani mikusanyiko ya watu kwa kuweka *zebra* na matuta na kila kitu. Kwa sababu linaonekana kwamba suala hili huwa wanafanya lakini baada ya kufutika vitu hivi kama *zebra* ikishafutika tena watu wanakuwa hawafuatilii tena kuweza kuzirejesha *zebra* zile wakati ni kitu muhimu na kiwe kinaendelea kila siku kuwepo. Kwa sababu kile hata dereva anajua kama hapa pana *zebra* mtu anatakiwa akatishe, lakini ikiwa hamna zile *zebra* ni sawa kwamba unamruhusu yule dereva na madereva wetu wenyewe ndio hawa wa siku hizi humjui kijana, mzee, wala mwenye umri wa kati; huyo kizee ndio umuogope zaidi kwa mwendo wa kasi kuliko hata huyo kijana. Kwa hivyo, hili suala la *zebra* liangaliwe zaidi na matuta kwenye barabara na haya matuta yanapowekwa yaoneshewe alama yale mabango yawekwe yawe yanaonesha kwamba hapa pana kitu gani, hapa kanakuja tukio gani na pakoje.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia suala la madaraja. Mimi ningependa kulizungumza hili suala la madaraja ndani ya barabara yetu hii itakayotengenezwa, kuna madaraja si chini ya matano pale. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, haya madaraja nayo yakawekwa katika hali ambayo kukawa kuna mpishano wa magari kama daraja la Mwanakombo na Tingatinga pale yaliyotengenezwa hivi karibuni tunaona njia ya Donge, ni madaraja ambayo yako vizuri na ya kiwango. Kwa hivyo, madaraja yakiwa katika hali kama ile basi tutauepusha ule msongamano wa magari lakini pia tutaondosha ule uharibifu wa kila muda ikiwa madaraja yale yako kwenye hali ya mashimo kama sasa hivi yalivyo, kwa kweli inakuwa hali ambayo haiko vizuri na inatisha. Kwa sababu katikati ya daraja unakuta kuna shimo pembeni hujui gari uikwepeshe wapi, hujui uipitishe wapi ili unusurike na yale majanga ya kuingia ndani ya shimo na majanga ya kuingia ndani ya daraja ilimradi inakuwa ni mtihani. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana hapa huyo mkandarasi atakayejenga hizo barabara akazingatia namasuala haya na kusimamiwa na kufahamishwa kila mara kwamba masuala ya madaraja ayaangalie.

Pia ningependa nilizungumze suala la kipaumbele kwa wanafunzi ambao wenye mahitaji maalum. Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kwamba binadamu yeyote ni mlemavu mtarajiwa, lakini kuna hawa ambao tayari mfano mtu kazaliwa nao labda au hata kama umempata baadae ni udogoni ambapo tayari ni mtu mwenye mahitaji maalum. Mimi nitazungumzia hawa wanafunzi ambao wako kwenye mahitaji maalum lakini wanaendelea na masomo yao ikiwa ya kidato cha kwanza au *standard* au hata ya vyuo, ni wanafunzi ambao wanatakiwa waangaliwe kwa jicho la huruma kwa sababu mahitaji yao ni mengi na ni ya muhimu zaidi. Mwanafunzi mwenye mahitaji maalum ni tofauti na mwanafunzi wa kawaida, mwanafunzi wa kawaida anaweza akatumia njia zake zozote

akaweza kufahamu *lesson* au *topic* au chochote kilichozungumzwa ndani ya darasa na anaweza kumfuata mwalimu kwa njia zake mwenyewe akaweza kufahamu nini ambacho kasomeshwa. Lakini mwanafunzi mwenye mahitaji maalum na yeye ndio anahitaji vitu maalum alifahamu lile somo ambalo kasomeshwa.

Mhe. Mwenyekiti, cha kuzingatia hapa na cha umuhimu zaidi ni kuwaimarisha zaidi walimu ambao wanaweza kuwasomesha kwa kiwango cha juu wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kupatiwa vifaa, lakini pia na ile elimu ambayo inastahiki kusomeshwa mtoto mwenye mahitaji maalum. Mheshimiwa mtu ambaye unamfahamu kwamba huyu ana uwezo wa kusomesha mwanafunzi mwenye mahitaji maalum unamjua kwa kupitia vipimo vyake vya usomeshaji na ambaye hafahamu pia unaweza kumfahamu. Lakini sio leo mwanafunzi wa *primary* akamsomeshe mwanafunzi wa sekondari au chuo ambaye ana mahitaji maalum ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, mimi ningeomba sana hapa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ikaliangalia suala hili la walimu ambao wanasomesha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikitoka hapo niende kwenye suala la Mfuko wa Maafa. Mheshimiwa Mfuko wa Maafa umeelezewa ndani ya kitabu hiki na nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwa kulisimamia suala hili la maafa pia.

Mhe. Mwenyekiti, katika vipaumbele ambavyo vimewekwa humu kwenye maafa mimi sijui ufahamu wangu mdogo au sikui kiswahili changu mimi ndio cha Kinungwi sifahamu. Kuna ukurasa wa 32(52.0)(iii) kinasema: "Kuandaa mazoezi mawili ya kukabiliana na maafa".

Sasa unaposema kuandaa mazoezi ya kukabiliana na maafa hayo mazoezi sijui yanakuwa ya namna gani. Mimi labda ningeomba tu hapa Mhe. Waziri aje atufahamishe haya mazoezi ya kukabiliana na maafa yatakuwa yakoje, mimi sijafahamu mazoezi haya yatakuwa yanafanywaje ya kukabiliana na maafa. Kwa sababu maafa tunavyoyafahamu ni jambo ambalo hulijui wala hulitarajii litatokea vipi na litatokea wakati gani, sasa ukisema kwamba tunaandaa mazoezi ya kukabiliana na maafa mimi kwa kweli nakuwa napata mashaka kidogo kwa sababu sijafahamu haya mazoezi yatakuwa ya aina gani na yatafanywa vipi. Ila tu, mimi ninachoomba suala la maafa ni suala la kuangaliwa kwa hali nyengine, kwa sababu ni kitu ambacho wewe binadamu hujipangii wala hujui kitatokea muda gani.

Lakini ndani ya mfuko huu ambao umewekwa hapa wa fedha hizi na hili fungu ambalo limetengwa la kukabiliana na maafa ni pesa nyingi zimewekwa, lakini fedha hizi ambazo zimewekwa hapa mimi sidhani kama zinatosheleza kwa suala la maafa. Kwa sababu maafa ndio maafa na kila baada ya muda tunasikia leo maji wapi, leo mvua wapi, leo mti umepiga wapi, upepo wapi halafu baadae hatupati ile kujua sasa hivi pamesaidiwa kitu gani, pamesaidiwa vipi na vipi watu wamepata msaada juu ya Mfuko huu wa Maafa halafu tukapata mrejesho fulani hapa tukajua aa! kutokana na yale maafa yaliyotokea pahali fulani kwa hiyo wananchi wamesaidiwa vipi na kiasi gani kimetumika na vipi kimeendela. Lakini pia kuna maafa mengine ambayo Mwenyezi Mungu atusalimu salama, atunusuru, atulinde na atukinge ambayo ni makubwa zaidi yanaweza kupindukia

yakaathiri mfano asilimia kubwa ya binaadam, huwezi ukautumia mfuko huu kwa fedha hizi ambazo zipo hapa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tukiangalia kwa undani zaidi suala la maafa ni suala ambalo tunapaswa tulipe kipaumbele …

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemalizika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namalizia. Ni suala ambalo tunapaswa tulipe kipaumbele kwa kuitenga fedha ambayo inaweza kukidhi haja. Kwa sababu itakapokuwepo ikabaki haiozi ile wala haiharibiki itatumika kwa mara nyengine, ila ikiwepo itakuwa tayari imeshakuwa na fungu lake ambalo linafaa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache niseme na mimi naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuwa bega kwa bega na mawaziri wake wote na kuwapa moyo na ujuzi wa kuendelea kutenda kazi katika mawizara yao. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hidaya Ali Makame. Waheshimiwa Wajumbe kuna mabadiliko tena kidogo badala ya Mhe. Hamza Hassan Juma kumalizia muda wetu nampa nafasi Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kwa dharura maalum. Mhe. Mwanaasha karibu sana.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii niweze kuchangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, nami nimshukuru sana na pia nitoe pongezi zangu kwa Mhe. Makamu wa Pili kwa hotuba yake lakini nije moja kwa moja katika kitabu cha hotuba ya mapato katika suala zima la masuala mtambuka ambayo yamezungumza mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze serikali kwa kutuletea ile sheria ya adhabu na sheria ya mwenendo wa adhabu tuliyoipitisha hivi juzi na nimpongeze Mhe. Rais kwa kuitia sahihi sheria ile ili iweze kufanya kazi na kuwaondoshea matatizo wananchi wake. Lakini pia nitoe wito Mhe. Mwenyekiti, kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kuwaelimisha wananchi wetu juu ya sheria ile na wao wapate uelewa wa sheria hiyo iweze kutekelezeka kwa urahisi.

Mhe. Mwenyekiti, katika masuala hayo mtambuka nije katika suala zima la kukabiliana na maafa. Katika hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika maeneo yaliyotajwa kuhusiana na maafa ikiwemo Tomondo, Ziwamaboga ambayo ipo katika Jimbo la Chukwani. Mimi nataka niiombe serikali bado lile suala ni kubwa na linaleta maafa siku hadi siku. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Makamu wa Pili suala lile basi katika mambo aliyoyaweka katika kipaumbele basi na lile liwekewe kipaumbele ili kuondosha ile athari ya pale ili wananchi wetu waweze kukaa kwa amani.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maafa kama sikosei ya aina mbili makubwa na madogo, lakini pia yanatokana na ujenzi holela katika mitaa yetu. Katika maeneo ya ujenzi holela pia yanakuwa yanasababisha maafa, lakini niiombe hii wizara kwa mtazamo wake waweze kusaidia katika eneo la pale Tomondo ulipojengwa msikiti yale ni maafa madogo, msikiti ule unaweza ukaleta maafa kwa wakaazi wa maeneo ya pale kwa sababu tayari maji ambayo yalikuwa hayakai sasa hivi yanatuama na kuingia katika majumba ya karibu ya wananchi wale. Kwa hivyo, ndio maana nikasema inawezekana kuna maafa makubwa lakini na haya maafa madogo yaweze kutibiwa kabla hayajafikia kuwa makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze tena hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika wizara hii kuanzisha hii Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Katika maelezo hapa wametoa mafunzo mbali mbali kuhusiana na suala zima hili la kuratibu na udhibiti wa madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani katika tume hii haiwezi kufanya kazi peke yake bila ya mashirikiano na vitengo tofauti vilivyokuwepo nchini kwetu. Mheshimiwa nimeona nizungumze hili kwa upana wake kidogo ili wizara ione au wajue kwamba katika hili wanafanya kazi watu wengi na tuangalie katika kile kitengo cha madawa ya kulevya kilichokuwepo pale Jang'ombe.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kile nacho kinafanya kazi kwa kusaidia tume hii lakini niiombe wizara wakiangalie kile kitengo kwa jicho lake la huruma. Kwa maana hiyo, kuna changamoto nyingi katika kitengo kile, kwanza tukiangalie tu lile jengo lenyewe halina hadhi ni la zamani sana, halina hadhi hasa ya kuwa Kitengo cha Madawa ya Kulevya na tukiangalia hawa waletaji wa madawa ya kulevya ni watu wenye pesa. Kwa maana hiyo, kama pale hapajaboreshwa katika vitendea kazi au katika kufuatilia yale mambo ya madawa ya kulevya basi inawezekana wakarubuniwa.

Kwa hivyo, nilikuwa naiomba serikali kupitia wizara hii kile kitengo wakiangalie kwa jicho la huruma na jicho la huruma lenyewe hawana vitendea kazi ukiwemo usafiri. Kwa hivyo, naomba sana katika bajeti hii waliangalie na hilo ili tuone kitengo kile kinafanya kazi vizuri pamoja na hii Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, pia nipongeze sana hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa jitihada zao kama Mtendaji Mkuu wa Serikali katika Wizara hii kwa mambo mbali mbali ambayo wameainisha humu ikiwa katika Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na mambo mengine. Lakini bado ipo haja katika hili waweze kushughulikia yale mambo ya Wizara ya Afya kama ni watendaji wakuu wa serikali kwa sababu tayari Wizara ya Afya pia na Elimu ina changamoto nyingi sana hususan madaktari, ma-*nurse* pamoja na wafanyakazi wengine tofauti.

Pia kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa sababu bado ofisi hii inafanya kazi ya serikali, kwa maana hiyo, bado katika Wizara ya Elimu nayo pia waangalie suala zima la elimu. Walimu ni kidogo na kila sehemu, kila mara ukienda

unakuta tatizo la walimu bado liko pale pale. Kwa hivyo, naiomba sana ofisi hii iweze kushughulikia mambo hayo kwa umakini wake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona nichangie haya ambayo kidogo nilikuwa ninayo ili kuiambia wizara hii husika waone hali halisi katika utendaji wao wa kazi. Nawashukuru sana, nawapongeza sana na naunga mkono Hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa asilimia mia moja. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwanaasha Khamis Juma. Waheshimiwa naomba niwataje wachangiaji wa kesho tukijaaliwa asubuhi tutaanza na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mohamed Said Mohamed akifuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa. Hao watakuwa wachangiaji wa kesho asubuhi penye majaaliwa. Baada ya hapo nichukue fursa hii kuwashukuru kwa utulivu wenu na michango yenu mizuri juu ya hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na hadi hapa naliakhirisha Baraza mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 10/05/2018 saa 3:00 asubuhi)